

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA SABA**

**Kikao Saba – Tarehe 4 Novemba, 2009**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Job Y. Ndungai ) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na Waziri Mkuu:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:-**

Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya ya Mwaka 2008.

Taarifa ya Mwaka wa Hesabu zilizokaguliwa za Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa kwa Mwaka 2007/2008 *(The Annual Report and Audited Accounts of Local Authorities Pension Fund of the Year 2007/2008)*.

Taarifa ya mwaka ya Shirika la Elimu Kibaha kwa Mwaka 2007/2008 *for the Year (2007/2008)*.

**MWENYEKITI:** Maswali ya leo tunaanza na ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ina maswali manne. Tunaanza na swali la kwanza Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya.

Na. 68

**Wagombea Urais Wawakilishi Ndani ya Bunge**

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ina mpango wa kuleta mabadiliko na Sheria ya Uchaguzi kufuatia taarifa iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri Mkuu katika hotuba yake ya Bajeti; kawa kuwa Bunge ndiyo chombo kikuu kinachotunga Sheria na kuamua juu ya mustakabali wa maisha ya Watanzania:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa kuna haja ya kuweka kifungu kinachoruhusu wagombea Urais wote watakaopata asilimia tatu hadi tano ya kura za Urais kuwa wawakilishi ndani ya Bunge kama nchi nyingine ili kutimiza matakwa ya demokrasia?

(b) Je , Serikali haioni kuwa Sheria hiyo ikiwaruhusu wagombea Urais hao kuwa wawakilishi itasaidia kuchangia mawazo katika yale yaliyowasukuma kugombea nafasi hiyo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Serikali ina mpango wa kuleta Bungeni mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Uchaguzi. Mapendekezo ya Marekebisho hayo ya Sheria ya Uchaguzi yana lengo la kuondoa kasoro mbalimbali zilizojitokeza katika mchakato wa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005 na chaguzi ndogo zilizofanyika baada ya Uchaguzi Mkuu huo. Madhumuni makubwa ya marekebisho hayo ni kuiwezesha Tume ya Taifa ya Uchaguzi kuendesha mchakato wa uchaguzi kwa wepesi na ufanisi zaidi hasa kwa kuwa Sheria za uchaguzi zinahusu zaidi mambo ya mchakato wa uchaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuweka kifungu kinachoruhusu wagombea Urais wote watakaopata asilimia tatu hadi tano ya kura za Urais kuwa wawakilishi ndani ya Bunge ni suala la Kikatiba. Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya mwaka 1977 inatamka bayana aina ya Wabunge na sifa za kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jamhuri ya Muungano. Namshauri Mheshimiwa Mbunge kukubali wagombea wajijimarishe kuwania ushindi na siyo kulenga kuwa wawakilishi wa vyama Bungeni kwa kuwa washindi wateule watakuwa wamepatikana na kujaza nafasi zote kwa mujibu wa Katiba.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mhonga maswali.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amesema kwamba hili ni suala la Kikatiba ni kweli. Sehemu ya pili ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano inaainisha aina za Wabunge na sifa zao, kwa kuwa sifa za kuchaguliwa kuwa Mbunge hazitofautiani sana na sifa za kugombea Urais ila tofauti inawezekana ikawa kwenye umri.

Je, Serikali haioni kwamba mchakato wa mabadiliko ya Katiba utakapoanza kuna haja ya kuainisha aina ya hii ya Mbunge anayetokana na kura za Urais?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili Serikali haioni kuwa kuna haja basi ya mgombea Urais akaruhusiwa pia kugombea Ubunge kama nchi nyingine zinavyofanya ili apate uwakilishi ndani ya Bunge. Kwa sababu anapomaliza tu kugombea nafasi ile huwa ni kama anamaliza ile kazi halafu basi, wakati hali ya kidemokrasia inahitaji sifa moja wapo ni kuwa na uwakishi mpana na wa watu wa aina mbalimbali. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mhonga unataka kugombea hiyo nafasi? Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri Mkuu naomba kumjibu Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya maswali yake ya nyongeza kama ifuatavyo.

Kama nilivyosema hapo awali kwa sasa Katiba inaainisha aina maalum ya Wabunge na aina ambayo anaitaja yeye ya Wabunge ambao walikuwa Wagombea wa Urais kwa sasa haipo, iwapo kutakuwa na haja ya kuwa na Wabunge wa aina hiyo wakati wa mchakato huo basi hoja hiyo itajadiliwa kwa utaratibu unaohusika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili kila nchi ina historia yake na kila nchi ina taratibu na kanuni zake za uchaguzi. Kwa Tanzania tofauti na nchi nyingine za jirani kwa mfano nchi kama ya Kenya, mgombea Urais au Rais siyo Mbunge na hakujawa na haja kama hiyo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea swali linalofuata Mheshimiwa Vedastusi Manyinyi, Mbunge wa Musoma Mjini.

Na. 69

### **Ujenzi wa Hospitali ya Kwangwa**

**MHE. VEDASTUSI M. MANYINYI** aliuliza

Kwa kuwa Serikali iliamua kutoa Hospitali ya Kwangwa na Baba Askofu wa Kanisa Katoliki aweze kumaliza ujenzi na kuiendesha kwa kuwahudumia wananchi:-

(a) Je, ujenzi na uendeshaji wa Hospitali hiyo utanza lini?

(b) Kwa kuwa nguvu za wananchi zilitumika kwa ujenzi wa hospitali hiyo, je, Serikali haioni kuwa kutokuanza kwa ujenzi huo kunawakatisha tamaa wananchi waliojitolea nguvu zao?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA  
NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Vedastusi Mathayo Manyinyi, Mbunge wa Musoma Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa ujenzi wa Hospitali ya Kwangwa ulianzishwa na Chama Tawala katika miaka ya 1970 kwa nguvu za wananchi wakiwemo wafanyakazi, wakulima na wafanyabiashara ambao walichangia si chini ya asilimia moja ya mapato yao na pia kupitia kwenye manunuzi ya bidhaa adimu kwa wakati huo. Michango hiyo iliendelea kwa kipindi kisichopungua miaka mitano, mradi ulianza kutekelezwa kwenye kiwanja Na. 374 chenye ukubwa wa hekta 62.8 katika eneo la Kwangwa, Musoma Mjini. Ujenzi ulisimama baada ya michango kusitishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2007 uongozi wa mkoa wa Mara ulianza mchakato wa kufufua ujenzi wa Hospitali ya Kwangwa kwa kuwatafuta wabia wa kujenga hospitali hiyo. Kwa bahati nzuri Kanisa Katoliki jimbo la Musoma lilionyesha dhamira ya kujenga Hospitali maalumu kwa ajili ya huduma ya Uzazi na Afya ya Mtoto (*Reproductive Health*). Mradi huo ulikuwa unasimamiwa na Hayati Baba Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu la Mwanza kwa kushirikiana na Jimbo Kuu la Musoma. Mchakato ulikuwa ni kwamba Katibu Tawala Mkoa apate hati ya kumiliki eneo na hatua ambayo ingefuata ingefuata ni kukabidhi mradi kwenye umiliki wa kanisa Katoliki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 9 Agosti, 2007 Katibu Tawala wa Mkoa wa Mara alipewa hati ya kumiliki eneo la hospitali. Aidha, kwenye eneo kulikuwa na mali za watu ambazo kulingana na tathmini iliyofanyika tarehe 25 Januari 2008 ziligundulika kuwa na thamani ya ya shilingi 30,130,809.30. Mawasiliano ya Ofisi ya Jimbo Katoliki Musoma yamebaini kuwa dhamira ya kujenga na kuendeleza mradi wa hospitali bado ipo, kinachoendelea ni kutafuta fedha za fidia pamoja na fedha za ujenzi .

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutowakatisha tamaa wananchi Serikali imeendelea kutoa pesa kwa ajili ya ukarabati wa hospitali ya Mkoa wa Mara ambayo ndiyo ya rufaa kwa mwaka 2007/2008 Serikali ilitoa kiasi cha shilingi 600,000,000/= kwa ajili ya ukarabati wa Hospitali ya Mkoa wa Mara. Aidha, kazi ambazo zimefanyika ni pamoja na jengo la upasuaji, wodi ya daraja la kwanza, huduma ya mama na mtoto na ukarabati wa wodi ya watoto. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2009/2010 Serikali imepanga shilingi 350,000,000/= kujenga chumba cha kuhifadhia maiti (*mortuary*), kununua majokofu, kukarabati mfumo wa maji safi na maji taka, kupata *transforma* ya kugawa umeme wa uhakika hospitalini na kuimarisha eneo la kuingia hospitalini kwa kuweka lami. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Manyinyi swali la nyongeza.

**MHE. VEDASTUSI M. MANYINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Waziri amekubali kwamba mchakato wa kuipatia hospitali hii Kanisa la RC ulianza mwaka 2007 na hadi sasa hospitali hii bado haijakabidhiwa kwa Kanisa Katoliki kwa sababu uthamini ulifanyika na fedha hazikulipwa, na kwa kuwa tunatambua kwamba Makanisa yote huwa hayafanyi biashara isipokuwa yanatoa huduma, lakini kwa Serikali kuchelewa kulipa fedha hizo sasa uthamini unatakiwa kufanyika upya. Je, Serikali haoni kwamba imesababisha uzembe kwani uthamini ukifanyika upya hizo gharama zitakuwa si milioni 30 tena isipokuwa zitakuwa zaidi ya hizo?

Na kwa kuwa Kanisa Katoliki kama Serikali ilivyoahidi kwamba ingewakabidhi hati na wao wako tayari kuanza ujenzi huo, na hati hawajakabidhiwa kwa sababu ya hili deni la fedha za fidia napenda kufahamu ni lini Serikali itaweza kulipa hizo fidia mara moja ili ujenzi huo uanze mara moja?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Vedastusi Manyinyi kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala ya fidia katika miradi yote karibu ni nchi nzima hata inayofadhiliwa na wafadhili hata na wabia wa maendeleo pamoja na taasisi binafsi mara nyingi fidia hutolewa na Serikali. Mimi nilikuwa napenda kumhakikishia tu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali ipo tayari kutoa fidia ili huo mradi uweze kuanzishwa, kwa kweli milioni 30 kwa Serikali ni fedha ndogo sana na mimi nimeahidi kwamba sisi tutalitekeleza hilo ili hospitali iweze kuendelea. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Rosemary Kirigini, swali la nyongeza fupi.

**MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kuniona, kwa kuwa ujenzi wa hospitali hii ulionekana kupamba kasi sana wakati akiwepo Waziri Mkuu Mheshimiwa Edward Lowassa na nafikiri wenzangu wa mkoa wa Mara watakubaliana nami. Lakini baada ya Mheshimiwa Edward Lowassa kuondoka basi ni kama ujenzi huu sasa umesitishwa na wananchi wa Mara na Wabunge wao sisi hatujui hatma ya hospitali hii ningependa Mheshimiwa Waziri atuambie na ni lini hospitali hii hospitali hii itaanza kujengwa na ni lini fidia hii ndogo italipwa na Wizara na Serikali asante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapochukua madaraka katika ofisi hii tunachukua na mambo yote ambayo tumeyakuta katika ofisi hii na hatuwezi

tukayaacha kwa sababu yalianzishwa na mtu fulani. Mimi nimhakikishie Mheshimiwa Rosemary Kirigini na Wabunge wa mkoa wa Mara kwamba fedha hizo tumesema kwamba tutazilipa na tutahakikisha kwamba hospitali hii tunawakabidhi na inajengwa, na tukumbuke kwamba kipindi hicho ambacho mchakato huu ulipamba moto sana aliyekuwa anasimamia suala hili au mradi huu ni Askofu ambaye amefariki, kwa hiyo, hapo napo kuna *gap* pia ya mawasiliano kwa yule ambaye atachukua mradi huo. Kwa hiyo, jamani siyo upande wa Serikali tu na pia upande wa misheni nako wana kikwazo baada ya Askofu kufariki. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali linalofuata ni la Mheshimiwa Sijapata Fadhili Nkayamba, Mbunge wa Viti Maalum, Kigoma.

Na. 70

### **Kubomoka Kwa Daraja la Kijiji cha Bitale - Kigoma**

**MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA** aliuza:-

Kwa kuwa katika kitongoji cha Nkuruba, Kijiji cha Batale, Kigoma Vijijini kuna daraja lililofunguliwa kwa mbio za mwenge mwaka 1995, na kwa kuwa sasa hivi daraja hilo limebomoka na wananchi wanapita upande mmoja na hivyo kupelekea adha kubwa hasa wakati wa kupitisha wagonjwa.

(a) Je, kwa nini daraja hilo liliachwa bila ya kuangaliwa licha ya kujulikana na kufunguliwa na mbio za mwenge?

(b) Je, ni lini sasa daraja hilo litatengenezwa ukizingatia mwaka 2010 ni mwaka wa uchaguzi na wananchi hutumia daraja hilo wakati wa uchaguzi mkuu?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sijapata Nkayamba, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, daraja la Nkuruba liko katika Kitongoji cha Nkuruba na lilijengwa kwa ushirikiano wa wananchi na na Shirika la *Caritas* na kufunguliwa na kiongozi wa mbio za mwenge wa Uhuru na Mheshimiwa Juma Seleman J. Kimea tarehe 9/9/1997. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, daraja hilo limekuwa likitoa huduma kwa wananchi tangu lilipofunguliwa hadi lilipokatika kutokana na mafuriko yaliyovunja kingo za daraja hilo mwaka 2008 na mpaka hivi sasa halijatengenezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Daraja la Nkuruba halijaacha kushugulikiwa na Halmashauri kwani ni kiungo muhimu cha wananchi wa kitongoji cha Nkuruba na shughuli zao za kilimo. Miradi mingi ya wananchi inapitia mchakato wa uibuaji chini ya

zoezi la fursa na vikwazo (*O&OD*). Hivyo daraja limeshaibuliwa na jamii ya Nkuruba na linajengwa kwa kushirikisha jamii kikamilifu, ili liweze kupitika. (*Makofi*)

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2009/2010 Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma imetengewa kiasi cha shilingi milioni 71.8 kwa ajili ya matengenezo ya madaraja na makalvati. Kati ya fedha hizo shilingi milioni 14 zitatumika mwaka huu 2009/2010 kutengeneza daraja hilo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sijapata swali la nyongeza.

**MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA:**Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Kwa kuwa wananchi wa Nkuruba katika kitongoji hicho wamekuwa wakipata adha ya kusafiri kwenda sokoni, na hospitali na wakati mwingine wamekuwa wakidumbukia humo na wanapata majeraha makubwa; na kwa kuwa mwaka 2010 una karibia na ni mwaka wa uchaguzi, sasa nilitaka kujua kama hili daraja halitatengenezwa nilitaka kujua na Waziri aniambie ni njia gani ambayo wataweza kupitia wakati wa uchaguzi? (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:**Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri Mkuu naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Sijapata Nkayamba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, daraja hilo kama alivyosema ni njia ya mkato ya kutoka kwenye kitongoji cha Nkuruba kwenda zahanati ya Bitale ninalifahamu. Ni kweli wakati wa mvua daraja hilo si rahisi kupitika linapitika wakati wa kiangazi kwa hiyo wakati wa masika wananchi yawapasa wazunguke kupita njia nyingine. Nimekwisha mhakikishia Mheshimiwa Sijapata Nkayamba kwamba daraja hilo litajengwa kwa hiyo, mwaka 2010. Hatungoji uchaguzi tu sisi tunafanya kazi zetu kwa mujibu wa Bajeti, kwa mujibu wa Sheria na hatungoji tu wakati wa uchaguzi ndipo tutengeneze ma daraja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la mwisho, Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu nalo linatoka kwa Mheshimiwa Martha Umbulla, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Manyara.

Na. 71

**Mikakati ya Kuboresha Huduma kwa Jamii za Wafugaji na Mikoa ya Pembezoni**

**MHE. MARTHA J. UMBULLA** aliuliza:-

Kwa kuwa kila mwaka Serikali hutenga fedha kwa ajili ya maendeleo ya jamii zilizo nyuma sana kimaendeleo:-

(a) Je, Serikali ina mikakati ipi ya makusudi ya kuelekeza nguvu katika kupelekea huduma za afya, elimu na nyinginezo kwenye jamii za wafugaji na Mikoa ya pembezoni?

(b) Je, Serikali imeunga vipi mkono kauli ya Rais Mheshimiwa Jakaya Kikwete na kusaidia zaidi jamii za kifugaji kama zile za Wahadzabe, Wabarbaig na jamii zingine za wafugaji zilizo nyuma kimaendeleo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijamjibu Mheshimiwa Martha Umbulla, swali lake lenye sehemu (a) na(b), kwanza niombe radhi kwamba yeye hakutaka swali lijibiwe na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, alitaka lijibiwe na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Lakini nimuhakikishie kwamba sisi wote ni Serikali kwa hiyo, majibu nitakayotoa ni majibu ya Serikali kwa hiyo, hata akiliuza swali la nyongeza tutalijibu kama Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi yetu jamii za wafugaji ziko katika Mikoa mingi ingawa kiwango cha maisha kina tofautiana ambapo baadhi ya Mikoa wakazi wake wanajishughulisha na kilimo cha mazao na ufugaji na wengine wamejikita zaidi katika ufugaji wa kuhamahama. Serikali imeweka mikakati mbalimbali na kuelekeza nguvu katika kupeleka huduma za jamii ikiwemo huduma ya afya, elimu na nyinginezo kwa jamii za wafugaji katika maeneo yao. Kwa mfano, kupitia mikakati wa Serikali wa kuwa na zahanati kwa kila kijiji na kituo cha afya katika kila kata itasaidia kusogeza huduma za afya kwa wananchi, ikiwa ni pamoja na kuboresha huduma za akinamama na watoto. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa huduma za elimu katika nchi yetu uko utaratibu wa jamii za wafugaji kujengewa mabweni kwenye baadhi ya shule za msingi na sekondari hususani kwa watoto wa kike mfano shule ya Sekondari ya Yaeda Chini iliyoko Mkoani Manyara.

Aidha, katika Mikoa ya Manyara na Arusha jumla ya shilingi 945,934,000/= zimetengwa katika Bajeti ya mwaka 2009/2010 kwa ajili ya kuendesha shule za bweni za watoto wa wafugaji katika Mikoa hii miwili. Halmashauri za Wilaya zina hakikisha upatikana wa chakula cha mchana kwa wanafunzi wa kutwa. Pia kupitia Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya (*DADPs*) Serikali inaendelea kuboresha na kuwajengea wafugaji mazingira mazuri ili wasihamehame kwa kujengea miundombinu ya mifugo.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuunga mkono kauli ya Mheshimiwa Rais ya kusaidia jamii za wafugaji kama nilivyoeleza katika sehemu (a) hapo juu, Serikali imefanya yafuatayo:-



Kwanza, mkoani Singida Halmashauri za Wilaya zimetenga maeneo ya malisho ya mifugo kwa jamii ya Wabarbaig na kuyawekea mipaka;

Pili, katika Mkoa wa Arusha umeweka mikakati wa kuwaingiza kwenye sekondari za bwani watoto wa Kihadzabe wanaofaulu mitihani yao ya darasa la saba. Kwa hivi sasa wapo wanafunzi 20 Kihadzabe wanaosoma sekondari ya Longido; na

Tatu, kwa upande wa Halmashauri ya Wilaya ya Karatu imejiwekea utaratibu wa kwenda kuchukua wanafunzi hao kwenye maeneo ya makazi yao, kuwapeleka shuleni na kuwarudisha wanapofunga shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuziendeleza jamii hizi Mkoa wa Manyara umeweza kujenga shule za msingi na shule mpya ya sekondari ya Yaeda Chini. Hali kadhalika harambee ya kuchangia mfuko wa elimu iliyofanyika mwaka 2008 mkoani Manyara ambapo zilipatikana shilingi 50,000,000/= zimetumika kujenga hosteli katika shule ya sekondari ya Yaeda Chini na kuziwezesha jamii za Wahadzabe kukaa shuleni kwa muda wote wa masomo. Aidha, Mkoa wa Manyara kwa kushirikiana na Shirika la Misaada la Uholanzi (SNV) na wadau wengine wa maendeleo umeunda kikundi cha kikazi (*Task Force*) kwa lengo la kuibadilisha jamii ya Wahadzabe ili ipate maendeleo ya kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri za Wilaya kwa kutumia mbinu shirikishi, Wahadzabe na Wabarbaig wameweza kuanza kujenga mabweni kwa ajili ya wanafunzi wa jamii hizo. Kwa mfano Halmashauri ya Wilaya ya Iramba katika Bajeti ya mwaka wa fedha 2008/2009 ilitenga shilingi 20,000,000/= kwa mwaka wa fedha 2009/2010 wanatarajia kutumia shilingi 30,000,000/= kukamilisha ujenzi wa mabweni kwa ajili ya wanafunzi wa jamii ya Wahadzabe na Wabarbaig. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Waziri, Waheshimiwa Wabunge sauti zimezidi kidogo tupunguze. Nina uhakika Mheshimiwa Philip Marmo angependa kuuliza swali la nyongeza kwa vile ni suala la Wahadzabe na Mheshimiwa Msindai. Lakini Mheshimiwa Marmo hataweza na Mheshimiwa Msindai utauliza swali baada ya Mheshimiwa Martha Umbulla. (*Makofi/Kicheko*)

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashukuru sana kwa maelezo ya kina na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri, na naipongeza sana Serikali kwa juhudi kubwa ambayo imeelekeza huko ya kujenga shule, zahanati na kadhalika lakini pamoja na majibu hayo nina swali moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa maeneo hayo ya jamii tajwa yana mazingira ambayo hayavutii hasa kwa walimu na wahudumu wa afya wanaopelekwa sehemu hizo. Je, Serikali itafanya juhudi ipi ya ziada ili kuhakikisha kwamba hizo shule zilizojengwa na zahanati na huduma nyinginezo zinakuwa na maana kwa ajili ya kupata watumishi na wahudumu wa kutosha?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:**Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Martha Umbulla kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema Serikali inajitahidi kujenga mazingira mazuri katika Mikoa yote iliyoko pembezoni na Wilaya zote zilizoko pembezoni pamoja na hizo Wilaya za wenzetu wafugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano katika ujenzi wa nyumba tunafahamu kabisa kule Kiteto tumejenga nyumba za watumishi kwa ajili ya kuweka mazingira vizuri na katika sehemu mbalimbali kuweka mazingira vizuri kama kujenga nyumba za watumishi kwa ajili ya kuweka mazingira vizuri. Longido katika Bajeti ya mwaka huu na Ngorongoro tumewapatia fedha kwa ajili ya ujenzi wa nyumba hizo za wafanyakazi, kwa hiyo, yote hiyo ni mikakati ya Serikali katika kuhakikisha kwamba tunajenga mazingira mazuri ili yaweze kuwavutia wafanyakazi pia na wananchi kwa ujumla kwa hiyo hilo la shule na kujenga mabweni pamoja na nyumba za wafanyakazi katika bajeti ya mwaka huu tumelizingatia na tumepeleka hasa kule kwenye sehemu zenye mazingira magumu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Swali la mwisho kwa Wizara hii Mheshimiwa Mgana Msindai.

**MHE.MGANA I. MSINDAI:**Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa tunaona jitihada za Serikali inavyofanya kuwasaidia wenzetu Wahadzabe na wafugaji wanaokaa majirani nao; na kwa kuwa Wahadzabe wako Wilaya za Iramba, Mbulu, Karatu na Meatu na kuwa mpaka sasa shule ya uhakika ya Wahadzabe wanaokaa bwenini iko Endamagani, Karatu. Je, Serikali sasa itakuwa tayari kuharakisha kukamilisha shule ya Wahadzabe Iramba kule Kipamba na Iramba ndogo kule Meatu ili wasiwe na matatizo tena na kwa sababu wameitikia wito wa Serikali wa kukaa pamoja? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mgana Msindai, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa wenzetu hawa kabila la Wahadzabe mpaka sasa hivi wamekubali kutohamahama na Serikali tunajitahidi kuhakikisha kwamba zile sehemu ambazo wamekaa pamoja tunatoa huduma zote za jamii, mimi niwaombe tu ndugu zangu ambao wametoka katika sehemu za wafugaji kwamba tukishajenga huduma za jamii, tukishajenga miundombinu katika sehemu fulani, ni vema wakawashauri hao wenzetu wanaohamahama wakakaa katika sehemu hizo. Nina mifano halisi baadhi ya sehemu tumejenga majosho lakini wafugaji wanahama wanaliacha josho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna baadhi ya sehemu tumejenga shule ndugu zetu wafugaji wanahama wanaacha shule, kwa hiyo, hilo nalo pia mliangalie Waheshimiwa Wabunge ili kuhakikisha kwamba hizi huduma za jamii zikishatolewa mahali fulani

hatuwezi tukazisambaza tena kwenda mahali fulani tukaanza kuhama nazo kutoka sehemu “a” kwenda nazo sehemu “b.” Naomba wenzetu wangukuwa wanakaa sehemu moja ili Serikali iweze kujipanga vizuri. *(Makofi)*

Na. 72

### **Jengo la Mahakama ya Wilaya ya Muleba**

**MHE. WILSON M. MASILINGI** aliuliza:-

Kwa kuwa Wilaya ya Muleba ilizinduliwa mwaka 1975 lakini hadi sasa mazingira ya Mahakama ya Wilaya yanasikitisha:-

(a) Je, ni lini Serikali itajenga jengo la mahakama lenye hadhi ya makazi ya mahakimu?

(b) Je, Serikali itatoa kipaumbele cha kwanza kama Halmashauri ya Wilaya ya Muleba itakuwa tayari kuchangia? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mwanasheria Mkuu wa Serikali, hayo ni makofi ya pongezi. *(Makofi)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kujibu la swali la Mheshimiwa Wilson Masilingi, Mbunge wa Muleba Kusini, naomba kwanza kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kusimama hapa kuchukua nafasi hii kutoa shukrani kwa Waheshimiwa Wabunge na kwa kuteuliwa kwangu na Mheshimiwa Rais kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Napenda kuwahakikishia Wabunge wote, wa aina zote, kuhusu ushirikiano wangu katika kutekeleza majukumu yangu. Ofisi yangu ambayo ipo katika ofisi za Bunge iko wazi kuanzia saa moja na nusu asubuhi mpaka saa tano usiku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo naomba sasa kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria kujibu swali la Mheshimiwa Wilson Masilingi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge ambaye ni mdau wa karibu wa sekta ya sheria na uongozi wa Wilaya ya Muleba kwa kuonesha nia ya kushirikiana na Serikali kujenga jengo la Mahakama Wilayani Muleba na hivyo kuboresha huduma za Mahakama Wilayani humo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni lengo la Serikali kujenga Mahakama pamoja na makazi ya Mahakimu katika ngazi zote. Kwa mfano, katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita Serikali imejenga Mahakama za Wilaya za kisasa katika Wilaya za Ludewa, Kongwa,

Mpwapwa na Hai ambazo zimeanza kutumika. Aidha, ujenzi wa Mahakama ya Wilaya ya Mafia unaendelea kwa kutumia fedha za Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kutokana na ufinyu wa Bajeti, Serikali inalazimika kutekeleza ujenzi wa Mahakama katika ngazi zote kwa kasi ndogo hivyo basi:-

(a) Kwa sasa Serikali haina mpango wa kujenga mahakama ya Wilaya ya Muleba pamoja na makazi ya mahakimu kutokana na ufinyu wa Bajeti. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa mara hali ya fedha itakaporuhusu, Serikali haitasita kujenga jengo jipya la mahakama Wilayani Muleba.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ipo tayari kukaa na Mheshimiwa Mbunge pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Muleba kwa lengo la kuangalia namna bora ya kujenga Mahakama ya Wilaya ya Muleba kwa kuchangia kama Mheshimiwa Mbunge alivyopendekeza katika swali lake.

Aidha, napenda kutoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge na Halmashauri za Wilaya kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa mahakama za ngazi zote. Kwa kufanya hivyo tutaweza kuboresha mahakama zetu pamoja na huduma zinazotolewa katika Mahakama hizo kwa manufaa ya wananchi. (*Makofi*)

**MHE. WILSON M. MASILINGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Jaji Frederick Werema, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kwa sababu mimi ni wa kwanza kumuuliza swali akajibu yeye nimhakikishie ushirikiano wangu na nilishampongeza. (*Makofi*)

(i) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imefanya kazi nzuri sana kujenga jengo la Mahakama Kuu Mjini Bukoba ambalo ni zuri sana na la kisasa, kwa hiyo Serikali inastahili pongezi kwa hilo. Kama alivyosema Mwanasheria Mkuu wa Serikali mimi ni mdau katika Wizara hii ya Sheria, kwa kuwa Serikali Kuu na Waziri Mkuu bahati nzuri yupo nikitoa mfano wa Wilaya ya Muleba shughuli zetu za Halmashauri ya Wilaya ya Muleba zinaendeshwa kwa ruzuku ya Serikali Kuu kwa takribani asilimia 95, kwa hiyo, mipango ikiwekwa ambayo wanasema haipo na maelekezo yakatolewa kwa Halmashauri zote yawezekana tukaweka kipaumbele ili jengo la Mahakama Kuu la Bukoba liweze kuwa na mahakama za kisasa zinazofanana na Mahakama Kuu, je, Serikali itaweza kutoa maelekezo hayo ili kusudi mipango iwepo na fedha kwa sababu zipo za ruzuku tuweze kuchangia kidogo kujenga majengo hayo? (*Makofi*)

(ii) Kwa kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa niaba ya Wizara ameonisha nia ya kukutana na mimi, kushauriana na mimi na ametualika tukae naye hata ikibidi saa tano za usiku, je, atakuwa tayari kukutana na mimi leo hii kabla ya saa tano za usiku,

mimi sitaki kukutana naye usiku, nataka leo mchana ili tuweze kuweka mipango na aishauri vizuri Serikali? (*Makofi/kicheko*)

**MWENYEKITI:** Pamoja na shukrani za wananchi wa Kongwa kwa jengo zuri la Mahakama ya Wilaya, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu majibu kwa Mheshimiwa Masilingi. (*Makofi*)

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu katika swali langu la msingi, Wizara ya Katiba na Sheria iko tayari kwa kushirikiana na Halmashauri kujenga hizo mahakama kwa mpango maalum, maelekezo ya jumla kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge itakuwa siyo rahisi kwa sababu kila Halmashauri nafikiri ina matatizo tofauti na Halmashauri ya Muleba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la pili, pale ninapokaa kuna kiti cha wanaozungumza na Waziri Mkuu lakini pia wanaozungumza na mimi, unakaribishwa. (*Makofi/Kicheko*)

**MHE. DR. WILLIBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza, lakini pamoja na swali hilo nimpongeze sana pia Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa uteuzi na kwa jinsi anavyoifanya kazi yake vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la msingi lilihusu Mahakama ya Wilaya ya Muleba ambayo hali yake ilisemekana inasikitisha sana, mazingira ya Muleba na mazingira ya Karatu yanafanana kabisa na kuwa ya Karatu siyo tu yanasikitisha ni kwamba mahakama hiyo haipo kabisa na wananchi wa Karatu wanateseka sana kwenda mahakama ya Monduli ambayo kidogo ipo nje ya barabara na matatizo haya nimeshayeleeza kwa Wizara, bahati mbaya anajibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali na siyo Waziri lakini kwa kuwa nimekwishaiandikia Wizara, je, kwa kuwa Serikali imekwishakujenga mahakama nzuri sana pale Karatu ambayo nayo imechangiwa na wananchi wa Karatu kupitia mradi wa *quick win*, Serikali sasa iko tayari wakati inaandaa utaratibu mwingine kuifanya mahakama hiyo iliyojengwa kuwa Mahakama ya Wilaya ya Karatu ili kuondoa adha ya watu wa Karatu kukaa *lockup* bila msaada wowote wa dhamana, wala huduma yoyote kwa sababu mahakama iliyopo iko mbali na eneo lao na hakuna mtu anayewafahamu, na taratibu hizi Wizara inafahamu kwamba ni ngumu sana, Mwanasheria Mkuu anatoa kauli gani kwa niaba ya Serikali?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la wananchi kufikia haki ni suala la Katiba, lakini pia ni suala la *dimension* ya *distance* kwa maana ya umbali kutoka kwa mwananchi mpaka kwenye mahakama, suala la fedha, suala la utamaduni na kwa hiyo, katika kujenga mahakama hizi Serikali inazingatia yote hayo. Lakini mfahamu pia kwamba uwezo wa Serikali katika kufanya kazi hizi ni mdogo lakini wazo lako nitalichukua na nitakupatia jibu ambalo ni sahihi zaidi kuliko la fikra, ahsante. (*Makofi*)

## **Zoezi la Kupiga Kura kubaini wauaji wa Albino Nchini**

**MHE. ANIA S. CHAUREMBO** aliuliza:-

Kwa kuwa hivi karibuni Serikali ilisimamia zoezi la kupiga kura za maoni kuhusu matatizo yaliyojitokeza na kero kubwa kwa wananchi kuhusu mauaji ya watu wenye ulemavu wa ngozi (*albino*), kukithiri kwa dawa za kulevya na ujambazi nchini.

Je, Serikali inasemaje kuhusu matokeo ya upigaji kura hizo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyoeleza Mheshimiwa Mbunge, Serikali iliendesha zoezi ambapo wananchi walipiga kura ili kubaini wahalifu wanaojihusisha na mauaji ya watu wenye ulemavu wa ngozi, biashara ya dawa za kulevya, ujambazi wa kutumia silaha na makosa mengine ya jinai. Lengo la kuendesha zoezi hilo ni kuweza kupata taarifa ambazo zitaviwezesha vyombo vya dola vinavyoshughulika na uchunguzi na upelelezi wa makosa ya jinai na ukamataji wa wahalifu, kutabiri mwelekeo wa uhalifu walizonazo ili kuweza kutambua mabadiliko ya uhalifu, maeneo korofi kwa uhalifu, wahalifu wanaohusika na mahali walipo ili kupanga mikakati ya namna ya kukabili uhalifu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ania Said Chaurembo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya upigaji kura uliosimamiwa na Serikali umesaidia sana Serikali kwa taarifa na kutoa mwanga katika kutuonyesha njia za kuwafikia wahalifu wanaojihusisha na mauaji ya watu wenye ulemavu wa ngozi, biashara ya dawa za kulevya, ujambazi wa kutumia silaha na makosa mengine ya jinai.

**MHE. ANIA S. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa Serikali imeshapata taarifa za kutosha kuhusu mauaji ya watu wenye ulemavu wa ngozi (*albino*), na kwa kuwa mauaji hayo bado yanaendelea, Serikali ina mikakati gani endelevu ya kuinusuru jamii hii ili iishi bila hofu.

(b) Kwa kuwa orodha ya watu ambao wanajishughulisha na dawa za kulevya ilipelekwa Ikulu kwa Rais, ningependa kujua kwamba matokeo yake ni nini, kuna baadhi yao tayari wamechukuliwa hatua yoyote?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli taarifa tunaipata lakini siwezi nikasema kwamba taarifa zinatosh

kwa sababu haya mauaji tunakiri kwamba yapo lakini kama nilivyosema hapa jana wakati najibu swali kuhusu mauaji ya ndugu zetu walemavu wa ngozi ni kwamba wimbi la mauaji sivyo kama nilivyokuwa na hii inatudhihirishia sisi kwamba jitihada zinafanyika za kuweza kukabiliana na tatizo hili.

Tunaposema Serikali inafanya nini naomba nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali si chombo ambacho kinaishi chenyewe, Serikali inahusisha na watu pia na tumekuwa tunasema kuwa kweli Serikali itafanya kazi yake lakini kwa kushirikiana na wananchi kwa kushirikiana na watu ambao wanaishi na jamii za hawa watu ambao ni walemavu wa ngozi kwa sababu ni huko ambako matatizo haya yanatokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna masuala ya ushirikina, Serikali itafanya nini kuhusu masuala haya, tumesema Serikali ihamasishe vyombo vya dini, taasisi mbalimbali waweze kutoa elimu kuweza kuwafundisha watu waondokane na hizi imani potofu za ushirikiana. Kuna matatizo ya waganga ambao ni waganga wa jadi na kadhalika, na jana nimejibu swali hilo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inafanya jitihada lakini pia tunataka ushirikiano mkubwa sana wa wananchi katika kukabiliana na suala hili na jitihada zimekuwepo na ushirikiano umekuwepo na ninaweza kusema kwamba jitihada zinariidhisha katika shughuli hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni kuhusu suala la dawa za kulevya, hili ni suala ambalo lilijibiwa na bado tunalijibu kwa kweli linafanyiwa kazi, hiyo orodha unayoisema kweli watu wamekuwa wanaisema. Hii ni nchi ambayo tunakubaliana kwamba tunakwenda kwa utawala wa sheria, hii si nchi ya kidikteta kwamba tukishapata orodha basi tunakwenda moja kwa moja tunawakamata watu, tunafuata utaratibu. Kama tukienda moja kwa moja mnasema kwamba tumekwenda kinyume na utaratibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka nikuambie kwamba jitihada zinafanyika na kwa kweli ni tatizo lakini sidhani kama ni tatizo kubwa sana kama nchi zingine za jirani ambavyo tunazona. Kwa hiyo, naomba katika yote haya mawili ushirikiano na raia ni muhimu sana ili kuweza kupata ufumbuzi wa masuala haya. *(Makofi)*

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniona, pia namshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake aliyotoa, pamoja na hilo nina swali dogo la kumwuuliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni nimeona kwenye televisheni baada ya kadhia ya mauaji ya kijana mmoja ambaye ni *albino* nikapata tafsiri ya kuwa Serikali katika jambo hili ni mdau mkubwa kama itakusudia kusaidia, kwa sababu inaonekana waganga wa jadi wanapata ruhusa kutoka kwa maafisa utamaduni wa ngazi mbalimbali katika Wilaya na Halmashauri, huoni kuwa sasa umefika wakati wa kufanya tathmini katika nchi nzima kwa hawa waganga wa jadi kwa sababu inaonekana wengine wapo kwa ajili ya kusababisha balaa na si kwa ajili ya kusaidia, sasa ikiwa hatuwezi kuwazuia

kabisa kwa nini basi hatufanyi utaratibu wa kuwajua wale ambao wanafanya kazi ya kweli na wale wababaishaji ili kupunguza hizi balaa za ushirikina ili ndugu zetu wakawa salama? (Makofi)

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la waganga wa jadi, Waziri Mkuu wa nchi yetu Mheshimiwa Mizengo Pinda alitoa tamko rasmi kuhusu tatizo la waganga wa jadi na kusema kwamba leseni ambazo zimekuwa zinatolewa zisimamishwe, na kusema kwamba hii shughuli ya waganga wa jadi pia isimamishwe kutokana na athari hizo ambazo Mheshimiwa Mbunge amezitaja, nikiri kwamba jitihada za utekelezaji wa agizo la Waziri Mkuu kweli umekuwapo lakini niseme kwa ukweli kabisa kwamba bado katika utekelezaji huo tumekuwa tunakwenda isivyo, na nafikiri tamko la Waziri Mkuu lilikuwa bayana kabisa na maelekezo yalikuwa bayana kabisa nafikiri, tatizo lipo katika utekelezaji na kwa kuwa Mheshimiwa Mbunge umetukumbusha nafikiri tutajitahidi kuona kwamba hilo agizo la Waziri Mkuu linatekelezwa. (Makofi)

Na. 74

### **Kuboresha vituo vya Kijeshi vya Kasanga na Kirando**

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ilifanya uamuzi wa busara wa kuanzisha vituo vya kijeshi katika vijiji vya Kasanga na Kirando hivyo kusaidia sana kuleta amani na utulivu katika Ziwa Tanganyika lililovamiwa na maharamia toka nchi jirani ya Kongo:-

(a) Je, ni kwa nini Serikali haitoi fedha za kutosha ili vituo hivi sasa vipate majengo ya kudumu na yenye hadhi kwa askari na maafisa?

(b) Je, Serikali itatoa lini boti ziendazo kasi ili kusaidia ulinzi katika ziwa Tanganyika?

(c) Kwa kuwa *detach* iliyopo Kasanga bado ipo katika Ngome Kongwe ya Bismark hivyo kuzuia utalii wa mambo ya kale na wala si heshima wao kuendelea kuwa pale, je, Serikali itawaondoa lini wanajeshi hao katika Ngome Kongwe?

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, Mbunge wa Kalambo, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haijatoa fedha za kujenga majengo ya kudumu kwa maafisa na askari katika vijiji vya Kasanga na Kirando kwa kuwa viteule vya kijeshi ni mpango wa muda mfupi unaotokana na matukio yanayohatarisha ulinzi



katika eneo. Itakapoonekana kuna haja ya kuwa na vikosi katika maeneo hayo Serikali itatenga fedha kwa ajili ya majengo ya kudumu.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia matukio ya ujambazi yanayojitokeza mara kwa mara katika Ziwa Tanganyika Serikali imenunua boti mbili ziendazo kasi kutoka Jamhuri ya watu wa China. Boti hizo zilizonunuliwa zipo Ziwa Tanganyika eneo la Kigoma. Jukumu la boti ni kufanya doria katika maeneo ya Ziwa Tanganyika ili kuzuia ujambazi na ujangili unaofanywa na maharamia kutoka nchi jirani. Boti hizo zina uwezo wa kutekeleza jukumu hilo kwa ufanisi katika pembe zote za Ziwa Tanganyika.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuwa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania linacho kiteule (*detach*) kilichopo Kasanga, kuwepo kwa kituo hicho kunatokana na umuhimu wa eneo hilo kiulinzi. Kasanga ni eneo la utalii wa mambo ya Kale na ni eneo maarufu linalotumiwa na wafanyabiashara. Ngome ya Bismark ni kituo cha muda na jeshi halikusudii kukifanya kituo hiki kuwa eneo la kudumu. Pindi hali ya kiusalama itakapoimarika wanajeshi walioko katika kituo hicho wataondolewa. (*Makofi*)

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

(i) Je, Wizara inachukua hatua gani kuzuia migongano inayotokea kati ya hao wanajeshi walioko katika kiteule hiki na wananchi katika kijiji cha Kasanga, migongano inayotokea mara kwa mara kutokana na kukaa katika mazingira ambayo wananchi wanaishi?

(ii) Ziwa Tanganyika lina urefu wa kilomita zaidi ya mia tano kutoka mpaka wa Kaskazini kwenda mpaka wa Kusini, boti ziendazo kasi zimewekwa Kigoma, je, Mheshimiwa Waziri, haoni ni busara kwa boti hizi moja ikawekwa Kigoma na nyingine ikawa Kasanga ili iwe rahisi kufanya *patrol* (doria) katika Ziwa, kuliko boti zote kuwekwa katika Mji wa Kigoma pekee?

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, habari ya kwamba, kuna migongano kati ya raia na wanajeshi katika eneo hilo la Kisanga kutokana na mazingira wanayoishi, tumeipokea kama taarifa muhimu, mimi binafsi nitafanya ziara katika eneo hili nikiambatana na Mheshimiwa Mbunge ili tujue tatizo ni nini, tuweze kujua hatua za kuchukua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili la nyongeza kuhusu urefu wa Ziwa na hoja ya kuona uwezekano wa boti moja kuwa Kigoma, tumelichukua pendekezo hilo kwa uzito unaostahili na tutalifanyia kazi. (*Makofi*)

Na 75

**Uchache wa Mahakama za Kazi**

**MHE. JUMA SAIDI OMARI** aliuliza:-

Kwa kuwa migogoro na migongano mahali pa kazi inatokea katika maeneo mbalimbali ya kazi hapa nchini; na kwa kuwa kuna Mahakama za Kazi chache sana hapa nchini:-

Je, Serikali inasema nini kuhusu uchache huo wa Mahakama za Kazi na migogoro inayotokea makazini?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruhusa yako kabla sijajibu swali hili naomba kwa ufupi sana, nitoe pongezi zifuatazo:-

Kwanza nimpongeze sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Jaji Frederick Werema kwa uteuzi wake. Pili, niwapongeze wana CCM na wananchi wa Wilaya yangu ya Ilala, kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kukipatia Chama cha Mapinduzi, ushindi wa karibu asilimia 93 katika uchaguzi uliopita. Niwapongeze hasa wananchi na wana CCM wa Kata ya Vingunguti ambao mitaa yao yote minne iliyokuwa imechukuliwa na *CUF*, tumeirudisha yote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na tatu kwa niaba ya Waziri wangu Profesa Juma Kapuya, napenda niipongeze sana klabu ya Simba kwa kipigo kile cha Jumamosi. (*Makofi/Kicheko*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo naomba kujibu swali la Mheshimiwa Juma Saidi Omari, Mbunge wa Mtambwe, kwa niaba ya Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuwa kuna kesi nyingi zimejaa katika Mahakama za Kazi hapa nchini. Serikali imechukua hatua zifuatazo ili kukabiliana na tatizo hilo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imefanya marekebisho ya sheria mpya za kazi ambazo ni:-

(i) Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Na. 6 ya mwaka 2004; na

(ii) Sheria ya Taasisi za Kazi Na. 7 ya mwaka 2004 na Kanuni za Utendaji Bora za mwaka 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchakato wa utatuzi wa migogoro ya kikazi umeanishwa katika Sheria ya Taasisi za Kazi Na. 7 ya mwaka 2004 ambayo imeanzisha taasisi mbalimbali za kushughulikia migogoro ya kazi hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchakato wa utatuzi wa migogoro ya kikazi huanzia kwenye Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA) ambayo ipo kila Mkoa Tanzania Bara. Tume hii hushughulikia migogoro kwa njia ya usuluhishi (*Mediation*) na uamuzi (*Arbitration*) na pale hatua hizi zinapokuwa zimeshindikana migogoro hii hupelekwa Mahakama ya Kazi, Divisheni ya Mahakama Kuu ya Tanzania ambayo ipo katika Mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Mbeya, Arusha na Mtwara. Hadi sasa Tume hii imeshapokea migogoro 19,000 na migogoro 16,587 imesuluhishwa ambayo ni sawa na 87.3% na 25% kwa njia ya uamuzi hadi Juni, 2009. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pande ambazo hazikuridhika zipeleke migogoro ya Mahakama ya Kazi, Kitengo cha Mahakama Kuu ya Tanzania kwa ajili ya mapito na marejeo au kukaza tuzo, zilizotolewa na waamuzi. Juhudi ambazo Serikali imefanya ni kutoa elimu kwa waajiri, wafanyakazi na vyama vyao ili wajue wajibu na haki zao kwa mujibu wa sheria na miongozo inayohusu ajira Tanzania Bara.

Aidha Serikali imeanzisha vyombo mbalimbali vya kuwashirikisha wafanyakazi katika maamuzi ya uendeshaji wa Taasisi zao, vyombo hivi ni mabaraza ya wafanyakazi, kamati za utendaji na uwakilishi wa wafanyakazi katika bodi za wakurugenzi pale sheria zinaporuhusu. Juhudi zote hizi zinalenga kuzuia na kupunguza uwezekano wa kutokea migogoro isiyokuwa ya lazima sehemu za kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Wizara ya Katiba na Sheria inakusudia kuajiri watumishi wa kutosha ili kuboresha utendaji wa kazi na kuongeza miundombinu ili kukabiliana na tatizo hilo. Hivyo tutakapoleta maombi yetu ya kuongezewa Bajeti kwa ajili ya maboresho hayo ni mtumaini yangu kuwa Bunge lako Tukufu litaidhinisha maombi hayo kwa ajili matumizi hayo.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sauti hizo tuangalie, tupunguze sauti Waheshimiwa! Haya swali la nyongeza Mheshimiwa Juma Said Omari.

**MHE. JUMA SAID OMARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

(a) Swali la kwanza, ni mikoa ipi hapa nchini ambayo inaongeza kwa migogoro na migongano mahali pa kazi?

(b) Ni nini kiini cha tatizo hili na nini ufumbuzi wake? Ahsante!

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali ya Mheshimiwa Juma Said Omar kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkoa unaongoza kwa migogoro na kutokana tu kuwa na viwanda na waajiri wengi na waajiriwa wengi ni Mkoa wa Dar es Salaam. Kwa kweli kiini kuna mambo mengi sana yanayoleta migogoro kwanza ni hali ya kikazi, masuala ya

maslahi, lakini vile vile kutojua tu taratibu na sheria ambazo kila mmoja kwa maana ya mwajiri na mwajiriwa kuzifuata. Tumekuwa tukisisitiza kila wakati kwamba kama kila mtu atazingatia hizi sheria ambazo tumezisema migogoro itapungua sana.

Na. 76

### **Mfuko wa Kusaidia Wananchi Majimboni**

**MHE. PARMUKH SINGH HOOGAN** aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi wengi ni maskini sana n hivyo imesababisha Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutenga mfuko ambao ungeweza kusaidia sana wananchi wengi majimboni:-

Je, ni lini mfuko huo utafika kwenye Jimbo la Kikwajuni?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, Mbunge wa Kikwajuni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, kwa kuunga mkono juhudi za Rais Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kutenga fedha za kuwasadia wananchi kwa kuwapatia mikopo yenye masharti nafuu. (*Makofi*)

Katika kutekeleza mpango huu Rais Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete alitoa shilingi milioni 600 kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Mheshimiwa Amani Abeid Karume, Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar alitoa kiasi kama hicho cha shilingi milioni 600 na kuwa na jumla ya shilingi 1,200,000,000/= kwa ajili ya wananchi wa Unguja na Pemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ilianza kutoa mikopo kwa wananchi wake mwezi Machi, 2009. Hadi kufikia Septemba, 2009 jumla ya shilingi milioni 861.97 zimekwishatolewa kwa wajasiriamali 414. Kati ya fedha hizo kiasi cha shilingi 646,070,000 zimetolewa kwa wajasiriamali wapatao 335 katika mikoa mitatu ya Unguja yenye Wilaya sita na kiasi cha shilingi 215,900,000/= zimetolewa kwa wajasiriamali 79 katika mikoa miwili ya Pemba yenye Wilaya nne. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Mjini, iliyoko Mkoa wa Mjini Magharibi na yenye majimbo 12 likiwemo jimbo la Kikwajuni, ilipata shilingi 121,400,000/= iliyowafaidisha wajasiriamali 91. (*Makofi*)

Kwa kuwa utaratibu wa utoaji wa mikopo umeandaliwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kuzingatia mgao wa Kiwilaya, napenda kumshauri Mheshimiwa Parmukh

Singh Hoogan, kuwasiliana na uongozi wa Wilaya yake ya Mjini, ili kujua wananchi waliofaidika na mikopo hiyo katika Jimbo lake Kikwajuni. (*Makofi*)

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mfuko huu mwanzo ulikuwa na utata sana kutoa mikopo hiyo. Je, tathmini imefanywa kuona mafanikio yake? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa tunaendelea na tathmini ya kuona ni namna gani mfuko huu umefaidisha wananchi. Lakini tathmini ya awali inaonesha kabisa kwamba wapo wananchi wengi sana waliofaidika na makundi mengi ya wajasiriamali wamefaidika ingawa ni kweli kwamba wajanja wachache vile vile walifaidika na hawa wanazidi kutambuliwa na kuchukuliwa hatua. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia matokeo ya tathmini ya awali vile vile imetuwezesha kuongeza taasisi ambazo zinahudumia badala ya benki peke yake kama ilivyo benki ya *CRDB* na *NMB* tumeongeza sasa vile vile taasisi zingine za kifedha ambazo si benki ili kuweza kuwafikia wananchi wengi zaidi. (*Makofi*)

Na. 77

### **Wanafunzi wa Kujitegemea wa Kidato cha Nne**

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA** aliuliza:-

Kwa kuwa wanafunzi watahiniwa wa kujitegemea wa Kidato cha Nne (*Private Candidates IV*) hujaza fomu za kuonesha mitihani ya kuainisha masomo aliyofaulu:-

(a) Je, iko sababu gani ya kutaka kuelewa matokeo yake ya mitihani ya nyuma kwenye fomu hizo?

(b) Je, uko uzito gani wa upungufu wa kutoainisha masomo yake aliyofaulu kwenye fomu hiyo?

(c) Je, kasoro gani zinazojitokeza kwenye mitihani kwa kutoambatanisha matokeo ya wanafunzi?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, Mbunge wa Chwaka, lenye sehemu (a) (b) na (c) napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa taratibu za uendeshaji wa mitihani katika Baraza la Mitihani la Tanzania ili mwombaji aweze kusajiliwa kama mtahiniwa wa kujitegemea wa mtihani wa kidato cha nne anatakiwa kuwa na moja ya sifa zifuatazo kabla ya kuleta maombi yake ya kutaka kusajiliwa.

Kwanza, awe amefanya na kufaulu mtihani wa maarifa, pili, awe amefanya na kufaulu mtihani wa taifa wa kidato cha pili katika shule iliyosajiliwa kisheria na Wizara ya Elimu na mafunzo ya ufundi na tatu, awe amewahi kufanya mtihani wa kidato cha nne na sasa anataka kurudia tena kufanya mtihani huo ili kuboresha sifa zake. Baada ya maelezo hayo napenda kujibu swali lake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna siri katika usajiri wa watahiniwa wa kujitegemea wa mitihani ya Taifa ya kidato cha nne. Lengo la kutaka taarifa zinazohitajika kujazwa katika fomu ya usajiri ni kusaidia Baraza la Mitihani, kuhakiki na kulinganisha taarifa alizojaza mtahiniwa na zile zilizopo katika kumbukumbu ya Baraza la Mitihani ili kuepusha uwezekano wa udanganyifu katika hatua ya usajiri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtahiniwa anayepaswa kuambatanisha matokeo yake ni yule aliyefanya mitihani ambayo haiendeshwi na Baraza la Mitihani la Tanzania au aliyesomea nje ya nchi. Watahiniwa waliofanya mitihani ya Baraza la Mitihani Tanzania hawapaswi kuambatanisha matokeo ya mitihani yao ya awali. (*Makofi*)

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa sisi tunaouliza maswali humu tumefanya utafiti wa kutosha na sisi ndiyo wazee wa watoto; na kwa kuwa kwa Zanzibar watahiniwa ni kinyume na alivyoeleza watahiniwa wa *private*. Watahiniwa wa *private* wanajaza matokeo yao ndani ya fomu zao. Hayo naeleza kwa uhakika kabisa kwa sababu nimefuatilia.

(a) Kwa nini ikiwa kuna ubaguzi kama huu wakati mtihani ni wa aina moja au Zanzibar ni nje ya nchi kama ulivyoeleza?

(b) Iko dhana kwamba mitihani ni kitega uchumi na ndiyo sababu kwamba hawa wanajaza matokeo ili kuweza zaidi kuitafuta *credit* ya tatu. Je, utawaeleza nini watahiniwa ili waondokane na mawazo kama hayo? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ujazaji wa fomu za kuomba kufanya mtihani uwe wa maarifa, kidato cha nne au kidato cha sita maelezo yake yapo bayana nyuma ya ile fomu. Katika fomu ile agizo la kwanza soma kwa uangalifu maelezo yote kabla hujajaza. Agizo la pili, hakikisha maelezo yote unayoyatoa ni sahihi na ya ukweli. Agizo la tatu weka sahihi kuthibitisha taarifa ulizoiweka ni sahihi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kile ni kiapo kwa lugha ya kisheria. Inavyotakiwa kutokana na hali ya sasa ilivyo ya kidunia, udanganyifu ulio mwingi watu kutokuwa na maadili ni vyema kila mhusika akaweka bayana habari zake. Kuna kosa gani kama

alifanya mtihani wa kidato cha pili akaonyesha? Kuna tatizo gani kama alifanya mtihani wa maarifa akaeleza kama kweli mtihani ni wake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tufike mahali chombo hiki tukiachie kitimize wajibu wake kwa faida ya kizazi na maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Pili, chombo kile siyo cha kibiashara kinatoa huduma, tena huduma muhimu kweli. Kwa taarifa fedha wanayokusanya kamwe haitoshi na ndiyo maana katika Bajeti ambayo Waheshimiwa Wabunge mmeipitisha mwaka huu Baraza la Mitihani limeongezewa fedha. *(Makofi)*

Naomba sote kwa pamoja tushirikiane kutoa maelezo kwa watoto wetu kuwa makini. Mimi mwenyewe kwa niaba ya Waziri mwenye dhamana ya Elimu nimefanyia kazi kwa kina na kwa undani mwaka huu nimebaini watu wetu walio wengi hawako makini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

Na. 78

### **Uchimbaji wa Visima kwa Ufadhili wa Benki ya Dunia**

**MHE. PAUL P. KIMITI** aliuliza:-

Kwa kuwa uchimbaji wa visima kwa kila kijiji kwa ufadhili wa Benki ya Dunia unaweza kukwama kutokana na ukosefu wa zana za kuchimba visima hivyo kutokuwepo:-

(a) Je, Serikali imejiandaa vipi ili tatizo kama hilo lisijitokeze kwa mikoa ambayo ina vijiji vingi na mashine moja tu kama ilivyo Rukwa?

(b) Je, uamuzi wa kuanzia Wilaya fulani na kuacha Wilaya nyingine unatokana na vigezo vipi ili wananchi waelewe sababu ya maeneo yao kutopewa umuhimu wa kwanza?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Paul P. Kimiti, Mbunge wa Sumbawanga Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kutekeleza mradi wa maji wa vijiji 10 katika Halmashauri zote nchini ikiwa sehemu ya programu ya kuendeleza sekta ya maji. Katika maeneo ambayo maji yanapatikana chini ya ardhi, Serikali inatumia wakala wake wa kuchimba visima na ujenzi wa mabwawa (*DDCA*) na kampuni ya kuchimba visima ni makubwa kuliko uwezo uliopo. Kwa sababu hii katika mwaka wa 2008//2009 Wizara yangu iliendelea kuijengea uwezo wakala kwa kuboresha mitambo na

vifaa vya kuchimba visima. Katika mwaka 2009/2010 Serikali inaendelea na mchakato wa kununua mitambo minane ya kuchimba visima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuongeza kasi ya uchimbaji wa visima, Serikali inatumia pia sekta binafsi katika kutekeleza miradi mbalimbali kama ilivyoainishwa katika sera ya maji ya mwaka 2002. Hata hivyo uwezo wa sekta binafsi bado haujatoshwa kukidhi mahitaji yaliyopo. Wizara yangu imeorodhesha kampuni 77 za uchimbaji wa visima na orodha hiyo imetumwa kwa Halmashauri zote nchini ili ziweze kuzitambua kampuni zinazoruhusiwa kuchimba visima na inapobidi kuziajiri kwa kufuata taratibu na sheria za manunuzi. (*Makofi*)

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri zimekuwa kwenye mchakato wa kutafuta watalaam washauri ambao watafanyakazi ya usanifu na usimamizi wa ujenzi wa miradi ya maji katika vijiji 10 vilivyochaguliwa. Kigezo kinachotumika katika kuchagua Wilaya gani ianze utekelezaji wa programu ni kasi ya ukamilishaji wa tathmini ya mapendekezo ya watalaam washauri na kuziwasilisha Benki ya Dunia kwa ajili ya kupata ridhaa ya kuendelea na hatua inayofuata na hatimaye Halmashauri kusaini mkataba kati yake na mtalaam mshauri. Kwa mfano, Halmashauri ya Sumbawanga Mjini ni miongoni mwa Halmashauri 103 ambazo zilikwishapata ridhaa ya Benki ya Dunia ya kusaini mkataba na mtalaam mshauri na mkataba ulisainiwa tarehe 14.7.2009. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziko Halmashauri 16 ambazo tayari zimekwishapewa ridhaa ya kusaini mikataba lakini bado hazijafanya hivyo. Halmashauri hizo ni za Manispaa ya Iringa, Ludewa, Muleba, Bagamoyo, Tabora, Nzega, Tunduru, Manispaa ya Shinyanga, Kishapu, Kahama, Meatu, Kilindi, Handeni, Korogwe, Pangani na Mkinga. Nazishauri Halmashauri hizo kufanya haraka kusaini mikataba yao ili kuwezesha kazi ya usanifu kuanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Simanjiro ndiyo peke yake ambayo kwa bahati mbaya haikupata hata kampuni moja na kurudia kutangaza kazi. Kufuatia tatizo hilo Serikali imekubaliana na Benki ya Dunia kutumia utaratibu wa *shortlisting* kutoka katika orodha ya watalaam washauri waliokwishapewa kazi katika Halmashauri nyingine ili kusaidia Halmashauri hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2008/2009 Wizara yangu iliendelea na jitihada ya kukarabati miundombinu ya maji kwa utaratibu wa dharura katika miji ya Mtwara, Lindi, Sumbawanga na Babati. Kwa upande wa Mji wa Sumbawanga mtalaam mshauri, mkandarasi wa kupima na kuchimba visima na mkandarasi wa kukarabati miundombinu ya maji, wote wamekwishajiriwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa napenda kuipongeza mamlaka ya maji safi na majitaka ya Mji wa Sumbawanga (*SUWASA*) bodi ya *SUWASA* chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Paul Kimiti, kwa kazi nzuri ya ufuatiliaji na kusimamia maandalizi ya utekelezaji. Matokeo ya ufuatiliaji huo ni kwamba Wizara yangu tayari imetenga shilingi bilioni 5.79 kwa ajili ya mradi wa maji Sumbawanga Mjini na tayari shilingi milioni 579 zimelipwa kwa makandarasi kama malipo ya awali ili waanze kazi. (*Makofi*)



**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri sana kuhusiana na suala hili, maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa kuna watu ambao wana macho lakini hawaoni, wana masikio hawasikii na katika suala zima wanasema Kimiti hajafanya lolote katika Mji wa Sumbawanga kuhusiana na maji, je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana na mimi ya kwamba arudie kidogo Serikali ya Chama cha Mapinduzi imesaidia nini katika mji wa Sumbawanga, chini ya Mbunge wake Paul Kimiti kuhusiana na maji?(*Makofi*)

Kwa kuwa Serikali ya Norway chini ya mradi wa umwagiliaji katika Manispaa ya Sumbawanga na mkoa wote wa Rukwa walifanya utafiti katika vijiji 334 na kugundua maeneo ambayo yanafaa kwa kuchimba kisima, Mheshimiwa Waziri atakubaliana na mimi ya kwamba washirikiane na Mheshimiwa Balozi wa Norway kuona uwezekano wa kutoa ile taarifa waliyokuwa nayo ili badala ya kusumbuka ya kutafuta wataalam wengine taarifa hiyo itumike kwa ajili ya uchimbaji wa visima. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na naomba wale wenye masikio wasikie kama alivyosema. Ni kweli kabisa Serikali imeshatenga fedha hizi kufuatia kama nilivyosema maandalizi mazuri yaliyofanywa na *SUWASA* chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Paul Kimiti na tumeshatenga fedha hizo na kazi hivi sasa inaendelea kwa kasi nzuri katika mji wa Sumbawanga.

Kuhusu hili la pili nakubaliana na Mheshimiwa Paul Kimiti kwamba tutashirikiana na Balozi wa Norway na ningependa pia ushirikiano huo kama alivyoutoa kwenye mradi wa maji wa mji wa Sumbawanga tuendeleo hivyo hivyo na kwenye mradi huo wa umwagiliaji nami nitaoa ushirikiano mzuri mpaka tuweze kujua sasa ni hatua gani tufanye ili tuchelewe kazi hii kuanza madhari tayari kazi ya awali ilikwishafanywa. (*Makofi*)

Na. 79

### **Hitaji la Umeme wa Gridi Namtumbo**

**MHE. VITA R. KAWAWA** aliuliza:-

Kwa kuwa Wilaya ya Namtumbo haina umeme kabisa na Serikali imekuwa ikiahidi kupeleka umeme wa Gridi kutoka Makambako – Songea hadi Namtumbo na kwa kuwa wananchi wa Namtumbo na ofisi za kisasa zilizojengwa Namtumbo wameshajiandaa kwa umeme huo uliokuwa umeahidiwa na Serikali tangu mwaka 2006 Bungeni.

Je, mradi huo wa KV 132 umefikia wapi?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Vita Kawawa, Mbunge wa Namtumbo, napenda nitumie nafasi hii kuungana na wenzangu kumpongeza sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa uteuzi wake lakini pia niwapongeze sana wananchi wa jimbo la Sengerema na Wilaya ya Sengerema kwa kuwezesha kupatikana ushindi mkubwa wa kishindi kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa na vijiji uliokamilika hivi karibuni pamoja na vitongoji, ushindi amboa zaidi ya asilimia 98. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba sasa niendele kujibu swali kama ifuatavyo maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa kupeleka umeme wa Gridi Songea kutokea Makambako unahusisha ujenzi wa njia ya umeme wa KV 132 yenye urefu wa kilomita 250, vituo vya kupoteza umeme vya KV 132/133 Madaba na Songea pamoja na kupanua na kusambaza umeme takribani kilomita 900 katika Miji/Wilaya za Songea, Namtumbo, Mbinga, Makambako, Njombe na Ludewa. Mradi huo utagharimu Dola za Marekani milioni 70.4 ambazo ni msaada (*grand*) kwa asilimia 80 na mkopo (*credit*) kwa asilimia 20 kutoka Serikali ya Sweden. Kama ilivyoenezwa hapa Bungeni mwezi Julai, 2009 wakati wa mawasiliano ya bajeti ya Wizara yetu, mkataba wa kupata fedha za msaada (*grand*) kati ya Serikali ya Uswidi na Serikali ya Tanzania ulisainiwa mwezi Disemba, 2008. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo ya utangulizi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua zilizofikiwa hadi sasa katika utekelezaji wa mradi wa Makambako – Songea ni kuanza kwa mchakato wa kumpata mshauri mwelekezi wa mradi. Tangazo la *expression of interest* kwa ajili ya kumpata mshauri mwelekezi wa mradi lilitolewa gazetini tarehe 28 Mei, 2009. Taarifa ya uchambuzi wa zabuni za kupata orodha ya washauri wenye nia ya kazi hiyo (*expression of interest*) pamoja na rasimu ya *request for proposal (RFP)* ziliwasilishwa kwa mfadhili (*SIDA*), mwezi Septemba, 2009 kwa mapitio na ridhaa.

Katikati ya mwezi Oktoba, 2009 *SIDA* wametoa maoni yao juu ya rasimu hiyo ya *RFP*. Maoni hayo yanafanyiwa kazi na *TANESCO* ili hatimaye yawasilishwe *SIDA* kwa hatua zaidi. Serikali iko kwenye majadiliano na Serikali ya Sweden kuhusu mkataba wa mkopo (*Credit Agreement*).

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii, pia nakupongeza kwa hatua nzuri iliyofikia Serikali lakini pia naomba kabla kwa ruhusa yako nami niwapongeze wananchi wa wilaya ya Namtumbo kwa ushindi mkubwa wa Serikali za Mitaa katika vijiji 440 tumeshinda vijiji 424 na vijiji vyote kasoro kimoja. (*Makofi*)

Kwa kuwa katika mradi tathmini ya awali ilifanywa kwa ajili ya matumizi ya umeme katika majumba na maofisi na baadhi ya viwanda vidogo, lakini kwa sasa hivi imeonesha kwamba kuna *potentiality* ya ongezeko la mahitaji makubwa ya umeme huu kwani kuna miradi mikubwa ya *uranium* ambayo tunategemea kutakuja kuwa na migodi na kwa kuwa wawekezaji wa madini ya *uranium* wameonyesha nia ya kushirikiana kusaidia kuweka *transmission line*, kutoka Songea itakayopita Namtumbo hadi kwenye *site* yao nawafikiria kuweka *generator* ya 20 Megawatt pale Songe na baadaye umeme wa gridi utakapouganishwa lije kuwa *backup power generator*. (Makofi)

(a) Je, Serikali mnashirikiana vipi na kampuni hiyo ya *MATRA Tanzania Limited* katika mawazo yao ya *project* hiyo?

(b) Kwa kuwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri wakati anamjibu Mbunge wa Nanyumbu tarehe 28 Oktoba, hapa Bungeni aligusia mradi unaweza kukamilika mwaka 2013 na alisema Wizara mnaendelea kufanya tathmini ya kushirikiana na *REA* ya kutupatia umeme wa *generator* angalau *megawatts* moja je, umefikia wapi na wakati wa mchakato huu unaendelea mnaweza kushirikiana na wataalam wa Wilaya ya Namtumbo ili kuona mahali itakapokaa hiyo *electric plug station* pia kutupa matumaini ya umeme huo kupatikana haraka?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kumpongeza sana Mheshimiwa Vita Kawawa, kwa jinsi ambavyo amekuwa akifuatilia kwa karibu sana upatikanaji wa umeme katika jimbo na Wilaya ya Namtumbo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba nijibu maswali yake mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Swali la kwanza kama ambavyo tumekuwa tukisema kwa kadri itakavyowezekana fursa zinazopatikana sera za nishati na Wizara kwa ujumla ikiwa ni pamoja na Serikali ni kuwashirikisha wawekezaji binafsi ili kurahisisha upatikana wa nishati hiyo katika nchi yetu. Kwa msingi huo basi tumekuwa tukiendelea vizuri na mazungumzo na kampuni ya *MATRA* ambayo inafanya utafiti wa *Uranium*, kimsingi imeshagundua na huo mpango wa wao kuweka pale mitambo yenye uwezo wa kuzalisha *megawatt 20* katika mji wa Songea ambazo baadaye zinaweza kusafirishwa mpaka Namtumbo, tunaendelea na mazungumzo na tunaendelea vizuri. (Makofi)

La pili kuhusu uwezekano wa kuwapatia umeme kwa kuanzia kwa sasa hivi wakati mpango mkubwa unaendelea ni kwamba *TANESCO* wameshakamilisha tathimini yao tunawashirikisha *REA* pia, sasa hivi ni kuhakikisha kwamba zoezi la kupata hiyo mashine au hiyo *generator* walau ikazalisha umeme wa kuanzia wakati ule mpango wa kushirikiana na *MATRA* unaendelea lakini pia wakati utekelezaji wa mradi mkubwa kutoka Makambako kuelekea Songea. Kwa hiyo, tunawapa matumaini wananchi kuwa mipango yote tunaifuatilia kwa karibu sana, ahsante. (Makofi)

## **Serikali Kujihusisha Katika Mradi wa Ujenzi wa Machinjio ya Kisasa Dar es Salaam**

**MHE. MGANA I. MSINDAI** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali haikutoa maelezo ya kutosha wakati wa kujibu swali namba 4497 la Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar na kwamba Kamati ya Bunge ya Kukagua Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) ndiyo ilikuwa inawakutanisha mwekezaji na Manispaa za Temeke, Kinondoni na Ilala na kuhakikisha kuwa watajwa hapo juu wanatoa michango:-

(a) Je, Serikali itakuwa tayari kukutana na Kamati hii ili ipate maelezo ya kina?

(b) Je, kwa kuwa mradi huu unayumba kutokana na wadau kutoridhia na kuchangia kwa sababu zisizojulikana, Serikali haioni kuwa umefikia wakati ijihusishe kikamilifu ili mradi huu uanze?

(c) Je, wakati mradi huu haujaanza Serikali inasemaje juu ya machinjio yasiyo na hadhi ya Mombasa - Ukonga na Vingunguti?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mgana Msindai, Mbunge wa Iramba Mashariki naomba kufanya marekebisho kuhusu namba ya swali alilorejea. Ni kwamba swali lililoulizwa na Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mbunge wa Viti Maalum lilikuwa ni swali namba 4338 na lilijibiwa kama swali namba 148 wakati wa Mkutano wa 14 tarehe 10 Februari, 2009. Aidha, swali namba 4497 analorejea Mheshimiwa Mgana Msindai, lilihusu ukarabati na uanzishwaji wa Chuo cha Ufundi cha Walemavu na liliulizwa na Mheshimiwa Mariam Kasembe Mbunge wa Viti Maalum. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya marekebisha haya naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Mgana Msindai, Mbunge wa Iramba Mashariki lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kwa ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku zote Serikali imekuwa ikipokea ushauri na maoni kutoka kwa Kamati mbalimbali za Bunge ikiwemo Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC). *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jiji la Dar es Salaam kupitia Halmashauri zake za Kinondoni, Ilala na Temeke waliamua kuchanga ili kujenga machinjio ya kisasa. Kwa taarifa tulizopata toka kwao walichanga *USD 2,005,083* wakati mahitaji halisi ni *USD 9,700,000*. Hivyo mradi huu umeshindikana. Aidha, si jukumu la Serikali kufanya biashara, hata hivyo Wizara yangu imewahamasisha wadau mbalimbali kupitia *TIC* kuwekeza katika miradi ya aina hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuboresha machinjio za Mombasa, Ukonga, Vingunguti na sehemu zingine hapa nchini Wizara yangu inaziagiza Manispaa, Majiji na Halmashauri zote nchini kutenga Bajeti ya kutosha ili kujenga machinjio ya kisasa yanayoendana na sheria ya nyama namba 10 ya mwaka 2006 pamoja na zingine za mifugo katika kulinda afya ya watumiaji nyama. *(Makofi)*

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu yasiyoridhisha ya Serikali naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa jiji la Dar es Salaam na Manispaa ya Ilala, Kinondoni na Temeke, zilikuwa zinashirikiana na mwekezaji kutoka nje na kwa kuwa hizi hela karibu shilingi bilioni mbili ni hela za walipa kodi wa nchi hii na hizi hela walikuwa wanapewa mwekezaji je, Serikali itarudishaje hizi hela kutoka wale wawekezaji wa nje? *(Makofi)*

Kwa kuwa machinjio ya Mombasa hayafai na Kamati yetu iliwahi kwenda ikakuta ng'ombe wanateremshwa kwa kusukumwa kutoka kwenye roli na wengine walikuwa wamekufa na tuna wasiwasi kwamba mara nyingine kama hawakuangalia unaweza kulishwa vibudu. Je, Serikali ilitumia njia gani kujenga machinjio ya kisasa ya Dodoma na kwa nini ishindwe kujenga machinjio ya kisasa kwa jiji letu kuu la Dar es Salaam? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza wabia waliokuwa katika mradi huu, ilikuwa ni Halmashauri ya Jiji ambayo ilichanga dola milioni moja lakini kama kiwanja, wengine ilikuwa Manispaa ya Ilala, wengine walikuwa Manispaa ya Temeke, Manispaa ya Kinondoni na wengine walikuwa ni kampuni ya *NICO* na mwingine alikuwa mwekezaji toka nje ambaye alikuwa anatoka Malaysia, ambaye alikuwa alete vifaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, habari tulizonazo ni kwamba tarehe 23 Julai, 2009, Naibu Katibu Mkuu wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa alikutana na wabia hawa *East African Meat Company* na katika kukutana nao, aliwaambia kwamba mradi huu umeshindikana na unatakiwa kufungwa na *East African Meat Company* wakakutana wote wale wabia kuamua kufunga bila mtu yeyote kumpeleka mwingine Mahakamani, kwa hiyo, naamini kwamba kama kulikuwa na pesa za mtu zimepotea za mbia, hapo kungejitokeza mashitaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama kuna ubadhilifu wowote umetokea hata kama hiyo kampuni imefungwa naamini Serikali italipeleleza hili jambo na kuchukua hatua zilizopo, lakini kwa sasa hivi wale wameamua kufunga bila mtu kumfikisha mwingine Mahakamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kwa nini mradi wa nyama Serikali imeshindwa kuanzisha mradi wa nyama bora jijini, nafurahi kwamba hilo tatizo Serikali imeling'amua na sasa kwa kupitia *National Lanching Company*, sasa hivi tuko katika harakati ya kujenga machinjio makubwa kuliko yote katika upande wa Afrika Mashariki na Kati,

machinjio hayo yameanza na tunatarajia ifikapo mwaka kesho mwishoni, machinjio hayo yatakuwa tayari na tutachinja ng'ombe 800 kwa siku ambao zitapelekwa katika jiji la Dar es Salaam na vile vile tutachinja mbuzi 400 kwa siku na hiyo yote ni kukidhi mahitaji ya nyama ya Dar es Salaam.

Lakini hata hivyo ninavyoongea kwa sasa hivi ukitaka nyama bora, ukienda pale Nkurumah utapata Kongwa, Ruvu, ukija hapa karibu na Mwalimu Nyerere wamefungua *butcher* nzuri pale, Mheshimiwa Mzee Mzindakaya amefungua pale Namanga. Kwa hiyo, tunajitahidi kuhakikisha kwamba nyama bora inapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile machinjio ya Vingunguti pia imefanyiwa ukarabati ni nia ya kuhakikisha kwamba nyama bora inapatikana Dar es Salaam. Lakini kwa kuongeza zaidi, Mheshimiwa Waziri Mkuu ametoa waraka kuagiza Mikoa ihakikishe kwamba *butcher* zote zinakuwa na mashine ya kukatia nyama na zinatoa nyama ambayo ni safi na bora. (*Makofi*)

Sasa hivi Mikoa yote na Halmashauri na Miji yote inafanyiwa kazi ifikapo tarehe 30 Januari, 2010 itakuwa kwamba ili kupata leseni lazima *butcher* hiyo iwe na mashine ya kukatia nyama na nyama itoke katika machinjio mazuri, kwa hiyo, Serikali inashughulikia jambo hili kwa Tanzania nzima na sio tu Dar es Salaam. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge mkiangalia saa yetu, muda wa maswali umekwisha kutokana na uendeshaji wa sayansi na teknolojia tumefikia pale pale bila kuongeza muda. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tutakapoanza uchangiaji baadae kidogo wa Sheria yetu ya Mtoto, wachangiaji watakuoanza wawili niwataje ili waweze kujianda ni Mheshimiwa Anne Kilango Malecela na Mheshimiwa Bujiku Sakila ili waanze kujiandaa. Tutakuwa na wachangiaji kama wanne hivi. (*Makofi*)

Naomaba nitangaze kikao cha Kamati ya Uongozi saa saba mchana kwa ajili ya kuzingatia masuala ya ratiba yetu Ukumbi wa Spika kama kawaida. (*Makofi*)

Pia Mwenyekiti wa Kamati ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Abdisalaam Issa Khatib anawaomba Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Viwanda na Biashara, kwamba leo tarehe 4 Novemba, saa 7.00 mchana kutakuwa na kikao katika ukumbi namba 133, ghorofa la kwanza, jengo la Utawala. (*Makofi*)

Mheshimiwa Alhaji Mohamed Missanga, Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu anaomba Wajumbe wa Kamati hiyo wamepata rufusa kutoka kwa Mheshimiwa Spika kwamba kikao chao kianze saa tano asubuhi hii, ukumbi 231, ghorofa la pili jengo la Utawala. (*Makofi*)

Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii anaomba Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Huduma za Jamii kwamba leo saa 7.00 mchana kutakuwa na kikao katika chumba namba 227 jengo la Utawala. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti Kamati ya Kudumu ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Wilson Masilingi, anawaomba Wajumbe wa Kamati yake katika kikao kitakachofanyika leo saa 7.00 mchana katika Ukumbi wa Pius Msekwa, na nakumbushwa hapa kuwa kwa ruhusa ya Mheshimiwa Spika, Kamati hii mkae saa 5.00 asubuhi pia.

Tangazo kwa Wabunge wote, naomba hili nilisome lilivyo linatoka kwa Mama Flora Masaga, Mkurugenzi Msaidizi Shughuli za Bunge kwamba fomu za tamko la rasilimali na madeni zinapatikana kwenye Ofisi ya Katibu wa Bunge, hivyo Wabunge wote mnaombwa kuchukua fomu hizo na kuzijaza kikamilifu ili ziweze kuwasilishwa kwa Kamishena wa Maadili kabla ya tarehe 3 Desemba 2009, tafadhali mnaombwa kuzingatia tangazo hili. Mbona wengine wananung'unika? (*Makofi/Kicheko*)

Tunaendelea na matangazo, wageni walioko Bungeni ni pamoja na wageni wa Naibu Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, Mheshimiwa Dr. Cyril Chami ambao ni pamoja na Mzee Augusti Chami, baba yake mzazi, yule pale karibu sana baba yetu, yuko Meinred Swai, Mwenyekiti wa Chama cha Wakulima wa Kahawa cha KCU karibu sana, yupo Martin Malya, Katibu wa Mbunge, hongera kwa kazi, pia ndugu Alfajiri Mshele, Msaidizi wa Mbunge, karibu Dodoma. (*Makofi*)

Wageni 13 wa Mheshimiwa Dunstan Mkapa, Mbunge ambao ni Wenyeviti wa CCM wa Kata wakiongozwa na Chibwana Mtimbe Geuza, Mwenyekiti wa CCM. Hao ni Wenyeviti wa CCM wa Kata kutoka katika Jimbo la Mheshimiwa Mkapa. Hongereni sana na karibuni sana Bungeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Castor Ligalama ana wageni ambao ni Madiwani 14 wakiongozwa na Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero, ndugu Mkopachuma Magwaja, karibuni sana Waheshimiwa Madiwani hapa Bungeni. (*Makofi*)

Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Savelina Mwijage wakiongozwa na Mheshimiwa Gervazi Silvanus mtoto wake, ahsante sana. Mtoto wa Mheshimiwa asimame tumuone, ooh, karibu sana.

Wageni wa Mheshimiwa Profesa Raphel Mwalyosi ni pamoja na Ndugu Selina Haule, Diwani Viti Maalum Tarafa ya Liganga, ahsante sana, Ndugu Consolata Mgogo, Diwani Viti Maalum Tarafa ya Mlangali, karibuni sana Dodoma. (*Makofi*)

Pia ninao wageni wa Mheshimiwa Lucy Mayenga, Mbunge ambao ni wanafunzi 20 kutoka shule ya sekondari ya Jitegeme Dar es Salaam, hongereni sana kwa taarifa yenu Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Lucy Mayenga nae alisoma katika shule hiyo ya Jitegeme. Wanafunzi hawa wanaongozwa na mwalimu Karume Geoffrey, mwalimu karibu sana. Lakini pia tunao wanafunzi 50 kutoka katika shule ya msingi Chalula hapa Dodoma, watakuwa mahali fulani *basement* huko.

Ninalo tangazo la mkutano wa wadau wa zao la kahawa, tangazo hili linatolewa na Naibu Waziri Mheshimiwa Dr. Cyril Chami, Naibu Waziri Viwanda, Biashara na Masoko, anaomba Waheshimiwa Wabunge wote wanaotoka Mikoa inayolima kahawa wahudhurie kikao leo saa 7.30 mchana katika ukumbi wa Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, watakutana na Mwenyekiti wa Chama cha Wakulima wa kahawa cha *KNCU*, Bwana Menired Swai. Naomba pia niwatambue Wenyeviti na Makatibu 12 wa CCM wa Kata kutoka eneo la Kibosho Moshi, wasimame pale walipo, karibuni sana hapa Bungeni niwahakikishie Mbunge wenu Dr. Cyril Chami, anafanya kazi nzuri sana, karibuni sana. Mgeni wa Mheshimiwa Hemed Mohamed Hemed ni Ndugu Masudi Muheluta ambaye anatoka Tabora Uyuwi, karibu sana. Huo ndio mwisho wa matangazo, Katibu. (*Makofi*)

## **MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

### **Muswada wa Sheria ya Mtoto wa Mwaka 2009**

*(The Law of the Child Bill, 2009)*

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nianze kwa kuwashukuru wananchi wangu wa Same Mashariki kwa kuhakikisha kwamba wanakipa heshima Chama cha Mapinduzi kwa kunyakuwa viti vyote vya vijiji kwamba viongozi na Wenyeviti wa vijiji kutokana na Chama cha Mapinduzi. Naomba niwashukuru sana wananchi wa Jimbo langu kwa kukipa heshima chama changu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri kwanza kwa kazi nzuri wanayoifanya ndani ya Wizara hii. Wizara hii ukiiangalia juu juu unaweza ukadhani ni Wizara rahisi sana, sivyo. Ni Wizara nzito, kwa sababu inahusu maisha ya mtoto na jinsia zote kwa ujumla lakini naomba Mama Margaret Sitta na ndugu yangu Naibu Waziri niwaambie Wizara hii imepata viongozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Serikali kwa dhati kabisa kwa kuleta Muswada huu, kabla sijaanza nikupongeze na wewe Mheshimiwa Mwenyekiti kwa kuendesha vikao vya Bunge kama Spika kabisa na kwa kweli wananchi wa Jimbo la Kongwa wamechagua lulu, sasa naomba nianze kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu Muswada ni Muswada muhimu sana kwa sababu, sasa mtoto anakuwa na sheria yake ambayo ipo mahali pamoja kuliko ambavyo tulivyokuwa tunaokoteza okoteza mara kwenye mirathi, mara kwenye sheria za ndoa sasa mtoto atakuwa anakuwa na mahali ambapo panaeleweka. Lakini mimi nitaongea kwa taratibu zangu nilizojipangia mwenyewe; kwa uelewa wangu mimi, mtoto ni mtoto wa Jamhuri, mtoto akishazaliwa anakuwa ni mtoto wa Jamhuri. Nilikuwa nimeuliza swali



Wizara ya Afya ambayo sasa nitalinzungumzia hapa kwa hiyo hata likija litakuwa hakuna umuhimu.

Kwa kuwa mimi ninavyoelewa kwamba mwanamke yeyote wa kawaida anaweza kwa mwaka kuzaa mtoto mmoja, naomba kidogo Bunge lingepunguza maongezi.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba sana toka asubuhi tunasisitiza habari ya kupunguza sauti naomba tuzingatie jambo hilo la Kikanuni.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi ninavyoelewa kwamba mwanamke yeyote ana uwezo wa kupata mtoto mmoja kwa mwaka, lakini mwanaume ana uwezo wa kutengeneza watoto katika siku 365 hata zaidi ya 100, mwanaume ana uwezo huo atakavyojipangia yeye mwenyewe na atakavyojichukulia nidhamu kiasi gani yeye mwenyewe. Tumekuwa na hili tatizo sana ndani ya nchi yetu kwamba wanaume, baadhi ya wananume wanakuwa na watoto wa nje ya ndoa, lakini baada ya kuwa na watoto hawa wa nje ya ndoa wanawatekeleza moja kwa moja na wanawakana watoto hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tukizungumza ukweli Mwenyezi Mungu tumshukuru kwamba mara kwa mara mtoto wa nje ya ndoa Mwenyezi Mungu anamuumba sana afanane na baba yake, utakuta kama sikio la baba liko hivi na lile la mtoto wa nje ya ndoa liko hivyo hivyo lakini bado akina baba wanawakana watoto na bado utaona akina baba wanadiriki kwenda kufanya *DNA* wanakataa na wakiambiwa hata wachangiwe wanakataa, sheria hii ningeomba imdhibiti mwanaume anayekataa kufanyiwa *DNA*, hii sheria naomba itusaidie hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hii ifikie mahali itusaidie kwamba baadhi ya akina baba wanaowatelekeza wale watoto wabanwe ili waweze kuchangia sawa sawa malezi ya watoto wale kuliko ambavyo sasa mwanamke wa Tanzania anaachiwa malezi ya watoto ambao amechangia na wenzie katika kumleta duniani. Hapo nilitaka nieleweke vizuri zaidi, naomba sheria imbane baba ambaye amezaa mtoto nje ya ndoa achange malezi ya mtoto yule. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna jambo linaloniudhi kama kuona watoto wanaoishi mitaani, wanaoishi katika mazingira magumu, watoto wale, wengi ni wale wanaotokana na kutelekezwa, mama anaachwa na yule mtoto, mama anakuwa hana uwezo basi mtoto anaingia barabarani, tunapoteza sana nguvu kazi ambayo sio lazima iwe hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwenye umri wa mtoto wa kike kuolewa, bado mimi ningeomba umri wa mtoto wa kike kuolewa uwe unaeleweka kabisa kunazia mika 18 na kuendelea kwa sababu tunaposema kwamba labda hivi labda hivi, tunampa nafasi mtoto wa kike kutokuwa na elimu ya kutosha tunavyosema vinginevyo, mtoto apewe nafasi ya kupata elimu ya kutosha kwa sababu mwanamke akielimika, tunakuwa tuna uhakika kwamba tumeelimisha jamii kubwa sana, akina mama wanasimamia sana shule upande wa watoto, mama kila jioni yeye ndiye anayeangalia mtoto amefanya kazi vizuri

shuleni, mtoto amefanya *assignment*, mtoto amejibu vipi maswali, sasa tunaposema mwanamke anaweza akaolewa kabla ya miaka 18 tunadhaliisha kabisa kwamba tuwe na akina mama ambao hawana elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ningeomba hili lisiwe na visababu vingine vidogo vidogo, ni sisi wenyewe tukatae kuwa tunaharibu jamii yetu, ni vyema tukasimama imara katika kuelimisha watoto wetu wa kike na kama tunataka wapate elimu, jamani wasiolewe mapema sana. Hii sheria naomba iwe *very specific*, kwamba mtoto aolewe lini isiweke vipengele ambavyo vitatoa mianya vya mtoto kuolewa miaka 13, 14 kwanza jamani hata kimaumbile anakuwa bado. Ni rahisi sana mtoto wa miaka 13 kuzaa mtoto ambao hakukamilika, naomba sana hili liangaliwe pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kina baba msije mkanielewa vibaya lakini kidogo leo naomba nizungumzie haswa hili jambo la malezi. Malezi ya watoto yameachwa mno upande wa mama, akina mama wa Tanzania wanalea watoto wenyewe, wanawake wanaotengana na waume zao wanaachiwa mzigo mkubwa wa kulea watoto. Wengi wao, hebu hii Sheria iwafanye baadhi ya wanaume wale ambao wanaona mama anaweza akalea watoto mwenyewe, waone kwamba ni muhimu sana nao ni wazazi sawa sawa na mama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo mifano mingi tena iko hai, akina mama wanalea watoto wenyewe. Baba labda anaoa mke wa pili wale watoto sita anamuachia mama, hii Sheria imkamate baba vizuri hapa. Kina baba msikasirike lakini, ni lazima nitetee akina mama wa Tanzania wengi wanahangaika sana na wengi wanajikuta wanakufa mapema kwa sababu ya mzigo mkubwa wa kulea watoto. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa leo naona imetosha naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi na mimi nichangie katika hoja hii. (*Makofi*)

Awali ya wote napenda niwashukuru wapiga kura wa Jimbo la Kwimba ambao walishiriki katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Jimbo la Kwimba na kukipatia ushindi Chama cha Mapinduzi kwa asilimia 95, labda nitumie nafasi hii kuwapa pole wananchi wa kijiji cha Kawekamo, Buyogo na Bugembe ambao kwa bahati mbaya sana walikosea, lakini naamini safari nyingine watajirekebisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea napenda kumpongeza Mheshimiwa Jaji Frederick Werema kwa kuteuliwa kuwa AG katika Bunge letu, nampongeza sana kwa niaba yangu mimi binafsi na kwa niaba ya wapiga kura ya Jimbo la Kwimba. (*Makofi*)

Naomba nitumie nafasi hii pia kumpongeza Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na timu yake kwa kuleta Muswada huu katika Bunge letu. Naipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu kwa kupitia Wizara hii kwa sababu ni Muswada muhimu sana, Muswada huu ni muhimu sana kwa sababu, kwanza kabisa Bunge linafanya huduma.

Tunaongelea juu ya kikundi cha watu ambao hawana sehemu maalum pa kujitetea, kwa hiyo tunatoa huduma kwa vijana hawa na kwa watoto wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila Bunge kujadili juu ya Muswada huu hawana mahali pengine pa kukimbilia, lakini vile vile Muswada huu ni muhimu sana kwa sababu tunatunga Sheria kwa ajili ya kulea Watanzania wa kesho, mimi naamini kama Sheria hii itakuwa nzuri tutakuwa na Taifa zuri sana, kama tutakuwa tumekosea katika kutunga Sheria hii tunaweza kuwa bomu baadae. Lakini naamini tumefanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, sehemu kubwa nimeshiriki katika kuandaa Muswada huu, tulikuwa na kazi kubwa sana. Unapoandaa Muswada ambao unatokana na mkataba wa Kimataifa, kuna mambo mengi sana ambayo unapaswa kuyaangalia. Kwanza kabisa katika kipindi hiki tunapita katika kipindi cha soko huria, unapoongelea juu ya soko huria kwa mkulima atafahamu ni soko huria kwa ajili ya mazao yake, lakini soko huria ninaloliongelea mimi hapa ni soko ambalo linahusiana na utamaduni vile vile, kila Taifa, kila nchi inajaribu kuuza utamaduni wake na njia mojawapo ni kupitisha utamaduni wake katika mikataba kama hii na ipo kanuni kwamba utamaduni ambao ni dhaifu au duni, mara nyingi huwa unamezwa na utamaduni ulioendelea. Lakini anaetambua kwamba utamaduni huu ni dhaifu, ni mwenye utamaduni, anaetambua kwamba huu utamaduni umeendelea ni mwenye utamaduni vile vile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inakuwa ni jukumu la kila mmoja kuamua aache utamaduni fulani aingie kwenye utamaduni mwingine na hapa ninayo mifano. Katika kabila la Wasukuma wana utamaduni wa kulima kwa kutumia ng'ombe, yapo makabila kama kabila la Wagogo hawakuwa na utamaduni huo lakini kwa sababu ya utamaduni wa kulima kwa kutumia ng'ombe umekuwa ni bora zaidi, tunashukuru kwamba hata Wagogo wa sasa wameanza kuiga utamaduni huo wa kutumia ng'ombe, ni jambo jema sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kama mambo haya yanaingia pole pole, unapopata msaada kama huu kazi mojawapo lazima uangalie ni kwa kiwango gani umebeba uchumi wa nchi yetu na ni kwa kiwango gani, mambo kutoka nje yameingia katikati ya Muswada huu, ni jukumu lako unaechambua kujua kwamba hapa naingiza utamaduni wa nje, hapa nalinda utamaduni wa nje na hapa nalinda utamaduni wa nchi yangu. Mimi napenda nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, amesikiliza wadau wengi sana, amepokea hoja nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile napenda niwapongeza wanasheria kutoka kwa CAG wamefanya kazi nzuri sana kutuongoza kwamba hapa tukienda mnakosea, hapa mkienda mnaenda vizuri na ndiyo maana mkiangalia hata lile Jedwali la Marekebisho ni kubwa sana. Limechukua muda wa siku nyingi sana. Labda nitumie nafasi hiyo kumtoa wasiwasi mama yangu aliyemaliza kuongea sasa hivi. Hata hivyo alikuwa anasema juu ya wanaume wanaokataa watoto, wanaokatakaa kwenda kupimwa hili tumeliona. Ninashukuru Mheshimiwa Waziri amelipokea na mimi nachukua sana wanaume wanaokataa na sasa hivi ni kwamba hilo wazo lichukuliwe na sasa hivi kama

ikitokea kwamba umekataa kwenda kupimwa unaweza kuchukuliwa hatua. Lakini katika Kamati yetu hatukuishia hapo, ni kwamba wapo akina mama ambao wanaiba watoto hospitalini, kwa hiyo *DNA* ishiishie kwa wanaume tu. Vile vile na akina mama washirikishwe katika kupimwa *DNA* kuhakikisha kwamba huyu mtoto ni wa Kwake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naongelea juu ya soko huria. Tumejaribu kuangalia ni kwa namna gani, utamaduni wetu unalindwa katika sheria hii na kwa kweli nadhani Sheria itakayotoka hapa itakuwa ni sheria inayolinda utamaduni kwa nchi yetu kwa kiwango cha juu sana. Inawezekana kabisa kuna maeneo ambayo hatukuweza kuyafikia, lakini mimi naamini kwamba Mheshimiwa Waziri tutakapofikia wakati wa kutunga Kanuni ataweza kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo mimi nilikuwa na maeneo mawili ambayo nilikuwa na wasiwasi nayo kidogo, pamoja na kwamba nilikuwapo kwenye Kamati hii, niliona kwamba yalizonisumbua niweze kusimama hapa kuomba kuongeza. (*Makofi*)

La kwanza, kuna maeneo ambayo yanasema mtoto anaweza kulelewa na wazazi wa kambo (*forced parents*). Ukiuangalia huu Muswada, zipo taratibu ambazo zinatakiwa kufuatwa ndiyo mtoto huyo anajulikana kwamba analelewa na wazazi wa kambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaweza kutokea kwamba mtoto mmoja ameamua kwenda kukaa kwenye familia fulani, anaweza kuwa na familia yao ya kwake au hana kabisa, anakwenda pale bila taratibu kufuatwa, nilikuwa najiuliza, huyu anayempokea huyo *voluntarily* kwa hiari yake, je, huyu mtoto atakaa kwa muda gani ili atambulike kama ni mtoto wa familia ile? Kwa sababu ukiangalia ile Sheria, inasema kwamba mtoto anapohama kutoka kwenye familia moja kwenda familia nyingine kwa taratibu ambazo zimewekwa na sheria hii anapoteza haki zake kutoka kwenye familia anakotoka kwa hiyo, anapata haki zake kwenye familia anakokwenda. Huyu sheria na taratibu hazikufuatwa, amekuja kwa hiari yake, akaamua kukaa pale, je, katika hali hiyo ambapo taratibu hazikufuatwa mtoto huyu je, atakuwa amepoteza zile haki zake kutoka kwenye familia alikotoka?

Je, anatakiwa kukakaa katika kipindi cha muda gani katika familia hii mpya ili ajulikane kwamba kweli ni mtoto wa pale, ili aweze kupata zile haki zake bila taratibu za kisheria kufuatwa? Hiki ndicho kitu ambacho nilikuwa na wasiwasi nacho, nilitaka kumuuliza Mheshimiwa Waziri ili ajaribu kusaidia kama kutakuwa na muda ambao atapamngiwa kwamba akikaa mahali fulani kwa muda fulani tayari atakuwa ameshajulikana kisheria kwamba huyu ni wa familia hiyo mpya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni nafasi ya jamii katika Sheria hii. Tunasema kwamba jukumu la kumlea mtoto ni jukumu la jamii. Lakini kwa mfano mtoto anafanya kosa fulani, mahali fulani, inatakiwa kufanya kitu gani, kwa sababu kwa miaka ya kule ya nyuma, unaweza kumuadhibu kidogo. Lakini sasa kwa sheria hii ile adhabu kuna sehemu ambayo inazuia *torturing*. Ni nani anayetambua hapa hii ni *torture*.

Kwa hiyo, ni kwamba yapo mambo mengine ambayo yanazidi kwa mfano mtoto amechomwa moto, amepigwa mpaka akavunjika mkono, hayo ni matendo ambayo yanaonekana, lakini kwa jamii mtu tu ambaye si mzazi wa mtoto anamkuta anafanya kosa anamkuta anafanya kosa, akimwadhibu mtoto bila kufikia hatua hiyo, je, Shberia inasemaje kwa mtu huyu ambaye ni sehemu ya jamii ambaye ana wajibu wa kurekebisha mtoto huyo. Nilipenda haya yajulikane kwa sababu itafika mahali jamii iogope kuwarudi watoto ambao wanakiuka taratibu za kijamii. Kwa sababu Sheria haikuwazi, inaweza kwamba mimi nafanya hivi kwa nia njema, lakini kumbe kisheria umeshavuka mipaka, kwa sababu haijawa wazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni kwamba tunatunga sheria ambayo kwa sasa hivi inatungwa na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto lakini utaona kwamba humu vile vile kuna Wizara ya Afya. Watu wengi wanapata wasiwasi, je, Sheria hii atakayeisimamia ni nani? Wengine wamefika kwenye wazo kwamba labda kuwe na Bodi ya kusimamia utekelezaji wa Sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa na wazo kwamba kama wazo la Bodi litakuwa ni gumu sana, mimi ombi langu kwa Serikali kwamba ni vema basi Maafisa Ustawi wa Jamii wasiishie Wilayani, waende zaidi karibu na watoto wa vijijini, angalau kila kijiji kipate Afisa Ustawi wa Jamii kwa sababu watoto ni wengi mno. Afisa Ustawi wa Jamii akifahamu kwamba kuna mahali fulani mtoto hatendewi vizuri ndiyo inaweza kuchukua muda mrefu sana. Kwa hiyo, nilikuwa nafikiri wangeenda mpaka kwenye ngazi ya Kijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema mimi kwamba nilikuwa kwenye Kamati hii, mchango wangu nilikuwa nimepeleka huko. Naunga mkono kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, nakushukuru Mheshimiwa Bujiku Sakila, kwa mchango wako. Kama nilivyosema Mheshimiwa Felister Bura, atafuatiwa na Mheshimiwa Dorah Mushi. Mheshimiwa Bura. (*Makofi*)

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia na mimi katika Muswada huu ambao uko mbele yetu. Lakini kabla sijaanza kuchangia, niwapongeze sana sana wananchi wangu wa Mkoa wa Dodoma kwa ushindi mkubwa tulioupata kwa uchaguzi wa viongozi wa Serikali za Mitaa na kwa uaminifu walioufanya tumepata asimilia 86.3 kwa ushindi wa viongozi wa vijiji. Tumekuwa wa tatu kwa ushindi wa viongozi wa Serikali za mitaa na tumepata asilimia 79.5 Kitaifa. Nadhani tuko namba za juu. Nawapongeza sana wananchi wa Mkoa wa Dodoma na wanachama wa CCM pia wa Dodoma Mjini kwa Mkoa wa Dodoma tumekuwa wa kwanza kwa ushindi kwa uchaguzi uliopita. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa pongezi kwa wananchi wa Mkoa wa Dodoma nimpongeze sana Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Mheshimiwa Margaret Sitta, kwa kazi nzuri anazofanya akisaidiana na Naibu wake pamoja na Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijamsahau Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Jenista Mhagama, pamoja na wanakamati wa Kamati hiyo kwa kazi nzuri waliyoifanya. Muswada tuliogawiwa mara ya kwanza haukuwa *volume* kubwa kiasi hiki, lakini najua ni utendaji wao mzuri kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wameweza kutengeneza Muswada mzuri ambao Wabunge waliotangulia kuchangia hawakuona kasoro nyingi. Nami sikuona kasoro nyingi lakini nina baadhi ya maeneo machache ambayo ningependa kuchangia. (*Makofi*)

Napenda niwaunge mkono Kamati na niungane nao katika aya ya 3.7 ambayo wamesema naomba ninukuu Mheshimiwa Mwenyekiti kwa ruksa yako, anasema katika sehemu ya saba; “Sheria imeweka adhabu ya mtoto atakayekamatwa akiuza bidhaa barabarani.” Tabia hii ikomeshwe kabisa katika jamii yetu. (*Makofi*)

Kamati inapendeza kwamba si mtoto tu anayetakiwa kupewa adhabu, bali hata yule mzazi. Nami nawaunga mkono kwa sababu mtoto hana uwezo wa kujiamulia kutokwenda shule akaenda kuuza bidhaa mitaani. Ni sisi wazazi tunaowatuma watoto wetu kwenda kuuza bidhaa kuacha shule na kwenda kufanya biashara ndogo ndogo, matokeo yake wanazoea biashara, watoto wanaacha kusoma, wanaacha kujiendeleza katika elimu. Kwa hiyo, mtoto mwenye umri wa kusoma shule atakayekutwa anauza bidhaa mitaani, Sheria imbane mzazi, sheria isimbane mtoto. Pamoja na mtoto kumbanwa lakini Sheria imbane mzazi kwa sababu mtoto huyu ametumwa. (*Makofi*)

Lakini kifungu cha 17.2 (2) pia imezungumzia hilo kwamba mtoto asiuziwe pombe, sigara wala dawa, mtoto anatumwa. Mtoto hana uwezo wa kwenda kujiamulia kununua sigara, mtoto anatumwa. Lakini Muswada huu pia ningependa uzungumzie wazazi wanaokwenda na watoto baa. Hivi nchi hii tunashindwa kuweka bango linaloonyesha kwamba mtoto haruhusiwi kuingia baa? Lakini wazazi tunakwenda na watoto baa, watu wazima wakishalewa wengine hawana adabu, wanamkumbatia mwana mama, anamkumbatia *bar maid*, anafanyaje, wanafanya vituko. Maneno ya ajabu ajabu, watoto wanasikia. Tunadhania kwamba maneno yale yanayozungumzwa baa hayawaathiri watoto, yanaawaathiri watoto sana. (*Makofi*)

Sisi wanawake hata tukilewa hatuwabusu wanaume, lakini wanaume wanafanya hiyo kazi, wakishalewa wanakosa adabu lakini siyo wote. Lakini wapo, wanaowashika wanawake maeneo ambayo siyo mazuri, wale watoto wanaona. Wazazi wanaokwenda na watoto baa ifike wakati sasa wa kwamba watoto wasiende baa. Hata maeneo ya kuogelea, wazazi wanakwenda kwenye maeneo ya kuogolea, hebu fikiria umevaa kile kibukta kile cha kuogelea unaonekanaje mbele ya mtoto wako?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata mimi mama nikivaa nguo ya kuogelea mbele ya mtoto wangu naonekanaje? Mimi naona hili pia liangaliwe. Muswada huu uangalie watoto wanaokwenda baa na wanaokwenda maeneo ya kuogelea watu wazima. Kuna maeneo ya kuogelea watoto. Lakini maeneo ya kuogelea watu wazima, watoto tunawapa picha gani, tunawafundisha kitu gani? Lugha zinazotumika katika maeneo ya starehe na

sisi wazazi maeneo ya starehe watoto wanacheza shoo, wanakatika mbele za wazazi, sisi wazazi ndiyo wa kwanza kwenda kuwatunza. Je, tunawafundisha nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtoto anapokatika mbele za wazazi, mbele za umma, halafu wewe mzazi au wewe unayestahili kuwa mzazi wake ndiyo wa kwanza kwenda kutunza, tuangalie Muswada huu utasaidiaje katika hili kwamba hatuwadhalilishi watoto kwa sababu wewe mtu mzima unayekwenda kumtuza mtoto unaona aibu kwenda kukatika pale mbele, lakini mtoto anapokatika unakwenda unamzawadia. Tunawadhalilisha watoto wetu, tunadhani tunawafundisha kucheza vizuri. Lakini kucheza siyo kunengua tu. Hebu tuache kuwadhalilisha watoto wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie pia suala la kuasili mtoto. Mimi nina mfano dhahiri ambao nimeshuhudia kuna wazazi nilishaona baba mmoja alimuasili mtoto na wala siyo mtoto mmoja, aliasili watoto wawili. Lakini baada ya kufariki yule baba na kwa sababu yule baba ndiye aliyekuwa ana kazi, mama alikuwa mama wa nyumbani, ndugu wa yule mwanamme wakamfukuza yule mama, wakasema na watoto aliowaasili awarudishe alikowatoa. Watoto kama hawa wana haki gani mbele ya Sheria hii, mbele ya Muswada huu? Kwa sababu yule mama hakujua Sheria yoyote. Baba walikubaliana na mama na baba ndiye aliyekuwa amesema akawaasili wale watoto wawili, lakini baada ya baba kufa mama akaambiwa arudi kwao na wale watoto kwa sababu alikuwa tasa, walimwita hivyo hivyo kwamba wewe ni tasa hukuzaa, basi arudishe hawa watoto ulikowatoa, na nyumba yetu uturudishie. Mtoto kama huyu ana haki gani, mtoto kama huyu anasaidiwa? Naomba Muswada huu uangalie namna ya kuwasaidia watoto kama hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwa wale akina baba ambao muda mrefu wanawakataa watoto. Tunao katika maeneo yetu, wanakataa kabisa, pamoja na kwamba mtoto kufanana masikio, pua nini lakini wanawakataa. Hebu Sheria ione namna ya kuwasaidia baada ya kufanyiwa *DNA* na kutambulika kwamba mtoto ni wake, alipe gharama zile za nyuma. Mama huyu amehangaika kwa muda mrefu akitunza mtoto, akimlea mtoto, mtoto ana miaka 14 sasa, ndiyo anakuja kutambulika kwamba ni wa baba fulani, baada ya kutambulika baba alipe gharama, siyo amchukue mtoto tu kirahisi na akina baba wengi wamefanya hivyo, akimuona sasa mtoto ana kazi ndiyo anajipeleka kimbele mbele, wewe mwanangu, wewe binti yangu. Lakini ya nyuma hayo ya mtoto kusoma, mtoto kuhangaika, ya nini na nini, *school fees* hakugharamia, sasa Muswada huu uoneshe kwamba baba baada ya kufanyiwa *DNA* au baada ya baba kukubali kwamba mtoto ni wake basi alipe gharama, alipe gharama kwa huyu mama ambaye amehangaika kumlea mtoto kwa muda mrefu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa twende kwenye vifungu. Lakini nimepita kwenye vifungu kuna vifungu ambavyo sikuvielewa. Ukurasa wa 26 kifungu cha 40 kuna Sheria inasema kwamba, kama mtu ametenda kosa la kumuondoa mtoto, adhabu ambayo anastahili huyu aliyekosa haikutajwa. Mimi nadhani ingekuwa vizuri adhabu ikatajwa. Ukiangalia kifungu namba 146 kifungu cha 2(b) adhabu imetajwa kwa yule ambaye atamfanya Afisa Ustawi wa Jamii asitekeleze wajibu wake. Lakini katika kifungu namba 40 adhabu haikutajwa. Mimi naomba kujua kwa nini adhabu haikutajwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kifungu namba 43(1)(b) mstari wa mwisho ambao unasema *birth of the child* (f) ile sijui ina namna gani. Wanasheria ambao wametengeneza Muswada huu wanisaidie kujua maana ya ile (f) au kama kuna neno ambalo limepungua katika mstari huo. Lakini ukienda pia katika kifungu namba 49, mstari wa tatu ambayo ina maneo *of the child or an* sielewi maana yake, maana ya neno hili. Ninaona Mwanasheria alieandika, wanasheria wahusika wa Wizara waangalie neno hilo lina maana gani. Wao ni wanasheria inawezekana mimi kwa kutokuwa Mwanasheria ndiyo maana sikuelewa.

Lakini ukiangalia ukurasa wa 35 kifungu namba 66(1)(b) ukimaliza *parent* kuna *adopted* nadhani ni *child* wao wenyewe wanasheria wanajua, sijui ni *typing error*, lakini juu ya *adopted* hapo pia kuna neno ambalo silielewi. Sijui ni *the court*, sijui ni *the* maana kuna neno *coull*, maana yake silijui. Naomba wanasheria watusaidie 66 kifungu 66(1)(b) mstari wa pili kutoka chini na mstari wa tatu kutoka chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda tena katika kifungu namba 72(2) mstari wa pili amesema, nanukuu maneno machache, *respect of any arrangement that may* sijui ni *may all* au ni *mayor*, wanasheria wanajua watusaidie. Nimeona ni bora niyaseme haya makosa yasije yakaendelea hivi kwenye Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kwenye kifungu namba 74(4) sentensi inayoanza neno baada ya *the* sijui maana yake na sijui ni neno la Kiingereza. Lakini sidhani kama ni neno la Kiingereza. Kifungu namba 78(1) ukisoma sentensi yenyewe *a person shall not employ or engage a child* sijui ni *will* sijui ni neno gani, wanasheria watusaidie kama kuna neno limekosekana hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu namba 85(1) kushoto kwangu wamesema wameandika *registration or a child in industrial* sidhani ni *or* nadhani ni *of*. Inawekana ni *typing error* au inawezekana ndiyo lugha ya kitaalam sielewi. Pia kifungu hicho hicho 85(2)(b) mstari wa tatu kutoka chini inayoanza na *undertakings* ukisoma maneno ya pale mbele baada ya *building* kuna *nr*, nadhani kuna maneno yanayokosekana hapa. Naomba wanasheria wetu watusaidie kutengeneza Muswada wetu ukaonekana ni mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kifungu namba 96(4) neno la mwisho *welfare officer, all any tick person, tick person* sijui maana yake. Ninawaomba wenzetu watusaidie ili sheria yetu iwe na maana. Hata kifungu namba 97 mstari wa pili neno la mwisho, nimejitahidi kutafuta hili neno la Kiingereza nimeshindwa kulielewa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 49 wa Muswada huu kifungu cha 99(2)(b) *any other person who* nikaona ni 11 (3) au ni 11(3), *the court* halafu 11(3) *ay* sijui ni neno gani. Tunaomba hawa watusaidie ili Muswada wetu uwe na maana. Lakini kifungu cha 100 kifungu cha tatu mstari wa pili pia kuna *pj11 triple 1* sijui maana yake. Ninaomba Wanasheria yetu, au Wizara yetu itusaidie na pia kifungu cha 108 kifungu kidogo cha kwanza, ukianza ukurasa wa 51 kuna maneno ambayo



**MWENYEKITI:** Mheshimiwa inaelekea una Muswada wa zamani kidogo, ule ambao uko sasa mengi katika haya yamerekebishwa. Endelea Mheshimiwa.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nina Muswada wa zamani ninaomba radhi sana. Lakini ndiyo Muswada nilionao mkononi mwangu na ndiyo niliufanyia kazi. (*Makofi/Kicheko*)

Baada ya hayo machache, maana naweza kuendelea kufanya masahihisho kumbe yalishafanyiwa marekebisho muda mrefu. Lakini hata *Schedule of Amendments* niliyonayo mezani kwangu nimejaribu kupitia sikuona. Ndiyo maana nikaona nisaidie ku-*highlight* maeneo ambayo niliona kwamba yana kasoro. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache, nakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Felister Bura, kama nilivyosema kwa upande wa Waheshimiwa Wabunge mchangiaji wetu wa mwisho ni Mheshimiwa Dorah Mushi, baada ya hapo Mheshimiwa Naibu Waziri, Afya ajiandae kuchangia. Mheshimiwa Dorah Mushi.

**MHE. DORAH H. MUSHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwa mchangiaji wa mwisho. (*Makofi*)

Kwanza kabisa naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uzima nami nikaweza kuwepo siku ya leo na kuweza kuchangia hoja hii iliyoko mbele yetu. Vile vile nitoe rambirambi zangu za dhati kwa aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Ruangwa Mheshimiwa Sigfrid Ng'itu, na nawaombea familia hii, Mungu aweze kuwapa faraja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile naomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Mheshimiwa Margaret Sitta, Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya, bila kuwasahau Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa, Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii pamoja na Naibu Waziri Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, bila kuwasahau pia wataalam wote wa Wizara hizi mbili kwa jitihada zao kubwa walizozifanya katika kuhakikisha kwamba Muswada huu unakamilika na kuweza kuletwa mbele ya Bunge letu Tukufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi zangu hizi, naomba nianze mchango wangu na suala la watoto walioko katika mazingira hatarishi. Mimi ni Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Manyara ambaye ninawakilisha wananchi wa Mji Mdogo wa Mererani. Mji huu ni mji ambao umeathirika sana na ajira mbaya ya watoto walioko katika mazingira hatarishi na kutokana na wananchi wa eneo hilo wengi wao wakiwa ni wachimbaji wa madini ya *Tanzanite*. Lakini baada ya Serikali kuchukua uamuzi wake wa kuwapa machimbo yale kwa wawekezaji wakubwa na wawekezaji wale kutokuwapa ajira wananchi wazalendo wa mji mdogo wa Marerani. Hii imepelekea wanaume wengi kutekeleza familia zao na kuwaacha watoto kujikuta katika mazingira hatarishi. Vile vile

ugonjwa hatari wa UKIMWI umechangia kuwepo kwa idadi kubwa sana ya watoto yatima na ambao wameingia katika mazingira haya ambayo ni hatarishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo hili limeathirika kwa kiwango kikubwa sana. Hivyo basi Sheria hii itaweza sana kuwasaidia kutatua matatizo ya watoto hawa ili waweze kupata haki yao kwa urahisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nizungumzie suala la watoto walioko katika mazingira hatarishi ambao wengi wao ni watoto wa kike na idadi yao ni kubwa pia kuliko idadi ya watoto wa kiume. Ukiangalia matukio mengi sana ya watoto wanaodhalilishwa watoto wa kike ni wengi kuliko watoto wa kiume.

Hivyo basi, sikuona mahali ambapo mtoto wa kike ambaye yuko katika mazingira hatarishi amepewa kipaumbele. Ninazungumza hivyo kwa sababu watoto wengi wa kike wanadhaliwa kijinsia, wanabakwa, wanadhulumiwa, lakini utaona kwamba hakuna mahali popote mtoto yule anaweza kwenda kutoa taarifa zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jamii inaona mambo haya na inayamaliza kimya kimya, eti wanaona kwamba wakitoa taarifa za mtoto aidha kubakwa, ni aibu. Kwa hiyo, mambo haya yanakuwa yameishia kwenye jamii kimya kimya bila kupelekwa katika vyombo vya kutoa haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimeshuhudia mtoto aliyebakwa na mzazi wake na akamuharibu sana, lakini yule mtoto mama yake anaficha ukweli akawa anaogopa hata kumpeleka hospitali akawa anamuhudumia yeye mwenyewe kwa kumkanda kwa maji ya moto. Mtoto ameharibiwa sehemu za siri, lakini kumpeleka hospitali hawezi, basi akawa ana mkanda kwa maji ya moto, eti anaogopa ni aibu. Ninaomba sasa kuwepo na upendeleo maalum wa mtoto wa kike ili anapopata adha ya kunyanyaswa kijinsia au adha nyingine yoyote ile ajue ni mahali gani atakwenda kutoa taarifa zake na ili aweze kusaidiwa, na ningeomba pia kwa kuwa watoto wengi wanaogopa kwenda polisi wengine wanaogopa magwanda ya polisi na pia wanaogopa wanapokwenda pale wanakutana na watu wengine labda na wanafunzi wenzao wa shule kwa hiyo ataogopa kusema kwamba amepatwa na tatizo. Kwa hiyo, mimi ningeona kwamba pawepo na kitengo maalum kwa ajili ya watoto kutoa taarifa zao kwa uhuru zaidi na waweze kupewa kipaumbele na upendeleo zaidi, naona hilo litasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nilikuwa nazungumzia suala la mtoto aliyeasiliwa na kwa kuwa Afisa Ustawi wa Jamii ndiye aliyepewa jukumu hili la kuhakikisha kwamba ulinzi wake na matunzo yake. Nilikuwa nataka niulize, Afisa Ustawi huyu wa jamii amewezeshwaje ili aweze kufanya kazi hii kwa ufanisi zaidi?

La pili nataka niulize, ikiwa Mahakama Kuu ndio imetoa kibali cha kumuasili yule mtoto na utakuta kwamba mtoto yule amepelekwa nchi za nje na kwamba yule aliyemchukua mtoto yule amepewa ni wa kwake kabisa na hakuna chombo chochote ambacho kitakuwa kinafuatilia kule nje, kwa mfano labda mtoto amepelekwa Ujerumani. Ni nani atakuwa anafuatilia masuala ya yule mtoto? Ni ubalozi, ni Afisa ustawi wa Jamii au ni nani basi? Inawezekana basi mtoto yule alipoasiliwa na kwenda nje ya nchi na wale

wazazi waliomuasili wakafariki yule mtoto akaingia kwenye matatizo, je, ni nani atakuwa anajua matatizo ya mtoto yule?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nilikuwa nataka niulize kwamba kwa kuwa Afisa Ustawi wa Jamii huyu amepewa majukumu yote ya kufuatilia na je, kwa wale walioasiliwa hapa hapa nchini Tanzania, ikiwa Afisa Ustawi wa Jamii, amefuatilia na akaona kwamba yule mtu aliyemuasili mtoto amekwenda kinyume na utaratibu au na makubaliano; Afisa Ustawi yule wa Jamii ataweza kupewa mamlaka kamili ya kuweza kusitisha uasili wa mtoto yule? Ingekuwa ni vizuri basi kama Mahakama ingempa uwezo, ingempa meno ya kusimamia kikamilifu yale makubaliano ili kwamba mtu akishindwa basi na yeye aweze kutoa mamlaka ya kusitisha uasili wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende tena kwenye suala la Mahakama inayoendesha kesi za hao watoto. Ningeshuri basi Mahakama itakayokuwa inashughulikia kesi za watoto iwe kama *Chamber Court*. Kesi za hao watoto zisiendeshe na za watu wazima. Kwa mfano, kesi ya mtoto isichanganywe na watu waliofanya ujambazi au masuala mengine, ningomba tu kesi hizi zitengwe yaani ziwe *specific* kwa ajili ya watoto tu. (*Makofi*)

Suala la matunzo na elimu kwa mtoto aliyezaliwa nje ya ndoa. Ie sheria ya zamani iliweka kiwango cha shilingi 100/=, sielewi ni kwa nini sheria ya sasa hivi haikuweka bayana kwamba mtu akizaa nje ya ndoa atatoa shilingi ngapi za matunzo ya mtoto yule kwa mwezi. Mimi ningona kiwepo kiwango kamili...

(*Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa Mzungumzaji*)

**MHE. DORAH H. MUSHI:** ...ambacho kimekubalika, na sio kukubalika tu...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dorah, muda hauko upande wako.

**MHE. DORAH H. MUSHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nimemaliza?

**MWENYEKITI:** Eeh, ndio.

**MHE. DORAH H. MUSHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nilijua muda hauwezi kukutosha kwa sababu wewe ni mdau mkubwa katika masuala haya ya watoto wanaoishi katika mazingira magumu na baadhi yao unawatunza, tunakushukuru sana Mheshimiwa kwa kazi hiyo nzuri. (*Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Mtoto Amina.

**MHE. DORAH H. MUSHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaomba Mungu amtunze na amlinde mikononi mwangu ili yule mtoto aweze kukua vizuri. Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, tunakutakia kila la heri kwa ajili ya maisha ya mtoto huyo mwenye ulemavu wa ngozi, ambaye umeamua kumtunza. Ahsante sana. (*Makofi*)

## **MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. JANETH M. MASSABURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, napenda kuipongeza Serikali, kupitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kwa hatua mbalimbali zilizochukuliwa na hatimaye kuletwa Bungeni kwa ajili ya kutunga Sheria ambazo zitamlinda mtoto wa Kitanzania. Kwa namna ya pekee, nampongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote waliohusika kuandaa Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kumekuwa na kesi nyingi katika jamii zetu zinazowatuhumu kina baba wanaowarubuni watoto wao wa kuwaza na kufanya nao mapenzi, hali hii ni mbaya na inamuathiri motto. Jamii inapotambua au mtoto mwenyewe kulalamika, jamii yetu inabaki kimya kwa kuogopa lawama au kutojali ama kutokuwa na uchungu. Je, Serikali inasemaje kwa kesi kama hizi au Sheria inasemaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, MAFATAKI BABA ambao huwanajisi watoto wao au wa majirani zao na wanapolalamikiwa, huwahonga wazazi wa kike wa watoto hao na mwishowe kesi hizo huishia kimya kimya bila hatua yoyote kuchukuliwa. Je, Serikali inaweza kuweka mpango wa kura za maoni kwa kila mtaa ili kuwabaini MAFATAKI hao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri watoto wawe na maadili mema ya Kitanzania na si kuwaacha kuiga mambo mabaya ambayo hayalingani na utamaduni wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono haja kwa 100%.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri Margaret Sitta, Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Nkya, Katibu Mkuu na Wataalamu wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971, inautata mkubwa hasa kwa malezi na matunzo kwa watoto wa aina mbili kama vile watoto wanaozaliwa nje ya ndoa na watoto wanaozaliwa ndani ya ndoa na kutelekezwa na wazazi wao, ama kwa kutengana au kuachana kwa wazazi, Sheria iangalie juu ya matunzo yao. Ni vema Serikali iweke angalau kiwango ili Mahakama iweze kutoa hukumu kwa kiwango kilichopendekezwa kwani gharama za maisha zimepanda sana na hususani watoto wengi hupewa mama ndiye awalee watoto, hasa gharama za matibabu, elimu na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama ya Watoto, elimu itolewe kwa wananchi kwa kutumia wadau mbalimbali ili wajue umuhimu wa mtoto kumpeleka kupata haki zake, hasa inapotokea ubakaji, uzalilishwaji wa watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haki za mtoto pia ziangaliwe kwa watoto walemavu wanaofichwa ndani, Sheria ilazimishe mtoto mlemavu kupewa haki zote na wale ambao wamefanya hayo, ni vema washitakiwe na Mahakama itoe maamuzi ya kifungo au faini kwa wazazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria isaidie kwa wale wanaotoa mimba, ashitakiwe mganga na mwanamke ambaye atabainika kutenda kosa hilo kwani faini itolewayo ni ndogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu kuwa na Wanasheria ambao watakuwepo Mahakamani, kutetea watoto pale ambapo hawakutendewa haki, au kunyimwa mirathi yake na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria iangalie jinsi ya kuwasaidia watoto ambao wameishi katika mazingira magumu hasa wale wanaoomba mitaani pamoja na wazazi wao. Ni vema Sheria ikamkamata mzazi ili achukuliwe hatua kali kama vile Dar es Salaam pale ‘Fire’ watoto ni wengi sana, hivyo, Sheria pia ikazie maeneo hayo, ambayo watoto ni wengi kwa nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazingira ya wale ambao wanakusanya watoto wanaoishi katika mazingira magumu na kujipatia fedha kwa manufaa yao. Serikali lazima ikague kwanza kabla ya kupewa kibali cha kufungua maeneo hayo, kwani wengi wao hukodi chumba kimoja na kuwaweka mchanganyiko. Watoto hao wasihamishwe toka Wilaya nyingine kwenda Mkoa mwingine wenye uwezo huo na kuhamisha watoto ni Serikali tu ambayo ina maeneo maalum ya shule zao.

Wafanyakazi wa Wizara hasa Maafisa Maendeleo, wapewe vitendea kazi ili watoe elimu kwenye vijiji, ili Sheria hii iweze kuenea maeneo yote hapa nchini na ufuatiliaji wake utakuwa na manufaa, kwani wao huishi na wananchi huko waliko.

**MHE. DR. MAUA A. DAFTARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa 100%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada umeletwa wakati muafaka, wakati huu watoto wengi wanakosa haki zao, wengi wako barabarani baada ya kupata mateso majumbani mwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada umekamilika na ni faraja kuona kwa wale wenye uwezo na nia ya ku-adopt watoto watapata nafasi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafuraha kuona Sheria itasaidia sana kuepusha ajira kwa watoto. Kwetu wazazi tunaona vijana wadogo wanaotumikishwa katika machimbo ya migodi na vito, wako wachache wanaojiriwa majumbani kama *House Girl* na kuwa vimada vya mabwana wenye nyumba na kwa malipo duni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, tunasemaje juu ya watoto wa mitaani wote walipo Tanzania na haki yao ya kusoma?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wale mama wa kambo wanaowachoma moto watoto wadogo, wanapoiba hata shilingi mia, adhabu itolewe, iwe kubwa ili kutoa funzo kwa wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *parental duty & responsibility*, pg 14, para 9 item (4), kwa wale watoto waliofiwa na wazazi wao na ndugu na jamaa za watoto hao wakakataa kuchukua jukumu la kuwalea kwa visingizio mbalimbali kwa mfano ugumu wa maisha, kutokuwa na kazi, shamba na kadhalika, je, tunasemaje? Ni vipi watoto hao watapata haki ya kulelewa ipasavyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mahabusu ya watoto izingatiwe na wasichanganywe na watu wazima na wasimamizi wao wawe Askari waadilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu umekamilika, umebeba mambo mengi yenye maslahi kwa malezi na makuzi ya watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote, hongereni.

**MHE. MGENI JADI KADIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kuchangia hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Waziri na Naibu Waziri pamoja na Katibu Mkuu na timu yote ya Wizara na wale wote walioshiriki, kwa kuchambua Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu umekuja wakati muafaka juu ya Sheria ya Mtoto kupata haki zake. Kwa kweli Muswada huu utamtetea mtoto kuondokana na uzalilishaji na utumikishwaji kwani idadi ya watoto wanaotumikishwa katika mazingira magumu, inaongezeka, kama vile kutumikishwa katika mashamba ya chai, kwenye migodi, uvunjaji wa kokoto na hata kufanyishwa kazi ya ukahaba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtoto ni lazima apate haki zake za msingi kama vile, malezi bora, afya bora, matibabu, elimu, haki ya kucheza na upendo ili awe huru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyombo vya habari vinafanya kazi nzuri ya kutoa habari kwa sababu mtoto atajua wajibu wake kama mtoto na hatakubali kunyanyaswa au kuonewa ama mzazi au mlezi pale atapopata matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtoto anataka apewe malezi mema na afundishwe maadili mema tokea mdogo, ajue kumstahi mkubwa wake, afundishwe juu ya kuishi na

heshima kwenye mavazi, kutembea saa za usiku, kwenda sehemu za starehe saa za usiku na kiwango kilichowekwa cha Shs.100/= kwa mwezi hakifai kabisa, kwa mtoto aliyezaliwa nje ya ndoa, naye ni mtoto na anahitaji matunzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Sheria hii itafsiriwe kwa lugha ya Kiswahili ili ifahamike na watoto nao waifahamu, wazazi nao wafahamu majukumu yao juu ya haki ya mtoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mchango wangu huu, naunga mkono hoja na nautakia mafanikio Muswada huu.

**MHE. DR. ABDALLAH O. KIGODA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria iweke msisitizo wa jinsi gani watoto *destitute* hasa vijijini wanavyoweza kuhudumiwa hasa katika kupata huduma muhimu za maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajira ya watoto ni “*out of desperation*”. Hivyo, kuwaadhibu watoto husika, haileti mantiki. Ajira hizi ni matokeo, Sheria ziangalie nini chanzo kinachowasukuma watoto hawa kuajiriwa na kutafuta *mechanism* za kuzuia ajira hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu watoto wa mitaani, inaweza kuwa ni tatizo la “*social vices*” sheria zilenge katika kupunguza na kuadhibu maeneo ya “*social vices*” na itakuwa ni njia mojawapo ya kuzuia hamasa ya kukimbilia mijini. Naunga mkono hoja.

**MHE. MHONGA SAID RUHWANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria iangalie uwezekano wa kuwa na *Family Court* ili iweze kuamua kesi za watoto kuliko ilivyo sasa kwani kesi zinazohusu watoto wanaofanya makosa ya kuvunja sheria bila kujua, zinafanyika katika mazingira ambayo yanamtisha mtoto kwani wapo Polisi na watu wazima wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria iangalie au iweke kifungu kinachokataza tabia mbaya za wazazi mfano kutukanana na watoto, kutukanana na watu wazima wenzao hata kupigana. Vivyo hivyo, wazazi kurudi wamelewa usiku wa manane na kutoleana maneno machafu na kupigana mbele ya watoto wadogo. Sheria itoe adhabu kwa vituo vya Televisheni vinavyoonyesha vipindi vya watu wazima na matangazo ambayo hayatoi maadili mazuri kwa watoto hasa masaa ya mchana hadi saa mbili usiku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtoto ana haki ya kumfahamu baba na mama yake. Lakini hivi sasa wazazi wengi hasa kina mama, huwa hawawaelezi ukweli watoto wao baba zao ni kina nani kwani wapo watoto wengine hufikia utu uzima bila kuwafahamu baba zao mpaka wafanye jitihada binafsi kumfahamu baba au mama yake. Hivyo kifungu kiainishe wazi kuwa ni kosa kumnyima mtoto haki ya kuwafahamu wazazi wote wawili. Hivyo, itolewe adhabu kali kwa mzazi atakayefanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Ndoa katika kipengele kinachoruhusu mtoto kuolewa akiwa na miaka 15 kwa ridhaa ya wazazi wao, kinachanganya kidogo yaani kuna *contradiction* kati ya Sheria ya Ndoa na Sheria ya Mtoto. Hebu suala hili liwekwe wazi kuwa mtoto haruhusiwi kuolewa mpaka afike miaka 18 na kuendelea. Hivyo, ile ya mwaka 1971, kipengele chake kife *automatic*, itumike Sheria hii ya Mtoto.

**MHE. FATMA OTHMAN ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza mimi naunga mkono hoja ya Muswada wa Mtoto na imeletwa kwa wakati muafaka. Suala la umasikini linachangia sana uharibifu kwa watoto wetu hapa nchini kwani kutokana na hali hiyo walezi wengi au wazazi huwa wanawatumikisha watoto kufanya biashara za kuuza bidhaa ndogo ndogo mitaani. Kwa kuwa sheria imetungwa kwamba hawa watoto wanaofanya biashara wafunguliwe kesi basi ingefaa na hao wazazi au walezi nao wakamatwe na kupelekwa kwenye vyombo vya sheria tofauti, isije ikawa kule alikopelekwa mzazi na mtoto akapelekwa huko huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la watoto wanaoishi kwenye mazingira hatarishi, watoto hawa ni bora kukamatwa na kurudishwa kwa wazazi au walezi wao kwani wengi wao huwa wanakimbia vijijini kutokana na hali ngumu ya maisha, hili litakuwa jambo la busara kuliko tukiwaweka kwenye vituo vya kulelea watoto. Sababu kubwa ya kuwarudisha makwao ni kupata malezi ya walezi au wazee wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu watoto kushtakiwa, hili suala sio zuri, mtoto anaposhtakiwa, anachanganyikiwa hasa akiwa anasoma lakini ikiwa hakuna budi basi asielezwe kuwa umeshitakiwa labda tutafute njia nyingine ya kumueleza ili asione kama anapelekwa Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi shule za *boarding* nazo zingekuwa zinafanyiwa uchunguzi kwani watoto wengi huwa wanapata mimba sana, hawa wanaoishi kwenye shule hizo na unapofanya utafiti, utaona wengi mimba wanapata kwa Walimu au marafiki wa Walimu. Ingekuwa vyema kukawa na ukaguzi wa Madaktari wanawake kwenda kila baada ya miezi sita kwa ajili ya uchunguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa Maofisa wa Ustawi wa Jamii na wao wawe na jukumu la kufika kwenye vituo vya kulelea watoto kwa kuangalia hali halisi ya vituo hivyo kwani vingi huwa havitekelezi yale ambayo wanayotakiwa kutekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kazi, mara nyingi sisi wazazi tuna matatizo kwani mtoto wa kike hata kama ana uwezo wa kusoma lakini akifika miaka kumi na sita huwa tayari ameshawekewa mchumba aolewe hata kama huyo mchumba ni mtu mzima.

Jambo lingine, mtoto kushirikishwa kwenye mambo ya kisiasa na kutumwa kufanya mambo kinyume na sheria. Mimi maoni yangu, yule mtoto akikamatwa aeleze Chama gani kimemtuma basi kile Chama ndicho kipewe adhabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto kupewa uhuru. Watoto wasipewe uhuru kupita kiasi kwani lazima huo uhuru uwe na mipaka na hiyo mipaka ielezwe wazi, uhuru wa



kupata habari basi zile habari zisiwe habari mbaya au kwenye vipindi vya TV wasionyeshe zile habari mbaya zinazomhusu mtoto au mchango watoto wasifundishwe ile michezo ya hatari kama judo au karate.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. MWINCHOUM A. MSOMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, nampongeza sana Mheshimiwa Margaret Sitta, Waziri wa Wizara hii inayohusika na watoto pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya, bila kuwasahau Katibu Mkuu, mama Mariam Mwaffisi, Wakurugenzi wake na vile vile Wizara ya Afya kwa maana ya Kamishna wa Ustawi wa Jamii, kwa mchango wao katika Muswada huu hadi leo kuingia Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika haki za mtoto na wajibu wa mzazi kumlea mtoto, iwe ni pamoja na uhuru wa kuabudu. Mzazi hana budi kulielewa hili ili kuendana sambamba na jambo la Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa na uhuru huo wa kuabudu mradi asivunje Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la elimu kwa umma ili kuitambua Sheria hii ikipitishwa na Bunge na Mheshimiwa Rais, ni jambo la muhimu sana. Ni matumaini yangu kwamba Wizara itahakikisha kwamba, suala hili linafanyika kupitia Redio, Magazeti na vyombo vingine vya habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazo *NGOs*, Mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali ya ndani na ya Kimataifa yanayojishughulisha na masuala ya watoto, Mashirika hayo nayo yatumike katika kusaidia kutoa elimu kwa jamii juu ya Muswada huu ambao utakuwa Sheria ya Mtoto. Aidha, kuwa mstari wa mbele kusaidia utekelezaji wake kwa nia ya kuwawezesha watoto wa Kitanzania kufaidika vyema na Muswada huu hasa katika kutoa msaada wa kisheria kila inapowezekana/inapobidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wafanyakazi wote wa Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kwa kuuleta Muswada huu muhimu. Mheshimiwa Mwenyekiti, ulinzi wa haki za watoto, ili kukidhi matakwa ya Mikataba ya Kimataifa, kuhusu haki ya motto, ni muhimu sana katika ustawi wa watoto wa Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu utajikita kuhusu uangalizi, matunzo na malezi ya mtoto kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na Sheria ya Mtoto ya awali kupitwa na wakati, jamii imepata kupitia kipindi kigumu ambacho uwajibikaji wa wazazi katika uangalizi, matunzo na malezi ya watoto ukawa siyo jukumu lao, matokeo yake tumepata

watoto wengi wa mitaani, kwa sababu malezi ya watoto hao yalibaki ama kwa mzazi mmoja (mama au baba) na mara nyingi ni kwa akina mama pekee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka ya nyuma (1960's na 1970's), Sheria ya Ustawi wa Jamii, kuhusu haki za mtoto, mahitaji ya matunzo ya watoto waliotelekezwa na mzazi wa pande moja hasa wanaume, Maafisa Ustawi wa Jamii (Mabwana au Mabibi Huruma kama walivyojulikana wakati huo), waliweza kufanya kazi kubwa ya kurudisha uwajibikaji wa makuzi ya mtoto kwa wazazi wa pande zote mbili. Hii iliwezekana kwa sababu sheria ilikuwa na nguvu ya kumwajibisha mzazi ambaye alikuwa na kipato kuweza kulipia matunzo ya mtoto kwa zaidi ya theluthi moja ya mapato yake, bila kuzidi kiwango fulani. Kutokana na kushuka kwa thamani ya fedha ya nchi yetu, adhabu hiyo ikawa haina thamani na kufanya maamuzi ya hao *Probation Officers* kutokuwa na *impact* yoyote, shilingi mia kwa mwezi kama gharama ya kulea motto, haina thamani leo. Napenda kuipongeza Wizara kwa kuzingatia jambo hili katika sehemu ya pili juu ya haki za mtoto kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto wote wanaojiita watoto wa mitaani, wana wazazi wao na wachache ni matokeo ya majanga ya maambukizi ya VVU. Lakini hali hii ikiendelea kubaki kama ilivyo watoto hawa watazagaa miji yote. Nashukuru Muswada umeliona hili na kuingiza katika Sheria ili kwa kiwango kikubwa watoto hao wapelekwe kwenye shule maalum kwa wale ambao tayari wameonyesha tabia mbaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi "*Approved Schools*" zilikuwepo miaka ya nyuma na zilisaidia sana kurekebisha tabia za watoto. Inasikitisha sana kusikia kwenye miji mikubwa kama Dodoma wapo watoto wanaovuta gundi kama njia ya kuzuia njaa, katika maisha yao ya mitaani. Wazazi ambao kwa makusudi watawaacha watoto wao kwenda kuishi mitaani lazima nao wachukuliwe hatua za kisheria. Shule ya watoto maalum (*Approved Schools*) zijengwe kila Mkoa kama siyo kila Wilaya kufuatana na uwezo wa Serikali.

Maafisa Ustawi wa Jamii wawe na "*role*" kubwa sana katika kushughulikia makosa ya watoto kuliko kutumia Jeshi la Polisi. Hii itajenga hali ya kuondoa uwoga kwa watoto na kujenga mazingira ya kirafiki kati ya Maafisa Ustawi na Watoto hao.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu muhimu kwa ajili ya kujenga Taifa bora baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu umekuja kwa kuchelewa kwa kuwa pengine kungekuwa na sheria nzuri ya mtoto tangu mwanzo kusingekuwa na mmomonyoko wa maadili kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, "Samaki mkunje angali mbichi" ni methali inayolenga kulelea watoto wetu wote katika maadili mema ya watoto ili jamii ya Watanzania wawe na msingi bora wa maisha. Kutokuwepo kwa sheria, kunasababisha maovu mengi kufanyika na watu wengi kukosa haki ya msingi. Sheria hii itapelekea kusajili watoto na

wanapokuwa wakubwa, inakuwa rahisi kushughulikia masuala mengi ya kimaendeleo na inakuwa rahisi kuratibu maendeleo ya watoto. Usajili na uandikishwaji utapelekea kupata takwimu sahihi ya sensa ya watu na Serikali kuweza kutoa maamuzi sahihi kuhusu “*population*” ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Mtoto pia inapelekea ukuaji mzuri wa watoto na hivyo kuweza kufuatia masomo vizuri na kuwa na Taifa lililoelimika. Pia ni rahisi kudhibiti kuwepo kwa watoto wa mitaani kama sheria hii itazingatiwa na wazazi pamoja na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria hii pia iwaguse wafugaji wanaonyima watoto kwenda shule, hasa watoto wa kiume. Wazazi wachukuliwe hatua kali wanapowanyima fursa watoto wa kiume kutokwenda shule. Pia iwaruhusu watoto wa kike kuwa na haki sawa ya kurithi mali ya wazazi, jambo ambalo sasa hivi halipo kwa watoto wa wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii 100%.

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza natoa pongezi kwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa kuleta Muswada huu. Haina shaka Muswada huu utapitishwa na kuwa Sheria bila tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 21, *Section 26*, kuna akina mama ambao huficha watoto baba zao. Kuna mila nyingine zinazokubaliana na uficho huo. Eneo hili limeelezwa kifasaha katika Muswada, mfano kama makabila mengine ni kawaida mtoto kuwa wa mama na siyo baba au mtoto kuwa wa mjomba hata kama ni wa ndani ya ndoa na pia mama ndiye mwenye mji na pindi mwanamke aolewapo, basi mume ni lazima aishi katika mji wa mke. Hali kadhalika wanapotengana, mume haruhusiwi kuondoka au kuchukua mtoto hata kama mtoto huyo angekuwa na umri unaostahili. Nachelea katika hili kwa sababu lina mwelekeo wa kumnyima mtoto haki zake za msingi. Hivyo basi, naomba eneo hili liangaliwe kwa undani, ni jinsi gani ifanyike ili kuokoa haki ya mtoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 15, *Section 12, Child Employment*, ninapenda kazi ziainishwe kwani kwa mtazamo wangu, kwa umri huo tajwa, kazi ambazo mtoto angeweza kufanya ni zile tu ambazo mtoto yeyote anaweza kufanya nyumbani na siyo za kuajiriwa na kupewa mshahara. Kwa ujumla kazi za kuajiriwa kwa mtoto zingeondolewa moja kwa moja. Kama ni kumsaidia, ni bora kuishi naye bila ya mshahara na kumpatia mahitaji yake kama mtoto yeyote apatavyo kwa mzazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hongereni sana.

**MHE. HARITH B. MWAPACHU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa fursa hii niliyoipata kuchangia hoja hii kuhusu Sheria ya Mtoto, ambayo ninaiunga mkono kwa asilimia mia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuchangia hoja, napenda kumpongeza Mheshimiwa Frederick Werema, kwa kuteuliwa kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na

Mheshimiwa Rais. Nimefanya kazi na Mheshimiwa Werema kwa miaka 10, nikiwa Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba kati ya mwaka 1995 hadi 2005. Mheshimiwa Werema ni mchapa kazi mzuri, mwadilifu, ni mweledi, mtu anayejiamini, msikivu na anayeheshimu watu wa rika zote. Naamini atakuwa mtu wa msaada mkubwa kwa Serikali na Bunge letu.

Aidha, nampongeza Waziri na Naibu wake, Katibu Mkuu na Watendaji wao, kwa kuandaa Muswada huu kwa kushirikiana na Wizara ya Katiba na Sheria. Muswada huu umechelewa sana kufikishwa Bungeni. Hata mimi kwa wakati nikiwa Waziri na aliyekuwa Waziri mwenzangu Mheshimiwa Dr. Asha Rose Migiro, hatukuwahi au tulikuwa kwa njia moja au nyingine kuuwasilisha Bungeni. Hongereni sana kwa uandishi mzuri wa Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninazo *observation* kadhaa kuhusu Muswada huu na nitashukuru iwapo Mheshimiwa Waziri Margaret Sitta atanipa maelezo na ufafanuzi kuhusu yafuatayo:-

Kwanza, ni uandishi wa Muswada huu. Kama Waziri alivyosema katika semina, huu ni Muswada ambao ni mpya kabisa toka enzi ya Uhuru wa nchi yetu. Kwa maoni yangu, lingekuwa jambo zuri na ingependeza iwapo kungekuwepo na utangulizi au *preamble*, angalizo, *background* ya Muswada huu kwa mfano, Katiba yetu inasema nini kuhusu mtoto, *Universal Declaration of Human Rights* kuhusu mtoto, *The Convention of the Right of the Child*, *The African Charter* kuhusu maslahi ya mtoto nayo inasema nini na *instruments* za kisheria mbalimbali nchini zinasema nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya *observation* hiyo, napenda kuomba Mheshimiwa Waziri Sitta afafanue masuala yafuatayo. Kwanza kabisa, Sheria ya Ndoa na Mirathi ambazo zinashabihiana na hii itakuja lini Bungeni na kwa hii inasema nini kuhusu *definition* ya mtoto? Mtoto akiwa bado yupo tumboni kwa mama yake, ni mtoto au kiumbe. Kwa vyovyote vile bado ana haki zake. Haki zake ni zipi? Pili, unaweza kukatisha maisha yake kwa mimba kutolewa, Sheria inasema nini? Tatu, siku hizi unaweza kumtambua mtoto aliyeko tumboni kwa kutumia teknolojia ya kisasa. Sheria hii inasema nini kuhusu suala hili? *Privacy* ya kiumbe au mtoto huyo iko wapi? Hii ni *right* ya wazazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanangu hivi majuzi ameniambia kuwa wanategemea kupata mapacha mwishoni mwa Desemba hii 2009 mmoja wa kike na mwingine wa kiume. *Is this correct?* Mila zetu zinakubali utaratibu huu? Mbona tunaingilia *privacy* za viumbe/watoto hao. Hao wanaofanya haya, yaani Madaktari wanayomamlaka gani kisheria? Sheria hii tunayoandaa inasema nini kuhusu hawa Madaktari? Hivi wanayo leseni ya kufanya “Utabibu” huu? Wanayo *right* gani ya kuchungulia uchi wa binti huyo mchanga?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe pia utakuwa unalifahamu tatizo la watoto wa kike wanapozaliwa, akizaliwa mtoto wa kike na wakiongozana Baba hulalamika, “wewe mama unazaa ma-*Bar maid* tu”. Kwa maana hiyo, iwapo Madaktari watawaambia wazazi

kuwa watoto wanao kuja ni hao, hawawezi kufanya hujuma, mathalani kutoa mimba au kuwauwa? Mbaya zaidi, ikionekana mtoto mtarajiwa ni mlemavu au zeruzeru huyu kiumbe analindwaje? Sheria hii inasema nini? Mheshimiwa Waziri, haya ni masuala mazito ambayo yanahitaji maelezo, kauli yako au ya Serikali ambayo yatatambuliwa Kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maoni hayo, napenda kumuuliza zaidi Waziri masuala yafuatayo, ukurasa kwa ukurasa. Baada ya kuzaliwa *definition* ya mtoto na haki zake ni zipi na wazazi wake ni wapi?

Hoja, mume akizaa na mtoto wa mkewe (sio mtoto wa mume) huyu bwana mzee anatambuliwa kama *parent* kisheria au vipi? Je, mtu, ndugu akizaa na dada yake au kinyume chake, huyu naye anaitwa *parent*, sheria inasema nini kwa wote hao wahusika? Aidha, yule ambaye anajitolea mbegu za kiume (manii) na mtoto akapatikana kwa kificho au la, mtoto huyo ni wa nani na yule aliyetoa mbegu anatambulika kama *parent*? Sheria inasema nini? Kwa hili, tumejifundisha vipi kuhusu watoto wa Michael Jackson?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nijielekeze kuhusu *right of child*, ukurasa wa 12 kuhusu umri wa mtoto. Kwa mujibu wa Muswada, mtoto ni yule ambaye umri wake ni chini ya miaka 18 na kwa maana hiyo kuolewa kwa binti ni katika umri huo huo. Hili linakingizana na Sheria za Kiislamu. Si ingekuwa vema vipengele hivyo vingesema, *subject to religious and traditional laws*”, Mheshimiwa Waziri anasema nini kuhusu suala hili?

Aidha, kwa vyovyote vile sheria inasema nini kuhusu uhuru wa mtoto kukubali au kukataa kuolewa. Hivi karibuni bibi mtu alijiuwa baada ya mjukuu wake kulazimishwa na baba mtu kuolewa. Sheria hiyo tarajiwa inasema nini? Anayo haki ya kukataa kuolewa? Hata kijana wa kiume anayohaki ya kukataa kuoa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tukiwa katika suala hili la *the right of a child*, suala la ukeketaji kwa wasichana linaangukia katika sheria fulani, je, mvulana ambaye hataki “kutahiriwa” ni katika umri gani ambapo atakuwa na haki ya kuamua kwamba kipande chake cha mwili kikatwe. Mheshimiwa Waziri naomba ufafanue kuhusu suala hili katika Muswada huu linaangukia wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo wazazi ambao hutaka kupima ubikira wa watoto wao ikiwa kwa msaada wa Madktari wao, hii ni sahihi? Sheria au Muswada huu unasema nini? Ni katika umri gani ambapo hawa wazee na Madaktari wanaweza kufanya uchunguzi huu? Hili ni suala ambalo linaonekana kuwa jepesi kwa wakati huu lakini sheria hii itazame mbele zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu una upungufu kuhusu haki ya mirathi kwa watoto. Miswada kuhusu ndoa na mirathi ingekuwa pamoja na Muswada huu wa Watoto. Serikali imekuwa na kigugumizi gani kuhusu masuala haya? Pamoja na upungufu huo, huu Muswada hauweki bayana “*the right to Parental Property*” na haujazingatia “*Islamic Law*” kuhusu suala zima la mirathi kuhusiana na watoto, jinsia na

kadhalika. Aidha, zipo sheria za kimila ambazo zinatamka namna watoto wanavyorithishwa mali za wazazi wao. Nini kauli ya Serikali kuhusu masuala haya? Je, nafasi ya mtoto wa nje ya ndoa ana haki ipi ya mirathi kwa ujumla? Sheria hii ingeweka wazi katika vifungu husika “*subject to religious and traditional laws ...*” Hapa sheria hii iko *vague-vague!*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria zetu zinaruhusu watu wa dini/madhehebu mbalimbali kuoana. Wazazi hao wakijaliwa kupata watoto, ni dini ipi kati ya wazazi hao wanapaswa kuifuata au kuiabudu? Ni katika umri gani wanayo haki ya kufanya maamuzi ya dini wanayoipenda, sheria hii haitamki suala hili!

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Sheria/Muswada huu maneno “*in the best interest of the child*” yametumika katika vifungu mbalimbali na yana uzito wake. Lakini maneno hayo hayajafanuliwa ni nini maana yake. “*What are the guiding principles?*” Ni vigezo gani hivyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *Part III, Care and Protection of Child*, linazungumziwa suala la *child trafficking*, lingepewa msisitizo wa kipekee. Nafahamu kuwa ipo sheria kuhusu hili na hapa ningependa kutumbukiza suala la mtoto ambaye ni *refugee* analindwa vipi na sheria hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 16(a) kinazungumzia kuhusu “*abandoned child*”. Hivi kama wazazi wakijarudi kwa sababu zozote zile, sheria inasema nini kuhusu haki ya wazazi au mtoto yule?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, naomba Mheshimiwa Waziri afikirie kuchapisha Matangazo (*Regulations*) kuhusu Muswada huu ili jamii ipate fursa ya kuchangia jinsi ya kuboresha utekelezaji wa Sheria itakapopitishwa.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze kwa dhati Mheshimiwa Waziri, Naibu na Katibu Mkuu, kwa maandalizi mazuri ya Muswada huu muhimu kwa kuliandaa Taifa letu la kesho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania kwa miaka mingi tumedanganyika na hali ya ulinzi na usalama uliomo ndani ya nchi, hadi kujisahau kwa madhara yanayoweza kuathiri tabia, makuzi na haki za msingi za watoto wetu. Lakini pia kwa kuzingatia mila na desturi za kwetu, tuweke wazi kuwa sheria zetu hazilazimiki kufuata tabia na malezi ya kigeni (ya kizungu).

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshauri Mheshimiwa Waziri atumie sheria hii kwa kuweka taratibu au kanuni ambazo zitatakiwa zitawanywe kwenye Halmashauri zote za Wilaya na Miji, maana sheria hii, siyo rahisi wote kuipata na kuelewa vilivyo na zaidi ya hilo ni tafsiri sahihi ya sheria yenyewe kwa lugha rahisi, itatakiwa iandikwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna umuhimu mkubwa wa sheria hii ikishapitishwa, kazi zifuatazo zifanyike. Kwanza, baada tu ya Serikali (Rais) kuidhinisha, Waziri aanze

bila kuchelewa, kuandaa vipeperushi na kufafanua vipengele vinavyohusika kwa kila sekta, vichapishwe na Wizara husika na siyo Wizara hii peke yake. Masuala ya ulinzi/usalama wa mtoto, Wizara ya Mambo ya Ndani iandae vipeperushi, masuala ya ajira, Wizara ya Kazi na Maendeleo ya vijana, masuala ya malezi, Wizara ya Maendeleo ya Jamii na masuala ya michezo/burudani, Wizara ya Habari na Michezo. Yapo mengi ambayo kwa kushirikiana na Wizara mbalimbali zingeweza zikatumia sheria hii, kuisimamia bila kuiachia Wizara moja kufanya kazi zote hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya kuwaachia watoto wawe wanazagaa mitaani, lipewe kipaumbele kwa kuelimisha wazazi kwanza juu ya athari ya kudekeza watoto wetu, kuendeleza tabia hizo ambazo zinaweza kuhamasisha watu wasio wema wakaanza mipango ya kuwabaka, kuwateka na hata kuwarubuni kwa kufanya kazi za udokozi mitaani. Mengi yamesemwa na Kamati zote husika pamoja na Wabunge waliochangia hoja hii nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi nyingi ziwafikie Waziri pamoja na Wizara, kwa kuleta Muswada huu kwa ajili ya kusaidia watoto wanaoishi katika mazingira magumu. Je, Muswada huu au Sheria unawasaidia vipi watoto ambao hawana misaada yoyote, kuanzia kwenye familia zao hawana wazazi, hata ndugu, Serikali au Muswada huu unawasaidia vipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Sheria hii itasaidia kuongeza miaka ya mtoto kuolewa kutoka miaka 18 hadi 25? Miaka 18 mtoto anakuwa mdogo ukilinganisha na hali ya sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna sheria inazungumzia kuhusu kuwafanyisha kazi watoto, je, wale ambao wana umri mkubwa kidogo, Muswada huu au Serikali imeainisha mshahara au kiwango cha kulipwa? Je, Serikali inawasaidiaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazazi wanaoozesha watoto wao wakiwa wadogo au kuwaachisha shule, iainishwe adhabu kwa mzazi au mlezi husika na iwe kubwa sana ili iwe fundisho kwa wote pamoja na wale wanaowafanyisha kazi za nyumbani na mateso wanayowapa watoto na wenyewe waadhibiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale wanaowazalisha watoto wetu wanawakataa je, Muswada huu utawasaidia kwa kutoa adhabu ili kupunguza migogoro ya kupelekana Mahakamani au kuwafanya watu kuogopa kuwapa watoto wetu mimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu unasemaje kuhusu watoto wanaopelekwa gerezani na kuwekwa pamoja na watu wazima ambapo hupata matatizo? Je, sheria inasemaje kuhusu wale watoto kupata haki yao? Adhabu zianishwe pamoja na watoto wanaozaliwa wakiwa walemavu, viongozi wawe na Sheria ya Mtoto, ikiwa hivyo wataishi na matumaini, watakuwa na kinga ya kuwalinda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada ukizingatia yote hayo, tutashukuru pamoja na wazazi wanaoficha watoto wenye ulemavu ndani, wanamnyima mtoto haki yake. Pia naomba vituo vilivyokuwepo vyenye malezi mazuri hasa tulivyokuwa navyo Mkoani Kagera vilifungwa, naomba virudishwe. Kuna watu wanajifanya wanalea watoto yatima huku ni kitega uchumi, hawana uwezo wa kulea watoto, wanateseka.

**MHE. AMEIR ALI AMEIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia uhai na uzima wa afya na kunijalia kuchangia Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Serikali kwa kuleta sheria hii ambayo ilikuwa inasubiriwa kwa hamu sana katika Bunge na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu ni mzuri na umeonyesha namna Tanzania inavyojali watoto kwa kuwalinda na kuwapa haki zao za msingi, lakini sheria hii tunayoitunga inatumika Tanzania Bara tu wale wa Tanzania Visiwani hawahusiki na sheria hii hadi iridhiwe na Baraza la Wawakilishi.

Ninaomba Serikali ya Muungano kupitia Wizara inayohusika wakutane na wenzao wa Zanzibar kulizungumzia suala hili kwa pamoja ili suala hili lipitie njia zinazohusika ili itakapopitishwa sheria hii kuwa sheria ipate kutumika pande zote za Muungano. Sheria hii kutumika upande mmoja tu wa Muungano naona tutakuwa hatukuwatendea haki watoto wote wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu umejitosheleza kwa vifungu vyote na mchango wangu unaishia hapo na naunga mkono kwa asilimia mia moja, ahsante.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Mheshimiwa Margaret Sitta, pamoja na Naibu wake, Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya, pamoja na timu yao yote katika kufanikisha Muswada huu. Shukrani za pekee, ziende pia kwa Wanasheria waliofanikisha kazi hii bila kumsahau Bwana Nzori kwa umakini wake na uzalendo wake pamoja na ubinadamu wake hivyo kumwezesha kuwa makini katika kazi yake, bila kuchoka wala kinyongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuwashukuru sana *WILAC*, *TAMWA*, *NOLA* na pia Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Jenista Mhagama pamoja na Makamu wake, Mheshimiwa Horoub Masoud, kwa jinsi walivyoweza na kushirikisha wadau mbalimbali na kuuboresha Muswada huu. Hii iliyofanyika ni kazi nusu, tunangojea Muswada wa Ndoa na Mirathi, tunaamini inawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msisitizo wangu ni kwamba elimu itolewe ili kutoa uelewa mpana kwa jamii na kuwezesha utekelezaji wake. Najivunia na kujisikia furaha kuwa ni mmoja wa wadau waliofuatilia Muswada huu kwa karibu na leo hii kuzaa matunda.



Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda kufahamu, kwa kuwa mfungwa ni sehemu ya jamii na pia mtekelezaji wa Muswada huu, kwa kuwa wengi wanakuwa na watoto, je, ni kweli mpaka sasa mfungwa akiwa jela hulipwa mshahara wa Shs.1 kwa mwezi? Kama ni kweli, je, pesa hiyo inawezesha kutoa matunzo kwa familia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mdumu katika kazi.

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi hii ya kuchangia katika sheria hii muhimu ambayo imeletwa kwetu leo. Pia nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri, Naibu Waziri na timu yao yote kwa kuweza kuandaa Muswada huu na kuweza kusomwa ndani ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto wetu wamekuwa wakiishi kwa shida kwa sababu kulikuwa hakuna sheria iliyokuwa inawatetea na wala kujua watoto ni nani. Kumekuwa na malalamiko toka kwa watoto wanaopatikana na makosa na kupelekwa Polisi au kwenye Magereza, wamekuwa wakichanganywa na watu wazima na matokeo yake watu wazima wamekuwa wakiwaingilia kimwili watoto hao (wavulana) ndiyo wamekuwa waathirika wakubwa katika hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na ongezeko kubwa sana la watoto wanaoishi katika mazingira magumu na sababu kubwa ni kuvunjika kwa ndoa za wazazi wao, ndiko kunakosababisha watoto hao kuzurura mitaani kuombaomba na hata kujiingiza kwenye mambo mabaya kama vile wizi, uvutaji bangi na kadhalika. Ila nashukuru Muswada huu umezingatia mambo mengi hasa lile la haki ya mtoto kupata elimu kama tunavyojua hakuna urithi mkubwa hapa duniani kama elimu. Katika hili, kinamama ndiyo wamekuwa wakibeba mzungo mkubwa wa kusomesha pale ndoa inapovunjika, wanaume hukimbia na kumwachia mama mzungo huo.

Pia liko tatizo lingine ndoa inapovunjika kinamama hukatazwa kuchukuwa watoto hata kwenda kuwatembelea huko wanakoishi. Hili limekuwa likiwaumiza sana kina mama, nategemea sheria hii ikipita, itatenda haki kwa wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niungane na Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusu watoto wanaolelewa bila ya kujua baba ni nani au mama yake mzazi ni yupi, tabia hii ni mbaya, kuwe na kipengele kinachomtaka mzazi kumweleza mtoto ukweli juu ya wazazi wake maana wengine hudanganywa kwa kuambiwa ameshafariki baadaye anapokuja kujua ukweli inamuumiza sana mtoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni kumezuka tabia mbaya ya wazazi wa kiume au walezi kuwabaka watoto wadogo. Suala hili limekuwa siri kubwa kwenye familia lakini yule aliyefanyiwa anakuwa amedhalilika sana na kuathirika na kumsababishia mtoto maisha mabaya pale anapokumbuka tendo alilofanyiwa na mzazi wake au mlezi, anaathirika kisaikolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 inaruhusu watoto wa kike wenye umri kuanzia miaka 15 waolewe lakini Muswada huu unasema mtoto ni chini

ya miaka 18 sasa hapa tufuate sheria ipi wakati Sheria ya Makosa ya Jinai inasema mtoto wa kike mwenye umri wa chini ya miaka 18 haruhusiwi kumfahamu mwanaume!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nategemea kupata majibu ya hayo niliyoeleza hasa lile la kinamama wanaoachiwa watoto kulea bila kupewa pesa za matunzo kutoka kwa mzazi wa pili.

**MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza sana Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kwa kuleta Muswada huu wa Sheria ya mtoto kwa muda huu ambapo haki za watoto zimeaonekana kukiukwa au kutokufuatwa kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo wimbi kubwa sana la *human trafficking* na hasa wahusika wakuu wakilengwa watoto kati ya umri wa miaka 10 – 18 na watoto hawa wengi wao hutolewa vijijini na kuletwa mijini kufanya kazi ya kuuza miili kupitia madanguro yaliyoshamiri sana mijini. Ni vizuri sheria hii ikatumika vizuri na kuzibana hizi danguro ili zikaondokana na biashara hiyo ambayo si tu haimtendei haki mtoto lakini pia imesababisha maambukizi makubwa ya Ukimwi katika umri mdogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hii pia ihusishe na kutoa adhabu kali kwa zile familia ambazo zina tabia ya kuoza wasichana katika umri mdogo sana kati ya miaka 12 – 18 ambapo mtoto huyu anakosa haki zake za msingi kama kupata elimu. Tukiitumia vyema sheria hii, tutaondoa wimbi kubwa la wanawake wanyonge katika jamii kwa ajili tu ya kukosa elimu kutokana na kuolewa katika umri mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hii itumike vizuri katika kupiga marufuku kuchanganya watoto na watu wazima katika Mahakama zetu na Magereza yetu kwani kwa kitendo kilichokuwa kikifanyika awali kimechangia kwa kiwango kikubwa kuwaharibu sana watoto wanapokuwa kwenye Magereza yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla Muswada ume-*cover* mambo mengi muhimu ambayo kwa kweli kama yatazingatiwa, yatasaidia sana kupatikana kwa haki za watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda Waziri anifafanulie ni sababu zipi zimepelekea mila potofu kama za masuala mazima ya ukeketaji kutokuingizwa katika Muswada kwani watoto wanapokeketwa yule mkeketaji anakuwa amempunguzia mtoto baadhi ya haki zake kwani mara nyingi zoezi hili hufuatiwa na tendo la kuozwa mtoto huyo na kumwondoa kabisa katika masuala ya elimu. Hivyo ingekuwa vyema sana kama Muswada huu ungeongelea adhabu kwa vitendo vya ukeketaji ambavyo humnyima mtoto haki zake za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. PROF. PHILEMON M. SARUNGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa pongezi zangu za dhati, kwa Mheshimiwa Waziri na timu yake, kwa kuleta Muswada huu muhimu mbele ya Bunge lako Tukufu ili uweze kupata baraka za Bunge

lako kuhusu utekelezaji wake. Muswada huu umeletwa wakati jamii yetu imepuuza na kusahau mila, desturi na malezi mema tuliyorithishwa na babu zetu. Nasema hongera Mheshimiwa Waziri, hongereni timu ya Wizara na Watumishi wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo, naomba kuchangia kwa kutoa ushauri/maoni katika maeneo yafuatayo ya Muswada. Sehemu ya Tano, mambo yanayohusu huduma kwa watoto kwa mfano afya (matibabu). Afya ya mtoto ndiyo nguzo muhimu katika kukua na kumwezesha mtoto aweze kufikia kiwango cha juu cha kipaji chake. Hivyo suala la afya lipewe kipaumbele cha kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto wanaoishi katika vituo vya kulelea watoto wapatiwe huduma bora ya afya kutoka kwa mabingwa, kila kituo kiwe na Muuguzi na Madaktari wawe wanafanya utaratibu wa kukagua mara kwa mara afya ya watoto. Iwepo *health port* kwa ajili ya huduma za kwanza na kwa ajili ya kutoa huduma wakati wa dharura. Kituo kisiruhusiwe kuchukua watoto bila kuhakikisha kuwa huduma za afya zinapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto wanaouza bidhaa mtaani. Wizara ifanye sensa katika miji yetu kwa kuanzia Dar es Salaam, kwa lengo la kupata idadi ya watoto wa mtaani pamoja na wazazi wao. Baada ya sensa, Wizara iwe na mipango kabambe ya kuwahudumia watoto hawa bila kikimbilia hatua za haraka ya kuwadhibiti. Watoto hawa hawakuamua kuuza bidhaa mtaani bali wamesukumwa na hali ngumu ya maisha. Ustawi wa Jamii utekeleze jukumu lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Pili ya Muswada, ndugu au mlezi anayejinufaisha kwa mali zilizoachwa na wazazi wa mtoto baada ya wazazi kufa. Kwa kuwa baadhi ya Wazazi wanapoteza maisha yao bila kuandika wosia, Kanuni ya sheria iwekwe itakayolinda mali zilizoachwa na wazazi kwa ajili ya mfiwa. Orodha ya mali isimamiwe na Wizara/Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia kumpongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake kwa kufanikisha ukamilishaji wa Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante.

**MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nampongeza Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta na Naibu wake, Mheshimiwa Dkt. Lucy Sawere Nkya, kwa kuwasilisha Bungeni Muswada huu muhimu wenye lengo kuu la kuboresha, kuhifadhi na kulinda haki za watoto nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maoni machache tu yanayogusa maudhui ya Muswada huu. Kwanza Ibara ya 4 ya Muswada huu inayoongelea “Maslahi bora ya mtoto” yaani “*Best interest of the child*”. Dhana hii inajitokeza sehemu kadhaa za Muswada lakini tafsiri halisi ya dhana hiyo haipo kwenye kifungu husika cha tafsiri. Kukosekana kwa tafsiri hiyo katika sheria, ni dhahiri kutazua mkanganyiko mkubwa wa

tafsiri kwa watendaji, viongozi na hata Mahakama. Katika nchi nyingine nyingi, upungufu huu haujitokezi kwa kuwa sheria husika inaeleza vipengele au masuala yanayohesabika kubeba “Maslahi bora ya mtoto”. Kwa mfano, ubora wa mahusiano ya mtoto na wazazi au walezi, wajibu wa msingi wa mzazi au mlezi kwa mtoto kwa mambo mbalimbali na kisaikolojia, uwezo wa hali na mali wa wazazi/walezi katika kutunza watoto, mahitaji ya msingi ya mtoto na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Nane ya Muswada inaeleza wajibu wa Serikali za Mitaa katika kulinda maslahi ya watoto kwa kuwa suala la mahitaji na maslahi ya watoto ni mtambuka (*cross – cutting*), utekelezaji wa sheria hii usiachiwe mamlaka moja tu – Serikali za Mitaa, bali uwe chini ya chombo mahsusi cha kisheria chenye uwakilishi mpana (wa Wizara cha Idara mbalimbali). Mfano, Wizara zinazoshughulikia masuala ya elimu, ufundi, ustawi wa jamii, michezo, utamaduni, afya, fedha na usalama wa raia, ziwakilishwe kwenye chombo hicho ambacho kitakuwa na majukumu mengi, yakiwemo:-

- (i) Kuandaa sera na mipango ya kuendeleza maslahi ya watoto;
- (ii) Kuweka vipaumbele katika utekelezaji wa mipango mbalimbali ya maendeleo ya watoto;
- (iii) Kusimamia, kuratibu na kuunganisha juhudi mbalimbali za kulinda na kuendeleza maslahi ya watoto;
- (iv) Kuunganisha juhudi za kutafuta ufadhili wa mipango na miradi mbalimbali ya kumwendeleza mtoto; na
- (v) Kusimamia utekelezaji wa mikataba mbalimbali ya kimataifa tuliyoridhia kuhusu watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, naunga mkono hoja.

**MHE. HAMZA A. MWENEGOHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumpongeza Waziri kwa kuleta Muswada huu Bungeni. Muswaada huu umechelewa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingawa Muswada huu unazungumzia umri wa mtoto kuwa ni miaka 18 lakini bado hii siyo tafsiri na msimamo kamili wa sheria zote zikitambua hizi. Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 inaruhusu mtoto wa umri chini ya miaka 18 kuolewa hapa tafsiri ya mtoto haikukamilika. Sheria hii inatakiwa kufuta vipengele vinavyohusu umri katika sheria mbalimbali. Sheria hii inajikanganya na ukweli kwamba mtoto anaruhusiwa kuajiriwa akiwa na umri wa miaka 14, je, Serikali inaporuhusu mtoto wa umri huu ambao ni chini ya miaka 18 maana yake ni nini? Hapa mtoto huyu hana elimu ya kuajiriwa, hajakomaa na wengi watakuwa ni wale wale ambao watafanya kazi za kuzurura na biashara za mitaani. Sheria hii hii vile vile inaruhusu mtoto kuolewa akiwa chini ya miaka 18. Sheria inayumba na kuonyesha haina msimamo wa sheria ya mtoto na haki za watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtoto na haki za watoto. Haki hizi ni nyingi sana za mtoto. Sheria iwe wazi juu ya haki za mtoto. Hizi haki zipo kwenye sheria mbalimbali. Sheria zote zifutwe ili hii sheria ya miaka 18 ibakie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania bado ni nchi masikini sana. Hivyo kumzuia mtoto asifanye kazi na kumtoza faini kubwa mtoto ambaye amekamatwa akiuza maandazi, hili ni jambo gumu sana kwa wananchi wetu. Hebu chukua mama aliyefiwa na mumewe na ameachiwa watoto sita. Kwa bahati mbaya hana msaada na anajitahidi kuishi na kumudu maisha kwa biashara ndogondogo kabisa. Kwa sheria hii, mama huyu hawezi kuwatumia watoto hawa katika kumudu maisha yao. Hii adhabu anayopachikwa mtoto iwe kwa mzazi ambaye ataweza kujieleza kwa nini?

Katika jumla ya haki za mtoto ni pamoja na kujaliwa na watu wazima na kupewa haki ya usafiri salama popote anaposafiri kwa vyombo vya usafiri vya umma. Hii itaongeza sana changamoto kwa Serikali kuanzisha taratibu njema za usafiri pote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii bado haijamwekea mtoto mazingira bora ya kulea watoto. Watoto wanahangaika barabarani kuombaomba. Watoto wanabakwa, watoto wanaolewa bado wangali wadogo mno, watoto wanafanyishwa kazi majumbani, watoto wengi wanatumiwa kuchunga mifugo na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto wanakutana na matatizo mengi ambayo chanzo kikubwa ni wazazi wao. Wazazi wao ni maskini sana. Kaya nyingi huishi chini ya mstari wa umasikini uliopindukia. Wazazi wengi huonyesha tabia mbaya mbele ya watoto wao hii ni pamoja na wazazi kupigana mbele ya watoto wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazazi wenye tabia za kulewa kupindukia na huonyesha tabia mbaya kwa watoto wao na watoto hupigwa na kukemewa ovyoovyo. Watoto wakilelewa katika sura ya upendo na malezi bora, mtoto anayeolewa katika mwelekeo huu, huwa na tabia ya kujiamini na kujiona huru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtoto wa Tanzania na pengine sehemu kubwa ya Afrika hunyanyasika sana wakati wa mirathi. Wasimamizi wa mirathi huwanyanyasa sana watoto. Mali za watoto hunyang'anywa ovyo ovyo hatimaye watoto huachwa bila ya kitu chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto hufanya makosa ambayo hulazimishwa kupelekwa Mahakamni. Mahabusu za watoto siyo nyingi nchini, hivyo watoto huwekwa pamoja na watu wazima. Hapa watoto hupata taabu na kufanyiwa vitendo ambavyo watoto hawa hawastahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii imesahau kabisa kuwafundisha kwa wingi Maafisa wa Maendeleo ya Jamii. Nchi hii Maafisa wa Maendeleo ya Jamii, ni wachache sana hapa nchini. Sasa wakati umefika kwa nchi kuwafundisha hawa Maafisa kwa jitihada kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia nafasi hii, kwa njia ya maandishi kumpongeza Dada yangu Mheshimiwa Margaret Sitta, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, bila kuwasahau Ndugu yangu Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya, Katibu Mkuu, Watendaji wote walioshiriki kuandaa Muswada huu pamoja na wadau wote walioshiriki. Napenda kukiri kwamba wamefanya jambo zuri sana kuleta Muswada huu ambao Watanzania wengi walikuwa wanausubiri kwa hamu sana tena wamejitahidi kuainisha vifungu vyake vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nitakuwa mchoyo wa fadhila endapo nitaacha kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Haroub Mosoud pamoja na wajumbe wa Kamati wote walioshiriki kuandaa maoni ya Kamati ambayo yamesaidia Wizara kukamilisha Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa, napenda kutoa rambirambi zangu kwa kifo cha Mheshimiwa Ng'itu, Mbunge wa Jimbo la Ruangwa. Naomba rambirambi hizi ziwafikie mjane wake, watoto wake, wazazi, ndugu zake, wapiga kura wake na Watanzania wote, Mungu ampunguzie adhabu ya kaburi, wote tulimpenda sana bali Mungu amempenda zaidi, amen.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu matunzo ya watoto wa nje ya ndoa ama baada ya baba kufariki au kumwacha mke, napenda kutumia nafasi hii, kuipongeza Serikali kwa kuweka kifungu cha kumbana baba kutoa matunzo kwa watoto ambao bado wana umri wa kukaa na mama yao. Ni ukweli usiofichika kuwa fedha iliyokuwa inatolewa kama matunzo ya watoto ilikuwa ndogo sana. Sasa sheria hii itatoa kiwango kinacholingana na uwezo wa baba pia kiwango kinacholingana na hali ya maisha kwa wakati huo. Ninaishauri Serikali kuweka bayana vigezo vya kuangalia kiwango cha kila baba kutoa kwa mtoto anayelelewa na mama ama mlezi mwingine. Bila kufanya hivi, bado hali ya huduma ya watoto itaendelea kuwa duni ama kiwango kiwekwe kwa wale akina baba wenye uwezo mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kuainisha haki za mtoto ambazo zitamsaida mtoto kupata kwa wazazi wake, jamii na Taifa kwa ujumla. Ni ukweli usiofichika kuwa mtoto ni wa Taifa hivyo lazima apate haki zake. Nimefarijika kuona haki nyingi zimeorodheshwa mfano kupatiwa mafunzo, mavazi, chakula, malezi mema, elimu, matibabu, huduma ya michezo, upendo wa wazazi, kupewa muda wa kupumzika na kadhalika. Ninaishauri Serikali kwa kuwa Sheria hii kutaja haki zote za mtoto sio rahisi basi kuwepo na maneno na kadhalika ili hata haki ambazo hazikuandikwa itakapojitokeza basi ipokelewe na vyombo vya sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo wazazi wenye tabia ya kuwatumikisha watoto kwa sababu zao ama hajazaa yeye ama kwa tabia ya ukatili au ulevi sasa sheria itawalinda watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali kutoa umri wa chini wa kuolewa, pia kutoa pendekezo kuwa umri wa mtoto wa kike au wa kiume utathibitishwa na Daktari bali wasiwasi ni pale mwanume anayetaka kumuoa anapozunguka kumhonga Daktari, Serikali iwe na mbinu za kufuatilia. Ninaomba Serikali pia itazame upande wa wanaume wazee wanaoaa mabinti wadogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana Serikali kuona umuhimu wa kujenga Mahakama za Watoto. Hivyo basi, napenda kuishauri Serikali kujenga Mahakama hizi mbali na Mahakama za watu wazima ili watoto wawe na mazingira rafiki na yenye dhamana na kuwawezesha kuwa huru kutoa maelezo yake ambayo yatasaidia kutoa hukumu inayostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza Serikali kwa kuwakumbuka watoto wenye ulemavu kwenye sheria hii. Ninaishauri Serikali kutenganisha haki za watoto wenye ulemavu wa muda mfupi na ulemavu wa kudumu. Hii itasaidia sheria kutambua haki ya watoto wenye ulemavu kwa makundi haya yote mawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada umeeleza wazi kuwa umri wa chini wa mtoto kufanya kazi ni miaka 14 nami ninaunga mkono, lakini ninapenda kushauri Serikali kutoa mfano wa zile kazi nyepesi ili iwe rahisi jamii kutambua kazi ambazo mtoto hastahili mfano kazi za usafi wa nyumba, kupika, kuosha vyombo, kumlea mdogo wake na kadhalika na siyo kazi kwenye migodi, kubeba zege, kuchimba mitaro na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kuna tatizo la watoto kutumiwa kuwa vitega uchumi mfano kutafutiwa wanaume, kufanywa kuwa mashoga, machangudoa n.k. Hii ni tatizo zito, sheria iweke adhabu kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuikumbusha Serikali kuwa mtoto hawezi kupatikana bila ya wazazi kuwa na ndoa hii. Ninaomba Sheria hii ya Mtoto iende sambamba na Sheria ya Ndoa. Hii itasaidia akinamama kupata haki pale ndoa inapokuwa na mgogoro au kuzaa bila ndoa. Kwani wanawake wengi hushindwa kulea watoto wanaotelekezwa na waume zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa angalizo kwa Serikali kuwa wako watoto watovu wa nidhamu, hivyo pamoja na kudai haki ama Serikali kuwapa haki zao pia na wao wadhibitiwe pale wanapokiuka sheria mfano dharau kwa wazazi, kufanya biashara, kukimbilia mijini na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumaliza kwa kuunga mkono hoja hii mia kwa mia.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Wizara na Mheshimiwa Naibu wake kwa kuwasilisha vyema Muswada huu, napenda kuunga mkono hoja 100%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia maeneo yafuatayo, kwanza, ajira kwa watoto. Kwa hakika inasikitisha sana kuona nchi yetu ina sheria mbalimbali zinazofuatwa katika kutenda haki lakini kwa upande wa watoto haitekelezwi vizuri.

Watoto wengi hawatendewi haki kwa kufanyishwa kazi nzito kama za migodini, mashambani na hasa biashara haramu za madawa ya kulevya na ujambazi. Watu wanaowaajiri watoto wapo wengi na wanafikia kuwanyanyasa kwa njia nyingi tofauti na kubwa kutokuwalipa mishahara yao ipasavyo. Kwa nini mtoto anayepaswa kupatiwa elimu ya kumuendeleza katika maisha yake anaajiriwa na kukoseshwa haki yake ya msingi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ndoa za utotoni zimekithiri sana katika maeneo mbalimbali hapa nchini kwetu. Hili linasababishwa sana na wazazi wenyewe kwa ajili ya tamaa ya fedha. Ni wazazi wangapi wamechukuliwa hatua kwa tendo la kuoza watoto wao? Tatizo hili ni kubwa sana kwa sababu linasababisha vifo vya watoto ambao hupata ujauzito (mimba) na kushindwa kujifungua salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa 100%.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia fursa hii, kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kwa kuleta Muswaada huu Bungeni. Muswada huu ni muhimu sana kwa sababu mbili, kwanza, tunatunga sheria ya kulinda haki za watu ambao kwa umoja wao hawana pa kuziombea, ni jambo la upendo wa hali ya juu. Ninaamini ni jambo linalompendeza Mwenyezi Mungu.

Pili, tunatunga sheria ambayo ndiyo itakayoandaa vizazi vijavyo vya Taifa letu. Ubora wa sheria utazaa Taifa bora. Sheria duni na hafifu itazaa jamii duni na hafifu. Ni kazi muhimu na nzito sana. Ni kutokana na uzito na umuhimu huu, ndiyo maana ninaipongeza Serikali kupitia Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizi, ninapenda kuonesha maeneo mawili ninayoyaonea mashaka katika kuyasimamia. Eneo la kwanza, ninao wasiwasi kuwa lipo kundi la watoto ambalo hatujaliongelea vizuri, fikiria juu ya mtoto ambaye hana au awe na familia kutokana na sababu ya aina yoyote anaamua kuishi kwa familia ya jirani au ya mbali na familia yake, je, ni baada ya kuishi na familia mpya kwa kipindi cha muda gani ili ahesabike kisheria kuwa ni wa familia mpya? Hili lisipooneshwa wazi si ajabu kijana huyu akapoteza haki zake. Ni baada ya kuishi kwa kipindi cha muda gani mtoto huyo atapoteza haki zake katika familia yake ya asili? Ninaomba ufafanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili, katika sheria hii je, nafasi ya jamii kumrudi mtoto anayekosea ikoje? Je, mtu anapomkuta mtoto wa jirani anatenda kosa la kibinadamu au kosa la kimaadili afanye nini? Amwangelie tu? Je, kila kosa lifanywalo na mtoto umfikishe mtoto kwenye Mahakama ya Watoto, mtoto akimkosea mzazi, mzazi aende Mahakamani.



Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoanza kwa kupongeza, namalizia kwa kupongeza Wizara hii. Ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia 100.

**MHE. ALI JUMA HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kuipongeza Serikali kupitia kwa Waziri, Mheshimiwa Margaret S. Sitta, Naibu Waziri wake, Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wake wote walioshiriki kwa namna moja au nyingine katika kutoa michango yao katika kufanikisha utayarishaji wa Muswada huu hadi leo umeweza kutufikia hapa Bungeni. Hongereni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze mchango wangu kwa kuzungumzia hali ya unyanyasaji kwa watoto ambao wanapata shida na matatizo makubwa mara wanapofiwa na wazazi wao hasa wazazi wao wanaume na ambao wanaacha mali na mali ile ikawa inatunzwa na ndugu wa marehemu. Muda mfupi tu baada ya kifo cha marehemu na wakati mwingine hata msiba unakua haujaisha, wana ndugu hao huanza kugombana wao wenyewe kwa sababu ya mali na hatimaye kuwafanya watoto nao kuwa hawana pa kwenda na kubaki wanatangatanga na kupita kuombaomba mitaani hali ya kuwa marehemu mzazi wao alikuwa na mali nyingi ambazo kama zingetumiwa vizuri basi watoto hao wasingepata shida yoyote na wangeweza kupatiwa matunzo mazuri na mahitaji yao yote ya lazima kama vile elimu, makazi mazuri n.k kupitia mali iliyoachwa na mzazi wao. Lakini kutokana na ubaya wa nafsi unaofanywa na ndugu wa marehemu wa kuwadhulumu watoto yatima ndio hupelekea watoto kutangatanga ovyo mitaani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, kutokana na matatizo hayo ya kuwadhulumu watoto yatima, naiomba Serikali, kwanza, kuanzisha chombo maalum mfano kule Zanzibar ipo “Kamisheni ya Walemavu na Mali ya Amana”. Chombo hiki hutunza mali zote za mayatima hususani zile mali ambazo wanandugu wanaanza kugombeana hali ya kuwa warithi wake wapo lakini pengine kwa wakati ule wanakuwa bado wadogo, hivyo chombo hicho huzitunza mali za yatima mpaka pale wenyewe wanakuwa wakubwa na kuelewa kila kitu ndipo wanakabidhiwa wenyewe. Kama ni fedha wanafunguliwa “Accounts” zao kila mmoja hadi anakuwa mkubwa (mtu mzima). Inapotokea haja, matumizi ya lazima kama vile kulipiwa karo, kununuliwa nguo n.k. basi anakuwepo mtu maalum aliyekubalika na familia yote kwenda kuchukua fedha huko katika chombo husika. Jambo hili likitendeka basi kiasi kikubwa cha dhuluma za watoto yatima zitapungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ni kwamba Serikali itunge sheria ambayo itatoa adhabu kali kwa kila mtu ambaye atabainika kuwadhulumu watoto yatima mali walizoachiwa na marehemu baba/mama yao na kuwaacha wanatangatanga ovyo mitaani, kwa kufilisiwa na yeye mali zake zote na hata kufungwa jela ili na yeye aone ugumu wa maisha unavyokuwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nije katika suala la watu wenye tabia ya kuwatesa watoto ambao sio wa kwao yaani mama/baba wa kambo ambao wamekuwa na tabia hiyo ya kuwanyanyasa watoto kwa sababu tu sio wa kwao. Watu wa namna hii, ni wakatili na wanastahili kuadhibiwa vikali sana, kuna watu wanadiriki hata kuwachoma maji ya moto au moto wenyewe.

Naiomba Serikali ilete sheria Bungeni ambayo inasema wazi kuwa ikibainika mtu kamchoma moto mtoto basi na yeye achomwe moto kama vile alivyomchoma mtoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naishia hapa na naunga mkono hoja asilimia mia moja.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta (Mb), Waziri mwenye dhamana, Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya (Mb), Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara, kuandaa Muswada huu muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa maoni yangu kama ifuatavyo, naomba Muswada ubainishe mtoto ni nani yaani ukomo wa umri wa kuitwa mtoto. Haki za mtoto ziwe bayana, zinaanzia wapi na ukomo wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua za kisheria kwa wahalifu wa makosa ya watoto adhabu ziainishwe mfano:-

(a) Mama anayekataa kumnyonyesha mtoto kwa visingizio ambavyo havina ukweli hivyo kumnyima haki mtoto ya kunyonya maziwa ya mama (hii kwa wazazi wote wawili ikigundulika wanahusika);

(b) Sheria iainishe muda maalumu wa mama kumnyonyesha mtoto;

(c) Sheria iainishe adhabu kwa wale wanaotumikisha watoto kwa kazi za harabu, mfano, migodini, majumbani, viwandani na kadhalika; na

(d) Wajibu wa mzazi kumpatia mtoto huduma ya kielimu uwe wa lazima na wazazi wenye kukwepa wajibu sheria ichukue mkondo wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria hii imlinde mtoto wa mtaani hasa wale wenye kuondokewa na wazazi wawili. Sheria itamke namna ya kulazimisha mamlaka za Kiserikali zilizopo kwenye maeneo yanayokabiliwa na matatizo hayo ili watoto wasaidiwe kwa masuala muhimu kama elimu, malezi na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kadhalika sheria itazame wahalifu wa kimapenzi wanaofanya na watoto wadogo kwa pande zote mbili wanaume na wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MOHAMMED AMOUR CHOMBOH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naanza kumpongeza Waziri na Naibu Waziri na wafanyakazi wote wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu mimi kwenye Muswada huu ni kushauri Serikali kuweka mkazo juu ya Sheria ya kujamiiana hasa kwa watoto wanaopewa mimba na kubakwa, adhabu iwe kali zaidi ya sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maoni yangu, sasa imefika wakati wa kuchukua uamuzi wa kuzifanya kesi zote zinazohusu mtoto ikifika Mahakamani ipewe kipaumbele badala ya kufuata mlolongo wa kesi ya kawaida, ili kuepuka mtoto kukaa mahabusu ambako kwa kawaida huwa wanakaa na watu wazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii, ahsante.

**MHE. BAHATI ALI ABEID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, pamoja na Watendaji wote walioshiriki kuandaa Muswada huu wa watoto hasa ukizingatia watoto ndio Taifa la kesho, ikiwawekea mazingira mazuri watakua vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Sehemu ya Pili ya Muswada inatoa mwongozo pale mzazi anapofariki, ni kweli kuna baadhi ya wazazi wanapofariki, watoto wanaobaki hupata tabu sana na wengine hupoteza mwelekeo wa kupata elimu na wale wanaojifanya ni walezi kwa kuchukua mali za urithi wa watoto hawa bila ya kuwatendea haki watoto hawa basi mlezi huyo achukuliwe hatua zinazofaa na ndani ya Muswada huu sheria inasemaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tunao watoto wengi ambao huwa tunawaita watoto wa mitaani wakati mtoto huyu amezaliwa na mama na baba. Kwa kuwa tendo lililofanyika hapa la watu wawili halikuwa rasmi na mtoto akapatikana basi mtoto huyu huitwa mtoto wa mama na mama kama ni mdogo hawezi kumlea na kumtunza humtupa na kupelekea kuitwa mtoto wa mitaani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kuna vipimo vya kupima vinasaba vya binadamu basi ni rahisi kukusanya watoto hawa wanaoitwa wa mitaani na kuulizwa wazazi wake na ni wepesi kumjua mama na mama atamtaja baba aliyempa mimba na wafanyiwe kipimo hiki ikithibitika kuwa ni kweli basi mtoto huyu wamchukue na kumpa haki zake kama mtoto, lakini kwenye watoto hawa sheria inasemaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono Muswada huu.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuanza kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia. Pamoja na shukurani hizo, ninaomba pia nimpongeze Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wote kwa kutuletea Muswada huu. Ni vyema pia nimshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, kwa kutushirikisha vyema wakati wa kuchambua Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Muswada huu utoe fursa kwa kina baba kulea mtoto toka wakati wa mimba. Kina baba wapewe nafasi kuhudhuria *clinic (MCH)*

toka mwanzo na pia wapatiwe likizo ya uzazi ya mwezi mmoja. Kwa wale watoto wa mazingira magumu, Serikali itenge eneo lao la kumiliki kwani hawana wazazi wa kuwarithisha chochote. Naunga mkono hoja.

**MHE. MARIAM S. MFAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wa Wizara kwa kuandaa Muswada huu kwa makini ambao tulikuwa tunaubiri kwa muda mrefu. Sheria hii itasaidia sana kulinda haki za watoto na kuwashughulikia wanaovunja sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo, naomba nichangie mambo yafuatayo:-

(1) Sasa hivi kumezuka makundi ya watoto ambayo yanajihusisha na wizi na vitendo mbalimbali vya uhalifu na ninapenda kujua sheria hii imeliona hilo na kama haikuliona, ninashauri likumbukwe ili kujua ni nani atashughulikia kundi hilo ili kulinusuru na maisha mabaya;

(2) Naomba niipongeze Serikali kwa kuliona suala la watoto wanaozaliwa nje ya ndoa na kuliingiza kwenye sheria;

(3) Niipongeze vile vile sheria kuwa na Mahakama ya Watoto. Ni vizuri Mahakama hii ianzishwe mapema;

(4) Naomba niombe Serikali iwe na kitengo ambacho kitasaidia watoto wasiokuwa na uwezo wa kujieleza katika Mahakama wakasaidiwa na Maafisa Ustawi wa Jamii;

(5) Niombe Serikali iwasaidie sana kuwashughulikia wazazi wanaotelekeza watoto wao na matokeo ndio tunapata watoto wengi wanaishia mitaani; na

(6) Naishauri Serikali idhibiti utaratibu wa uanzishwaji wa kutunza na kulea watoto wadogo kwani baadhi ya vituo vimeanzishwa bila kuwa na maandalizi mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta (Mb), Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, nampongeza pia Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya na Katibu Mkuu wa Wizara, mama Mariam Mwaffisi na wataalamu wote wa Wizara hii, kwa kufanikisha kuufikisha Muswada huu hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo, napenda nichangie mambo machache kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya Bunge hili, ni kutunga sheria na kazi ya Wizara ni kutayarisha kanuni zinazosimamia utekelezaji wa sheria. Mara kadha Bunge hili

limetunga Sheria na Sheria (Miswada) hiyo kusainiwa na Mheshimiwa Rais kuwa Sheria. Tatizo kubwa hubaki Wizarani, kwani sheria huchelewa mno kuanza kutumika kwa sababu kanuni hucheleweshwa sana. Ombi langu kwa Mheshimiwa Waziri, ni kumwomba aharakishe utungaji wa kanuni ili sheria hii ianze kutumika mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria iliyopo sasa inaruhusu mtoto wa kike kuolewa akiwa na miaka 14 lakini Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inamtambua mtu mzima kuwa ni yule aliyefikisha miaka 18 na kuendelea, huyu ana haki zote kwa mfano kuchagua viongozi na pia kuomba kuchaguliwa katika baadhi ya nafasi za uongozi. Unapomwoza mtoto wa kike miaka 14, moja ni kuvunja Katiba ya nchi, ikiwa ni pamoja na kutoruhusiwa kwa mfano kupiga kura na kuomba kuchaguliwa katika nafasi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu, naomba sheria hii mpya sasa iondoe utata uliopo ili kuondoa mgongano wa sheria kuu ya nchi na sheria nyingine. Watu wote ambao wako chini ya miaka 18 wajulikane kama watoto na kuwe na tafsiri moja ya mtoto na siyo vinginevyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante.

**MHE. BERNADETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Wakurugenzi wote na Katibu Mkuu, kwa kuleta Muswada huu muhimu, Muswada huu unaonekana kuwa umeandaliwa vizuri ili kuweza kulinda haki za mtoto na kuonyesha *commitment* yetu ya dhati kwa mikataba ya kimataifa kuhusu mtoto tuliyoridhia, ni muda muafaka kuletwa kwa Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna watoto wanaopata shida, ni wale wanaofiwa na wazazi wote au baba na wakalazimika kulelewa na ndugu za baba yao. Kwa mara nyingi, mali za watoto hufujwa, hawapati malezi sahihi, wanaonekana kama watoto wa daraja la pili kwenye familia na pengine hunyimwa nafasi ya kupewa elimu bora. Je, sheria inasema nini kuhusu walezi wa watoto yatima hawa? Je, wanastahili kuchukuliwa hatua gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mimba za utotoni zimeongezeka sana, wanaume wanazaa na wasichana, wakipata mimba, wanaume hawa huwakana na kuwakwepa mabinti hawa. Hii husababisha mabinti wengi kukata tamaa ya kuishi na watoto wanaozaliwa hukosa matunzo na malezi ya baba. Kwa kuwa tatizo hili lipo nchi nzima na vinasaba vinapimwa kwenye Hospitali kubwa tu kama Muhimbili na kwa kuwa si wazazi wote wana nauli na uwezo wa kwenda mbali kote, je, ni lini Hospitali za Mikoa zitawezeshwa kupima vinasaba, ili kuondoa kero hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria hii imetungwa ili kumlinda mtoto wa Kitanzania, kulinda haki zake za msingi na kusaidia kuandaa mazingira ya kulelewa vizuri na hatimaye kuwa mtu kamilifu mwenye uzalendo wa nchi yake Tanzania. Sheria hii imebainisha kazi ambazo mtoto hatakiwi kufanya, kazi kama kuuza karanga

barabarani na kadhalika sisi Watanzania tuna tabia na utamaduni wa kuwafundisha watoto wetu kazi wakiwa bado wadogo. Mama anamfundisha mtoto kulima, kuosha vyombo, kuchanja kuni, kupika na kadhalika wakati mzazi anahangaika kutafuta vitu vya kutunza familia, watoto wetu tumewatumia kulinda nyumba, kuuza vitu vidogo vidogo kama mayai na karanga ili wasaidie kuchangia kipato cha familia.

Je, hamuoni kuwa tukimzuia mtoto baada ya saa za shule, kusaidia wazazi wake walio masikini, ni kitendo ambacho hakina tija na tunaiga mambo ya mataifa yaliyoendelea kabla ya muda wake? Je, hii haitachochea watoto wa Kitanzania kila kukicha kuwaona Mahakamani, kuwashtaki wazazi wao, eti wamewafanyisha kazi, kama tunavyoona huku nchi nyingine kama Amerika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hii, ibara ya 4(1), mtoto anatambuliwa kuwa ni yule mwenye umri chini ya miaka 18. Sheria ya Elimu inasema umri wa kuanza shule ni miaka 7, hivyo watoto wanasoma kwa utaratibu wa 7:4:2. Anatakiwa kumaliza kidato cha sita akiwa na umri wa miaka 20. Sheria hii kipegele cha 8(1), kinabainisha elimu kama haki ya msingi ya mtoto lakini Sheria ya Ndoa, inamruhusu mtoto wa kike wa miaka 15 kwa ridhaa ya wazazi wao. Sasa huyu mtoto wa miaka 15 ambaye kama anaendelea na masomo atakuwa yuko Kidato cha Kwanza, sheria hizi mbili zinakinzana. Mimi nashangaa, kwa nini wanaume wanataka kuwaoa watoto wadogo wa miaka hata 15, je, wamekomaa vyakutosha, watasoma lini? Napenda kujua kama Muswada huu unamlinda mtoto kwa nini Muswada huu huu unatoa mwanya kwa mtoto wa kike kuolewa katika umri mdogo kwani wakubwa hawapo? Je, angekuwa wako ungemruhusu aolewe akiwa na umri mdogo hivyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Margaret S. Sitta (Mb), Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kwa kuwasilisha Muswada huu muhimu sana kwa jamii. Muswada huu umekuja katika wakati ambao jamii inaona umuhimu wa kuweka mazingira ya kisheria ya kumlea na kumlinda mtoto. Naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Aidha, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Dr. Nkya (Mb), Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wakurugenzi wote, kwa kumsaidia Waziri kwa uaminifu na uadilifu hadi kumwezesha kuwasilisha Muswada wenye maudhui mazuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, napenda kushauri kwamba Waziri atakapotunga Kanuni (*Regulations*) chini ya kifungu 157, suala la ukaguzi wa Taasisi na maeneo wanakotunziwa watoto liwekewe utaratibu ili lisiwe la hiari bali la lazima. Naunga mkono hoja hii.

**MHE. ZULEIKHA YUNUS HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza natanguliza shukrani, kwa Wizara, kwa kuleta Muswada huu Bungeni na sasa kujadiliwa, Muswada ambao ulikuwa ukisubiriwa kwa muda mrefu na jamii kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli Muswada huu umeainisha mambo yote kuhusu mtoto ingawa kuna mambo fulani yanahitajika ufafanuzi zaidi kama suala la kuolewa na kuoa, yawe yanaanzia miaka 18 na kama bado anaendelea na masomo basi mpaka analize masomo yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ajira kwa watoto basi zianzie kuanzia angalau miaka 16 na ziwe ajira nyepesi nyepesi zisiwe za kwenye machimbo na kubeba mizigo mikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu fungu la fedha kwanza litakuwa wapi, Wizara ya Maendeleo ya Jamii au Ustawi, maana Wizara ya Maendeleo ya Jamii ndio inayomtambua mtoto na Ustawi wa Jamii ndio inayoshughulikia na kutekeleza, naomba nifafanuliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii muhimu ya Muswada wa Sheria ya Mtoto. Naipongeza Serikali kwa kuwajali watoto wa Tanzania, kwa kuhakikisha sasa kunakuwepo Sheria ya Mtoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Bodi ya Uratibu, kwa kupitia michango mbalimbali na maswali niliyouliza hapa Bungeni, nimekuwa nashauri Serikali kuanzisha Chombo Maalum cha Uratibu kuhusu masuala mbalimbali ya watoto, kwa vile sasa itakuwepo Sheria ya Watoto, ni muhimu kikaundwa Chombo cha Uratibu ambacho kitasimamia kwa ukaribu utekelezaji wa masuala mbalimbali ya watoto ikiwemo kupata haki zao. Ili kuhakikisha kwamba watoto wanashirikishwa, chombo hiki pia kihakikishe kwamba unakuwepo ushiriki wa watoto. Chombo hiki ikibidi kiwe chini ya Ofisi ya Rais au Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya sheria kupitishwa, kanuni zitengenezwe ambazo zitasaidia utekelezaji wa kutumika sheria hii, kanuni hizo zitoe usawa kwa watoto wote (*non discrimination*) ikiwemo ushiriki wa watoto. Umri wa watoto wa kuolewa uwe sawa kwa wavulana na wasichana (miaka 18).

Mheshimiwa Mwenyekiti, adhabu ya viboko iondolewe kwa watoto majumbani, shuleni au kwenye vituo vya kulelea watoto, kwani hii ni kuwanyima haki kwani adhabu hizi zimeacha watoto wengine wakiwa na ulemavu wa kudumu na kuwanyanyasa kisaikoljia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama ya Familia na Watoto zianzishwe ngazi ya Kata na Wilaya (*Family & children's Courts*) ili kusikiliza kesi zote zinazohusu watoto. Kata na vijiji zishughulikie matatizo madogo madogo yanayowakabili watoto na zile kubwa zipelekwe ngazi ya Wilaya (*Family & Children's Courts*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. ANIA SAID CHAUREMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia kwa maandishi Muswada wa Sheria ya Mtoto wa mwaka 2009 (*The Law of Child Act, 2009*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto pamoja na Naibu Waziri na Wataalamu, kwa kuleta sheria hii ili kuwalinda watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama za Watoto, ni vyema zikaongezwa ili kumlinda mtoto kwa sababu kuendelea kuhukumiwa na wakubwa kunamchanganya kisaikolojia na kushindwa kujieleza vizuri. Baadhi ya watoto, wanatabia ya ujeuri wa kupindukia, hutukana wazazi na hata kupigana nao, sheria pia iweke adhabu kwa watoto wa aina hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri sheria hii itafsiriwe kwa lugha ya Kiswahili ili kuwafikia walengwa na kwa wazazi iwe rahisi kuelewa, ikishapitishwa Muswada huu Kanuni nayo ifuate.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufanyishwa kazi watoto, elimu ya ziada itolewe kwa sababu baadhi ya wazazi wanashiriki kutumikisha watoto kutafuta kipato. Watoto waelimishwe na kutoa taarifa kwenye Serikali za Mitaa ili hatua za kisheria zichukuliwe kwa wazazi wa aina hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haki ya mtoto kucheza. Hivi sasa watoto hawana nafasi za kutosha kwa ajili ya michezo. Sheria iboreshwe kwa kuitaka Mikoa na Wilaya zote kutenga maeneo ya michezo kwa watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la Muswada huu kutoa dira katika kumlinda mtoto, kifungu cha 54(1), kuasaili mtoto, ni lazima maombi yapitie Mahakama Kuu, naungana na Kambi ya Upinzani kutokana na mazingira ya nchi yetu Tanzania ni kubwa, ni vyema maombi ya kuasaili mtoto yafanywe katika Mahakama za Wilaya, kutasaidia sana zoezi kwenda kiurahisi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, atafuatiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maendeleo, Jinsia na Watoto. Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kuweza kupata nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia sheria ya mtoto ya mwaka 2009.

Lakini kabla sijaanza kuchangia napenda kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kumpongeza sana Mheshimiwa Jaji Frederick Mwita Werema, kwa kuteuliwa kuwa Mwanasheria Mkuu na Mheshimiwa Rais, kwa hiyo, tunamkaribisha sana, tutampa ushirikiano. Lakini vile vile nachukua nafasi hii kuwapongeza sana wananchi wa mkoa



wa Tanga kwa kukichagua Chama cha Mapinduzi katika Serikali za Mitaa na vitongoji, nawapongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kwa masikitoko makubwa niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa pole kwa marehemu Mbunge mwenzetu Mheshimiwa Sigfrid Selemani Ng'itu, ambaye ametutoka tarehe moja mwezi Novemba, 2009. Tunawapa pole sana familia pamoja na wapiga kura wake, sisi tulimpenda lakini Mungu amempenda zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile nimpongeze sana Mheshimiwa mtoa hoja Mheshimiwa Margaret Sitta na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya, kwa Muswada huu ambao tumeshirikiana nao sana kwa kweli mpaka kufikia hatua hii. Niwapongeze sana na wale wote wafanyakazi wa Wizara zote ambazo walishirikiana ili kuweza kufika hapa. Baada ya utangulizi huo naomba niseme kwamba ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile Muswada huu umetugusa sana na sisi wa Wizara ya Afya, basi kwanza nitatoa maelezo kidogo ya ujumla lakini nikipata nafasi, pia nitajibu baadhi ya hoja ambazo Waheshimiwa Wabunge, wameuliza maswali ili kuweza kumsaidia Mheshimiwa Waziri na yale ambayo yatabaki basi yeye mwenyewe atamalizia wakati anatoa ile hoja yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, kupitia Idara ya Ustawi wa Jamii, ina wajibu wa kusimamia utoaji wa huduma mbalimbali za ustawi wa jamii zikiwamo huduma za mtoto. Huduma hizo zimekuwa zikitolewa kwa kuzingatia sheria mbalimbali zinazohusu haki na ustawi wa mtoto. Sheria hizo kwa mujibu wa Muswada huu wa Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009, zitafutwa kwa kuwa zilikuwa kwa kiasi kikubwa haziendi sambamba na taaluma ya ustawi wa jamii yaani *social work*, ambayo inalenga katika malezi, matunzo, ukuaji, usalama na ulinzi wa mtoto ndani na nje ya familia yaani *Holistic, Care, Survival, Protection na Development of a child*.

Kwa hiyo, kuna sheria hizi ambazo zitafutwa na sisi tulikuwa tunazifanyia kazi kama Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii; naomba kwa ruhusa yako nizataje kama Sheria ya Matunzo kwa Watoto Waliozaliwa Nje ya Ndoa, Sheria ya Kuasili ya Mwaka 1953, Sheria ya Watoto na Vijana, Sheria ya Makao ya Watoto na Sheria ya Vituo vya Kulelea Watoto Wadogo Mchana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua na kuzingatia hayo, Muswada huu wa Sheria ya Mtoto wa Mwaka 2009, unampa nafasi na uwezo wa kitaalamu Afisa Ustawi wa Jamii yaani *social worker*, kutoa huduma za kitaalamu za Ustawi wa Jamii kwa mtoto ndani na nje ya familia kwa kuzingatia miiko, mbinu na maadili ya taaluma na ustawi wa jamii. Kwa hiyo, kwa mujibu wa Muswada huu katika kufanikisha utoaji wa huduma za ustawi wa jamii kwa mtoto itahusisha ushirikishwaji na ushiriki wa wadu mbalimbali kutegemeana na aina ya tatizo na mahitaji ya mtoto katika mazingira husika. Serikali inatambua kwamba huduma za ustawi wa jamii hazijawafikia wananchi walio wengi, hata Waheshimiwa Wabunge hapa wamelisema, kutokana na huduma hizo kutokuwa sehemu ya mamlaka ya Serikali za mitaa.

Ili kukabiliana na tatizo hili, Serikali imefanya maamuzi ya kuzitoa huduma za ustawi wa jamii na kuzijumuisha katika mamlaka ya Serikali za Mitaa ili kusogeza huduma hizo karibu zaidi na wananchi. Aidha, Halmashauri za Wilaya, Miji na Manispaa na Majiji zimeanza kuajiri wataalamu wa Ustawi wa Jamii ili kukabiliana na upungufu huo uliopo.

Serikali kwa kushirikiana na Mamlaka ya Serikali za Mitaa itaendelea kuajiri wataalamu wa Ustawi wa Jamii ili kuboresha huduma katika ngazi mbalimbali. Aidha, Serikali itaendelea kutoa na kuboresha mafunzo ya wasaidizi wa Ustawi wa Jamii, yaani *para-social workers*, kwa ajili ya kutoa huduma katika ngazi za Kata na Vijiji na vile vile kuongeza udahili wa wanafunzi watakaosomea fani ya Ustawi wa Jamii hapa nchini. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Muswada huu kupitishwa na kuwa Sheria, Wizara yangu itaandaa kanuni za utekelezaji wa Sheria hii kwa kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na Serikali kwa lengo la kuhakikisha kuwa sheria hii inatekelezwa ipasavyo. Aidha, Wizara itaandaa mkakati wa utekelezaji wa masuala yote yanayohusu haki na ustawi wa mtoto kama inavyoainishwa katika sheria hii, uhamasishwaji wa wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na Halmashauri na jamii kwa ujumla. Ili kuhakikisha kwamba sheria hii inaeleweka katika ngazi zote na inaelekezwa na kila mdau katika suala zima linalohusu haki na ustawi wa mtoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo ya ujumla naomba sasa nijibu baadhi ya hoja ambazo Waheshimiwa Wabunge wamezisema ili kuweza kusaidia kuzijibu. Mheshimiwa mtoa hoja mwenyewe atataja waliochangia na kwa maana hiyo nitamuachia. Lakini nilitaka niseme tu katika hoja zilizozungumzwa na Waheshimiwa Wabunge, walikuwa wanazingumzia kwamba kwa mfano Kamati ya Maendeleo ya Jamii, ilishauri kwamba tafsiri ya maneno *child with disability* ijumuishe ulemavu wa kudumu, lakini vile vile *clutches* iongezwe katika Muswada huu. Kwa hiyo, Serikali tunasema kwamba tumechukua ushauri huo na hayo marekebisho ya Muswada yatafanyiwa kazi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala pia limesema kutokana na kuongezeka kwa maombi ya kuasili watoto na ili kupunguza mzigo Mahakama Kuu katika kusikiliza mashauri, Kamati ilishauri Mahakama za Wilaya na za Hakimu Mkazi zipewe mamlaka ya kusikiliza maombi ya kuasili mtoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepokea ushauri huu wa kuufanyia kazi katika Jedwali la Marekebisho. Lakini hata hivyo Mahakama hizi pamoja na Mahakama Kuu zitapewa mamlaka ya kusikiliza maombi ya kuasili watoto hususan pale yanapofanywa na ndugu wa karibu kwa mtoto huyo, kwa mfano kaka, baba au mama mdogo. Lakini uasili huu wa nje ambao tutausema kwamba unaitwa *open adoption* ndio utaweza kuruhusu, lakini vinginevyo uasili wa aina nyingine utabakia ndani au utabaki chini ya

Mahakama Kuu ili kuhakikisha kwamba haki za mtoto zinalindwa na kuamuliwa na mhusika aliye na uzoefu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo limezungumzwa ni kwamba ili kujenga uhusiano endelevu kati ya mtoto katika shule za maadilisho, wazazi waruhusiwe kumtembelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepokea ushauri huu lakini hata hivyo mara nyingi huwa tunawaambia wazazi waende kumtembelea mtoto katika eneo lile ambalo akiwa katika shule za maadilisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ambacho kilijitokeza vile vile kilikuwa kinazungumzia kwamba ili kumuondolea uwoga mtoto na kumjengea mazingira rafiki akiwa Mahakamani, Kamati ilishauri Mahakama za Watoto zijengwe mbali na Mahakama za kawaida. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepokea ushauri lakini hata hivyo katika kifungu cha 98 na 102, vimetoa masharti na mazingira ya Mahakama ya Mtoto na kutofautisha watoto walio katika ukinzani wa sheria na watu wazima. Kwa hiyo, hili nimelifuatilia katika Muswada wenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama za matunzo kwa shilingi 100/= bado ipo. Waheshimiwa wengi walilizungumzia hili. Lakini ni kwamba sheria iliyohitaji kulipia kwa shilingi 100/= inafutwa kwa kifungu cha 159(i)(a) cha Muswada huu na gharama za matunzo ya mtoto wa nje ya ndoa limezungumzwa hili lakini katika Ibara ya 44 ya Muswada huu tumefanya mabadiliko makubwa na kutoa muongozo utakaotumika na Mahakama itakapokuwa ikitoa amri ya matunzo; ambapo imeongezeka kuzingatia kipato cha wazazi na kadhalika. Kwa hiyo, katika Ibara hii imeelezewa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo nataka nilizungumzie ni lile lililokuwa linasema kwamba idadi ya Maafisa Ustawi wa Jamii imepungua. Nadhani hili nimelizungumzia pale, lakini pia lilikuwa linauliza shule za maadilisho je, ziko ngapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule ya maadilisho iko moja. Kifungu cha 21 kinampa mamlaka Waziri kutamka shule yoyote kuwa shule ya maadilisho. Lakini pamoja na kuwa na shule moja, tatizo bado sio kubwa; bado jamii yetu imezingatia maadili ya tatizo kwa hiyo, haja yake haijawa kubwa. Lakini kutokana na *law reforms* Serikali imeshaliona hilo na kwa sasa inaandaa mikakati ya kufanya kila kanda tuwe na shule ya maadilisho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni watoto wa mazingira magumu uasili wa afya za watoto walioathirika na UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili katika kila hospitali ya Mkoa kuna Maafisa wa Ustawi wa Jamii ambao wanaweza kuwabaini hawa na hivyo waweze kupata matibabu kama itakavyokuwa imeagizwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine lilikuwa limezungumzia juu ya haki ya mama kumnyonyesha mtoto, yaani mtoto ni lazima anyonye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipengele cha 9(iii)(a) kuhusu suala la kunyonyesha mtoto; Muswada wa Sheria umezingatia jambo la matunzo pamoja na maslahi bora ya mtoto katika kila uamuzi bora unaohusu suala hili. Hili linapatikana katika kifungu namba 9.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, Mheshimiwa Waziri atamalizia. Ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda nichukue fursa hii nimshukuru Mwenyezi Mungu, ambaye ameniwezesha kufika hapa na sisi wote kukutana leo. *(Makofi)*

Pili napenda nichukue fursa hii kuwashukuru wananchi wa mkoa wa Morogoro kwa kuchagua Chama cha Mapinduzi katika uchaguzi uliopita na napenda kwa njia ya pekee niwashukuru wale wote ambao wamehakikisha wanawake wote wamerudishwa kwenye kugombea kwenye nafasi mbalimbali wamechaguliwa kwa kishindo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda nimpungeze Mheshimiwa Jaji Werema, kwa kuteuliwa kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Naomba nimhakikishie kwamba tutampa ushirikiano kama inavyohitajika. Napenda niwashukuru wote ambao wamechangia Muswada huu kwa namna zote mpaka tukaweza kufikia katika hatua hii. Ni watu wengi wamechangia, Wizara nyingine zimechangia pamoja na Kamati na wadau wote. Napenda niwashukuru Waheshimiwa Wabunge, kwa michango yenu ambayo ni mizuri na pia imesaidia sana kuboresha Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shukrani hizo, sasa napenda nije kwenye hoja. Waheshimiwa Wabunge wengi wamechangia kwa mdomo na kwa maandishi, sasa nitapitia vipengele ambavyo tumeona kwamba vinahitaji ufafanuzi. *(Makofi)*

Wabunge zaidi ya nane wamechangia kuhusu hali na mazingira ya Mahakama ya Mtoto. Ushauri wao umepokelewa na kuzingatiwa katika Ibara ya 98 na ya 102 ya Muswada huu. Wengine wamependekeza ifuatavyo, wamependekeza kuwa kuwepo na Mahakama ya Familia na Watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini kwamba mtoto anapopata matatizo inakuwa ni vizuri pia familia ikashirikishwa au walezi pamoja na Afisa Ustawi wa Jamii, ili mtoto aweze kujisikia kwamba anapendwa na sio kwamba yeye anaonekana kwamba ni mhalifu. Lakini naomba kusema kwamba suala hili la kuwepo kwa Mahakama ya Familia au kutokuwepo ni ushauri ambao tunautoa ili Mahakama Kuu na wale ambao wanahusika waone kwamba kama inahitajika basi watatengeneza mchakato wa kuweza kuweka mazingira ya namna hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wamesema kwamba watoto wanapopelekwa Mahakamani wawepo watu wazima. Jambo hili limepokelewa na litapelekwa katika mamlaka husika kwa ajili ya utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mwanne Mchemba, amezungumzia juu ya tatizo la kutoa mimba. Ni kweli tuna matatizo hayo, na pia akashauri kwamba Mahakimu ambao watakuwepo katika Mahakama za watoto wawe ni wazee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la mimba, sheria ya Kanuni za Adhabu Sura ya 16 imebainisha wazi kuhusu makosa ya utoaji mimba kuwa ni kosa la jinai. Suala la mahakimu wazee kuwa katika Mahakama za Watoto; hili tutalifikisha kwa mamlaka husika waone jinsi ambavyo watalitekeleza, kwa sababu haliko kwenye mamlaka yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wengi wamezungumzia juu ya vyombo vya habari wanavyojihusisha au kushughulikia watoto. Wamesema kwamba kuwepo na mipaka ya kupiga picha na kuandikisha maelezo yoyote kwenye vyombo vya habari kuhusu watoto. Tunashukuru kwa ushauri huu na ninaomba kusema kwamba hii imezingatiwa katika kifungu cha 158 (i) (d) na (a). (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazazi au walezi watoe habari ambazo ni chanya, wengi wameandika *positive*, pale wanapotafuta watoto wao waliopotea. Tumepokea ushauri lakini ni suala la elimu kwa jamii ili wazazi au mlezi ambaye anamtafuta mtoto wake aweze kutoa maelezo ambayo yanaweza yakasaidia katika kumtafuta mtoto. Kwa hiyo, ninasema kwamba katika utekelezaji wa sheria hii, tutahakikisha kwamba elimu ya umma inatolewa ili vifungu ambavyo ni muhimu sana vya kueleweka katika jamii viweze kuzingatiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge kama watano wamezungumzia kwamba watoto wazuiwe kuingia katika *internet cafes* bila kuambatana na watu wazima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri huu umezingatiwa katika sura ya 16 ya Kanuni ya Adhabu na adhabu yake imetolewa. Kwa hiyo, tunachoomba hapa ni kwamba wazazi wazingatie hili kwa sababu ni mzazi ndiye anayempa mtoto hela za kwenda katika *internet cafe*, sasa kama mzazi anaona kwamba kuna umuhimu wa mtoto kwenda, basi ahakikishe kwamba anakwenda na mtu mzima kwa sababu tumeanza kuona madhara yake katika mmomonyoko wa maadili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa wengi, wamezungumza juu ya ajira kwa watoto, wanazungumzia hasa umri wa miaka 14 ambao umezungumziwa kwamba mtoto anaweza kufanya kazi; na wakasema kwamba basi hizo kazi ziainishwe vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepokea na limezingatiwa katika kipengele cha 77(i). Kipimo ni kuhakikisha kwamba ajira ni nyepesi na kujua ajira ni nyepesi nafikiri Maafisa wa Kazi watakuwepo na wahusika katika Wizara hii ya *labour* wamesikia na watashirikiana na sisi katika kuhakikisha kwamba tunapoandika Kanuni tunaweka hivi

vipengele na tunatekeleza kwa pamoja kwa sababu watoto ni wetu wote. Tafsiri ya kazi nyepesi imetolewa katika kifungu hiki na imezingatia mikataba ya Kimataifa, kwa hiyo, naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba katika Kanuni zetu jambo hili litajitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rai nyingine imetolewa na Wabunge kama wanne hivi, wanazungumzia watoto kuzurura na kuchunga ng'ombe. Ni kweli watoto wengi ukipita barabarani hasa unapotoka Dodoma, unakuta wanachunga ng'ombe, wengine wanachunga mbuzi bila kuwepo na ulinzi wa mtu mzima. Tumepokea ushauri, ila kwa sasa mazingira yataangaliwa kwa sababu ni lazima liende sambamba na kutoa elimu kwa wale ambao wanashughulika na ufugaji ili wajue umuhimu wa kulinda watoto. Pamoja na wao kuhakikisha kwamba wanapunguza ule mtindo wa kuzurura zurura na ng'ombe ili watoto waweze kutulia na kusoma shule. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge watano wamezungumzia faini kwa watumikishaji wa watoto. Wamesema kwamba ile faini iliyokuwa imetolewa haitoshi. Ni kweli; naomba niwahakikishie kwamba tumesharekebisha na kiasi kimeongezwa na faini sasa inakuwa ni kiasi kisichozidi shilingi 5,000,000/= na sasa naomba niwaambieni kwamba sisi tumeshatoa hilo lakini kifungu hiki kinategemea na jinsi ambavo hakimumu anayeendesha hiyo kesi atakavyotoa tafsiri yake katika kutoa adhabu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa hawa pia wamezungumzia juu ya haki za mtoto na wakashauri kiongezwe kifungu na kizungumzie haki kwa ujumla. Kuhusu masuala ya haki za mtoto yamezingatiwa katika sheria hii ili kuhakikisha mtoto anapata haki zote za msingi. Na masuala haya mahususi yamejitokeza katika sura ya pili ya sheria hii na sura ya tatu ya sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa wengi wamezungumzia, wametoa rai yao kuhusu umri wa binti kuolewa. Sheria itamke umri wa kuo na wa kuolewa, sheria ikataze watu wenye umri mkubwa kuo mabinti wadogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri kwamba suala hili la umri wa mtoto kuolewa au kuo, linahitaji kubadilisha Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 kwa sababu sisi tunasema kwamba mtoto ni mtu yeyote ambaye yuko chini ya umri wa miaka 18, kwa hiyo mtu ambaye yuko chini ya umri wa miaka 18 mtu atakayemwambia akaolewe ni kwamba anavunja sheria. Lakini kutoa wazi kinagaubaga kwamba mtoto aolewe baada ya umri wa miaka 18 au kuo ni katika sheria ambayo sasa hivi inaingia kwenye *white paper* ambayo ni sheria ya ndoa ya mwaka 1971. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamezungumzia juu ya adhabu ya viboko, Mheshimiwa Ledian Mng'ong'o na wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, adhabu ya viboko kulingana na utafiti uliofanywa na Tume ya Kurekebisha Sheria, imesema kwamba watu wengi ambao wamefanyiwa hiyo *survey* wamesema kwamba watoto ni lazima wapate adhabu kidogo ili mtoto ajue

kwamba kukosea, ni jambo baya katika jamii. Kwa hiyo tunachosema katika sheria hii ni kwamba mtoto asichapwe viboko kwa namna inayomdhalilisha na adhabu isipite kiasi. Katika kifungu cha 13 cha Muswada, kinaweka mipaka ya namna ya kumpatia mtoto adhabu. Kifungu hicho kinaeleza kwamba izingatiwe umri na afya na uelewa wa mtoto mwenyewe ambaye amefanya hilo kosa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo wamezungumzia Waheshimiwa Wabunge wengi ni michezo. Wengine wamezungumzia aina za michezo ambazo watoto wanatumika, wanaigiza kama wanaume ambao ni watoto wa kike na wakiume ambao ni watoto wa kiume. Kweli hilo tumeliona kwamba ni tatizo kwa hiyo tumepokea huo ushauri na litafafanuliwa katika kifungu kidogo katika kifungu cha 158. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haki ya mtoto ni jambo lingine ambalo tunalizingumzia na wamezungumzia Waheshimiwa Wabunge wengi ni watoto wawe na wajibu, tumelipokea na limezingatiwa na Muswada huu katika kipengele cha kumi na tano. Lingine ni haki ya mtoto kumfahamu baba yake, nafikiri hilo ni haki ya msingi kufahamu wazazi wake na hilo tumelizingatia na litaambana na ile sheria ya *DNA* pamoja na kulazimisha kuhakikisha kwamba mahakama na vyombo vya sheria vinawajibisha wazazi wa kiume kwenda kufanyiwa *test* ya *DNA*. (*Makofi*)

Jambo lingine ambalo nimeona kwamba ni la muhimu katika hili ni kwamba usajili wa watoto utasaidia kujua mtoto halisi na watoto wa mitaani na haki za mtoto kumiliki mali za wazazi wao, tumepokea ushauri huo.

Waheshimiwa wengi wamezungumzia juu ya haki ya mtoto kucheza na kupata burundani, hivyo viwanja vya michezo vipatikane. Suala hili tunashauri kwamba mamlaka husika ambayo ni Wizara ya Ardhi, pamoja na Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa waangalie namna ambavyo wataweka kanuni na sheria ambazo zitawajibisha jamii iweze kutenga maeneo ya watoto kucheza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine wamezungumzia juu ya akina baba wanaofanya mapenzi na watoto, kuna baba wazazi na mafataki, nafikiri suala hili ni kosa la jinai na liko chini ya kanuni ya adhabu ya sura ya kumi na sita toleo la mwaka 2002, kwa hiyo, hiyo ni kuvunja sheria tunaomba jamii ijitokeze kuwafichua hao watu. Wazazi wasiowajibika kwa watoto wao kiwepo kipengele maalum cha adhabu. Sheria imezingatia kifungu namba nane, ambacho kinatoa wajibu kwa mzazi katika kutoa matunzo na endapo mzazi anakiuka masharti ya kumtunza mtoto adhabu zinatolewa chini ya Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine kubwa zaidi ambalo tunaona kama ni muhimu ni haki ya mtoto kutoa maoni, kifungu cha 11 kinasomwa pamoja na kifungu cha 8(4) pamoja na kifungu cha 9(2) kinasisitiza kwamba watoto wapewe haki ya kutoa maoni kwa sababu ndiyo njia pekee ya kuwafundisha watoto kuwajibika na kufikiria kwa njia ambayo ni *very constrictive* na ndiyo sababu Wizara yetu imeunda mabaraza ya watoto ili watoto waanze kujifunza kuwa viongozi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, basi yale ambayo Waheshimiwa Wabunge hawakuyasikia hapa yatatolewa ufafanuzi na Mheshimiwa Waziri na sisi tutatoa jedwali ambalo tutawapelekea Waheshimiwa Wabunge linalofafanua mambo ambayo wametoa hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na naomba kuunga hoja mkono asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Naibu Waziri Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya kwa mchango wako, kabla sijamuita Mheshimiwa Waziri mtoa hoja naomba niwatambulishie wageni wawili ambao ninaamini watakuwa kwenye *Speaker's gallery*, *may I introduced two guests you are seated in the Speaker's gallery who are guests of the Minister for the Community Development Gender and Children they are Hemo Lakonnen, UNICEF Representative and Peter Canty from the UK. May I acknowledge your contribution to this bill, thank you very much. (Applause)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuhitimisha hoja ambayo iliwasilishwa jana. Napenda kutumia nafasi hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwa kuzungumza ndani ya Bunge lako Tukufu na Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa njia ya maandishi, wote tunawashukuru sana kwa michango yao ambayo itakuwa msaada mkubwa sana katika kurekebisha na katika matumizi ya sheria hii. *(Makofi)*

Kabla sijaendelea naomba nitumie nafasi hii ambayo hutaihesabu katika muda wangu kuwatambua Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hoja hii. *(Makofi)*

Wa kwanza alikuwa Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, wa pili ni Mheshimiwa Anna Maulidah Komu, Mwakilishi wa Kambi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Profesa Idris Mtulia, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Anna Lupembe, Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Margreth Mkanga, Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, Mheshimiwa Anne Killango, Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mheshimiwa Felister Bura na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda na Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, waliochangia kwa njia ya maandishi ni Mheshimiwa Janeth Masaburi, Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mheshimiwa Dr. Maua Daftari, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Abdallah Kigoda, Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya, Mheshimiwa Fatma Othman Ali, Mheshimiwa Castor Ligallama, Mheshimiwa Martha Umbulla, Mheshimiwa Mwanawetu Zarifi, Mheshimiwa Bakari Mwapachu, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Sevelina Mwijage, Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, Mheshimiwa Rosemary Kirigini,



Mheshimiwa Profesa Phillemon Sarungi, Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mheshimiwa Ali Juma Haji, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Mohammed Amour Chomboh, Mheshimiwa William Shellukindo, Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, Mheshimiwa Benardeta Mushashu, Mheshimiwa Shally Raymond, Mheshimiwa Mariam Mfaki, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Bahati Ali Abeid na Mheshimiwa Zuleikha Yunus Haji. (*Makofi*)

Naomba radhi kama kuna wengine nimekosea matamshi kwa bahati mbaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya Wabunge sitini wamechangia hoja hii, 24 wakiwa kwa njia ya kuongea na 86 wakiwa wamechangia kwa njia ya maandishi, tunawashukuru sana. Natanguliza kuomba radhi kwamba itakuwa vigumu kutokana na muda niliona kuwataja wote kwa majina kama walivyochangia lakini tumeyaheshimu mawazo ya wote na tumechukua na kama alivyoahidi hapo awali Naibu Waziri. Ni kweli tutaleta majibu kwa njia ya maandishi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba nianze kwanza kwa kujibu hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii baadaye na kisha nijibu hoja za Kambi ya Upinzani na zile za ujumla tu, kwa sababu za Mheshimiwa Mbunge mmoja itakuwa si rahisi kutokana na muda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii awali ya yote ilitoa pongezi ambazo sisi kama Wizara tumezipokea na tunashukuru sana. Wametupa nguvu mpya, ari mpya ya kufanya kazi. (*Makofi*)

Kamati ilishauri tafsiri ya maneno *child and with disability* ijumuishe ulemavu wa kudumu. Tumeupokea ushauri huo na umezingatiwa. Pia kulikuwa na maneno yaliyoongezwa. Neno lililoogezwa ambalo linasema *clèche, clèche*, ni mahali ambapo wanatunzia watoto wadogo, iongezwe katika Muswada, jambo ambalo limeshafanyiwa kazi na litaonekana kwenye *schedule of amendment*.

Pia Kamati ya Kudumu ya Maendeleo ya Jamii ilizungumzia juu ya sheria kutamka bayana kuwa pale mzazi wa mtoto anapofariki, ndugu au mlezi atakuwa na wajibu wa kumpatia mtoto haki zake zote za msingi kama mzazi, Serikali imepokea ushauri huo na pia suala hili litaongozwa na sheria za mirathi, pia kamati ilishauri kuwa kanuni zitakazotungwa chini ya sheria hii zitoe mamlaka za mtaa kutenga sehemu maalum kwa ajili ya michezo ya watoto. Kwa kawaida sheria hii itasomwa na sheria nyingine ambazo zinaainisha masuala yanayolenga kulinda haki za mtoto. Moja ya sheria hizo ni sheria ya afya ya jamii na wakati huo huo suala la kutenga maeneo ya michezo tutalifikisha rasmi kwenye Wizara zenye dhamana ya mambo ya ardhi na makazi.

Kamati pia ilitoa ushauri kwamba kutokana na kuongezeka kwa maombi ya kuasili watoto na ili kuipunguzia mzigo Mahakama kuu katika kusikiliza mashauri, Kamati ilishauri Mahakama za Wilaya na za Hakim Mkazi zipewe mamlaka ya kusikiliza maombi ya kuasili mtoto. Tumeupokea ushauri na kuufanyia kazi katika

jedwali la marekebisho. Hata hivyo, Mahakama hizi pamoja na Mahakama kuu zitapewa mamlaka ya kuasili watoto pale yanapofanywa na ndugu wa karibu wa mtoto, kwa mfano, kaka, baba mdogo na kadhalika, uasili wa aina hiyo katika marekebisho unaitwa *open adoption* na utaratibu wake utainishwa katika kanuni zitakazotungwa kwa ajili ya sheria hii. (*Makofi*)

Usaili wa aina nyingine utabakia chini ya mahakama kuu ili kuhakikisha haki za mtoto zinalindwa kutokana na kuamuliwa na mhusika aliye na uzoefu yaani Mheshimiwa Jaji, katika utoaji wa haki. Kamati ya kudumu pia ya Maendeleo ya Jamii ilishauri kiongezwe kifungu ambacho kitahusu haki ya mtoto kuabudu dini yake ya asili yake hadi pale atakapofikia umri wa kuchagua mahali pa kuabudu, yaani atakapokua zaidi ya miaka kumi na nane na kuendelea. Serikali imeupokea ushauri huo na umezingiwa katika jedwali la marekebisho kwa kuongeza kifungu kidogo 6 cha namba 53(4). Kamati pia ilishauri kuongeza adhabu ya faini inayotajwa katika kifungu cha 30 kutoka shilingi 50,000, hadi faini isiyopungua shilingi 100,000/= tumeupokea ushauri huo na umezingatiwa katika jedwali la marekebisho la kifungu cha 30(1) na kuongeza pia kifungu kidogo cha 2.

Kamati ilishauri adhabu itolewe kwa mtu yeyote anayempa bidhaa za kuuza mtoto ili iwe fundisho kwa jamii nzima. Serikali imepokea ushauri huo na umezingatiwa katika jedwali la marekebisho kwa kuweka faini isiyozidi milioni tano badala ya ile ya awali ya kifungu cha 14. (*Makofi*)

Kamati ilishauri kwamba ili kulinda haki za mtoto na kuhakikisha anakuwa na maadili mema, sheria iweke mipaka kwa vyombo vya habari katika kupiga picha na kuandika habari zinazohusu mtoto. Serikali imeupokea ushauri huo na umezingatiwa katika kifungu cha 158(1)(b) na (d).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea tunaomba radhi ya kutomtaja Mheshimiwa Ania Saidi Chaurembo ambaye alichangia kwa njia ya maandishi, samahani sana Mheshimiwa Mbunge.

Kamati pia ilishauri wazazi na walezi watoe ushirikiano pale wanapomtafuta mtoto aliyepotea, tumeupokea ushauri huo. Jambo hili linahitaji kutoa elimu kwa jamii ili ijenge tabia ya kutoa ushirikiano pale wanapomtafuta mtoto aliyepotea.

Kamati pia ilishauri kwamba ili kumuondolea mtoto uoga na kumjengea mazingira rafiki akiwa mahakamani mahakama za watoto zijengwe mbali na mahakama za kawaida. Serikali imeupokea ushauri huo na umezingatiwa katika kifungu cha 98 na kifungu cha 102 ambavyo vimetoa masharti na mazingira za mahakama ya mtoto na kutenganisha watoto katika magereza ya watu wazima yaani sasa watoto hawatachanganywa na watu wazima. Watu wazima wataingia tu wale walioruhusiwa. Pia kesi itaendeshwa baada ya kuhakikisha Afisa wa Ustawi wa Jamii yupo, kwa kuwa ana utalaam wa kumtuliza mtoto aongee bila uoga.

Pia kesi za watoto zitaendeshwa kwa siri na kwa lugha ya kitalaam *in camera*. Kamati ilishauri vipimo vya vinasaba vimhusishe na mama wa mtoto ili kupata uhakika wa mwenye mtoto pale anapotuhumiwa mama kuiba mtoto. Serikali katika kifungu namba 36(1) sheria ya kusimamia vinasaba vya binadamu ya mwaka 2008 imeweka utaratibu wa kutambua mzazi wa mtoto husika pale inapotokea ubishi kwamba nani mzazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia ilishauri ili utekelezaji wa sheria hii uwe na ufanisi, Maafisa Ustawi wa Jamii waajiriwe hadi katika ngazi ya kijiji na wapewe elimu kuhusiana na haki za mtoto. Serikali imepokea ushauri na Naibu Waziri wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ameshalitolea ufafanuzi kwamba wana mpango wa kuandaa Maafisa Ustawi wa Jamii wengi kadri ya uwezo wa Serikali.

Kamati ilishauri pia kwamba ili kujenga uhusiano endelevu kati ya mtoto awapo katika shule ya maadilisho Wazazi waruhusiwe kutembelea mtoto. Serikali imeupokea ushauri huo. Wazazi wanahimizwa kuwatembelea watoto wawapo katika shule za aina hii ili kujenga uhusiano endelevu na tabia njema kwa watoto. Napenda kulifahamisha Bunge lako tukufu kuwa wazazi hawazuiwi kuwatembelea watoto hao walioko kwenye shule maalum za kurekebisha tabia.

Natoa wito tena kupitia Bunge lako Tukufu na kwa Waheshimiwa Wabunge kuwatembelea watoto walioko katika shule hizo maalum za maadilisho.

Kamati pia ilishauri kwamba Sheria iainishe majukumu na wajibu wa shule za maadilisho. Tumepokea ushauri huu na utazingatiwa katika kutengeneza kanuni. Kamati pia ilishauri kwamba kutokana na umuhimu wa sheria hii, sheria hii itafsiriwe katika lugha ya Kiswahili na kuchapishwa katika Gazeti la Serikali ndani ya miezi 24.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeupokea ushauri huo na mara baada ya Muswada huu kuwa sheria Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto itawasiliana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili taratibu zianze za kutafsiri sheria hii katika lugha ya Kiswahili.

Kwa upande wa Kambi ya Upinzani, wao walishauri kwamba Mahakama katika uasili wa mtoto madaraka yahamishiwe kutoka Mahakama Kuu kwenda Mahakama ya Wilaya. Tumeupokea ushauri huu na kuufanyia kazi katika jedwali la marekebisho. Hata hivyo mahakama hizi pamoja na Mahakama Kuu zitapewa mamlaka ya kusikiliza maombi ya kuasili watoto hususan pale yanapofanywa na ndugu kama nilivyoeleza katika kujibu hoja za Kamati ya Maendeleo ya Jamii kuhusu *open adoption*. Lakini uasili mwingine kama nilivyosema utabakia katika mahakama Kuu.

Haki ya mtoto kumfahamu baba yake. Huu ni ushauri mwingine uliotolewa na Kamati ya Upinzani. Suala hili tumelipokea na limezingatiwa katika sheria, ibara ya 6.

Pia Kambi ya Upinzani ilishauri kwamba kifungu cha 8 (1) kimejirudia katika kifungu cha 8 (2) na kifungu kidogo cha 4. Kifungu cha sheria cha 8 (1) kinaweka msingi. Kifungu cha 8 (2) na kifungu 8 )4) vinaelezea wajibu wa kuzingatiwa katika kutimiza haki zilizopo katika kifungu cha 8 (1). Kambi ya Upinzani ilishauri pia kuwa

gharama za matumizi ya mtoto ya sheria ya matunzo ya mtoto wa nje ya ndoa shilingi 100/= ni ndogo sana.

Je, na kama itaendelea katika sheria hii mpya. Na inaelezea nini kufuatana na matunzo ya mtoto. Sheria ya kulipwa kwa shilingi 100 inafutwa. Ibara ya 44 imejibu na kuzingatia maoni ya Kambi ya Upinzani kwamba kiasi hicho hakitoshi ambapo gharama halisi ya matunzo ya mtoto yatazingatia kipato cha mzazi mwenye jukumu la kumhudumia mtoto, majukumu ya kifedha ya mzazi huyo kwa wana familia wengine na gharama za maisha katika eneo ambapo mzazi na mtoto wataishi.

Kambi ya Upinzani pia ilizungumzia michezo ya kuigiza ambapo mtoto wa kike anacheza katika nafasi tofauti na alivyo. Suala hili sisi tumelipokea na tumezungumzia kwa ujumla kwamba jamii na hasa vyombo vyote vinavyohusika katika kuonyesha michezo, filamu na kadhalika kwamba yale ambayo maadili yake yataathiri watoto yasionyeshwe. Kama itabidi basi iwe baada ya saa ambazo watoto wamelala hasa usiku. Lakini kwa kifupi maonesho yote yenye maadili yasiyo mema kwa watoto au inayoweza kuathiri kiisaikolojia watoto yasionyeshwe.

Kuhusu faini kwa watumikishaji wa watoto. Kambi ya Upinzani ilisema kwamba ni ndogo. Kiasi sasa kinaongezwa kuwa faini isiyozidi shilingi milioni tano ili kumwachia Hakimku kumtoza faini mkosaji kulingana na uzito wa kosa. Kambi ya Upinzani pia ilizungumzia kuhusu kifungu cha 19(7) kuiongeza kifungu kingine cha taarifa ya daktari wakati wa kupokea mtoto yaani kiongezwe kifungu kuhusu taarifa ya daktari katika kumpokea mtoto. Kifungu hiki ni tayari kimeongezwa.

Kambi ya Upinzani ilizungumzia pia kifungu cha 14 cha Muswada huu. Tayari kimefanyiwa marekebisho na kuongeza faini kiasi kisichozidi shilingi milioni tano kama nilivyosema hapo awali kulingana na uzito wa kosa.

Suala lingine lilihusu Muswada unaotoa mwongozo gani kuhusu umri wa mtoto kuolewa. Huu ni Muswada wa Haki za Mtoto, hauwezi kumzungumzia masuala ya ndoa. Kwa hiyo, umri wa kuoja na kuolewa haubadilishwi na sheria hii. Bado itakuwa kama sheria ya ndoa itakavyoeleza. Hata hivyo kwa kuzingatia unyeti wa suala hili Serikali, inaandaa utaratibu wa kupata maoni ya wananchi kuhusu marekebisho ya Sheria ya Ndoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kambi ya Upinzani ilizungumzia kuhusu ajira kwa watoto wenye umri wa miaka 14 ushauri umepokelewa na umezingatiwa katika kipengele cha 77 (1) yaani kipimo ni kuhakikisha kwamba mtoto anapewa kazi nyepesi isiyoweza kuathiri maumbili yake na makuzi yake na elimu kama anaendelea kupata elimu.

Suala la uchungaji wa mifugo liongezwe katika kazi hatarishi kwa mtoto. Kazi ya kuchunga ng'ombe inaweza kuwa kazi hatarishi au kazi yoyote ikijulikana kama kazi hatarishi au pale tu itakapokuwa imekidhi au vigezo vilivyotolewa na kifungu cha 77 (1) na kifungu cha (3) cha sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kumaliza maswali na ushauri kutoka Kambi ya Upinzani. Napenda kumalizia kwa kutaja masuala ya jumla tu. Kama nilivyosema si rahisi kupitia masuala yote yaliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu haki ya kutoa maoni, haki ya kutoa maoni ipo katika sheria hii. Lakini ningependa kukumbusha tu wazazi na walezi na wale wote watakaohusika na makuzi ya watoto. Maoni ya watoto yatategemea umri wake na yule mzazi anayemhusisha mtoto katika kutoa maoni. Naamini mzazi au mlezi ataangalia ni jambo gani analozungumzia. Mfano hawezi kuzungumzia kwamba tujenge nyumba au tusijenge nyumba na mtoto wa miaka mitatu au minne. Nadhani itategemea suala linalozungumziwa na umri wa mtoto. Mtoto atajibu vizuri kutokana na malezi anayoyapata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningetumia nafasi hii kutoa wito kwa wazazi/walezi kuhakikisha familia zetu zinazingatia malezi mazuri. Mtoto aliyelelewa katika maadili mazuri hata utoaji wake wa maoni utakuwa pia umezingatia maadili mazuri. Kwa walezi, wazazi na jamii kwa ujumla tuwalee watoto katika maadili mema. Maadili ya taifa yatategemea maadili tunayowapa watoto katika familia zetu.

Suala la chombo cha kusimamia sheria hili limetolewa na Waheshimiwa Wabunge wengi. Lakini nilitaka kusema kwamba hili ni suala la kiutendaji tu Mheshimiwa Lediani ni mmojawapo wa Wabunge ambao wamekuwa wakiutilia mkazo. Lakini suala hili sisi tumeliona ni la kiutendaji zaidi. Pale ambapo Serikali itakapona kwamba Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Ofisi Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa bado hawasimamii utekelezaji wa sheria ya mtoto vizuri basi inaweza kuamua chombo gani kifanye kazi hiyo. lakini mpaka sasa hivi tunaamini vyombo vilivyopewa wajibu huu vitafanyakazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafsiri ya mtoto ni mtu mwenye umri wa miaka chini ya 18 na ana haki ya kupata haki zake zote kwa sheria hii. Mtoto wa ndani ya ndoa au wa nje ya ndoa si la sheria hii.

Sheria hii katika sura ya pili imetoa pia wajibu wa mtoto kwa hiyo, watoto nao wana wajibu wao wa kushiriki katika masuala ya kifamilia, masuala ya kitaifa kulingana na umri wao. Kulikuwa na suala la kuwaficha watoto walemavu nadhani sheria imejieleza vizuri sana. Mheshimiwa Bujiku Sakila alilitilia mkazo sana lakini sheria imezungumzia vizuri sana. Watoto walemavu wanaofichwa na wazazi hili lipo sana katika kifungu cha 8 kwa hiyo, nataka kumtoa wasiwasi Mheshimiwa Zuleikha na Mheshimiwa Mkanga kwamba sheria hii imeeleza vizuri na adhabu isiyozidi milioni 5 kwa yeyote atakayehusika na kuficha watoto wenye ulemavu ili wasipate haki zao za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi napenda kumalizia kama nilivyoanza kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri kabla hujamalizia naomba kuwatangazia Wabunge, uwepo wa Mheshimiwa Mbunge wa Urambo Mashariki Mheshimiwa Samuel Sitta, katika nafasi yake. Baada ya hapo Mheshimiwa Waziri endelea umalizie. (*Makofi/Kicheko*)

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Nashukuru sana. Umenikumbusha yupo ahsante nachukua nafasi hii kumshukuru sana kwa ushirikiano wake. Nashukuru ofisi yake na Katibu wa Bunge kwa ushirikiano. Kwa kweli bila kupata ushirikiano wa Katibu na Ofisi ya Bunge Muswada usingesomwa jana na kukamilishwa leo. Lakini pia nichukue nafasi hii tena kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliotoa michango yao kwa kuzungumza na kwa kuandika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nimshukuru pia mwakilishi wa *UNICEF* ambaye ametambulishwa sasa hivi Hemo Lakonnen. Kwa kweli *UNICEF* wametusaia sana. Tumeshirikiana nao kwa karibu sana. *NGO* zote zilizohusika katika kutoa maoni tunawashukuru sana.

Lakini pia kipekee namshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Waandishi wa Sheria, *CPD* pia. Kwa kweli wametusaia sana Ndugu Kyuki hatutakusahau, Ndugu Nzori kwa ufafanuzi wake na Ndugu Richard. Kwa kifupi Ofisi ya Mwanasheria Mkuu imekuwa msaada mkubwa sana. (*Makofi*)

Kamati ya Maendeleo ya Jamii ikiongozwa na Mheshimiwa Jenista Mhagama na Makamu wake Mheshimiwa Haroub Said Masoud na wajumbe wote wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii wamekuwa msaada mkubwa sana, tunawaomba Wabunge ndani ya Kamati hii waendele kutupa ushirikiano waliotupa safari hii na safari zilizopita ambao kwa kweli utakuwa msaada wetu mkubwa sana katika kutimiza wajibu wetu ndani ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Mwisho kabisa kabla sijatoa hoja, natoa wito kwa wazazi na walezi wa nchi hii kwamba tuwajibike kuwalea watoto, kwanza watoto huwa hawatuombi tuwazae hakuna hata mtoto mmoja aliyepomba kuzaliwa na mzazi yeyote. Tunawaza sisi wenyewe, kwa kupenda sisi wenyewe, basi tuwajibike tuwalee na tuwape haki zao zote. Sheria hii imetoa adhabu kwa yeyote ambaye hatawajibika kamleta mtoto na asipowajibika Sheria hii inambana. Tuwalee lakini pia tuisahau maadili. Watoto walivyo ni kutokana na malezi yetu. Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na ninaomba kutoa hoja. (*Makofi*)

(*Hoja Ilitolewa iamuliwe*)

(*Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kumaliza masuala yote ya hoja yako na umetoa hoja na imeungwa mkono.

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**Muswada wa Sheria ya Mtoto wa Mwaka 2009**  
*(The Law of the Child Bill, 2009)*

Kifungu cha 1  
Kifungu cha 2

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilivyopitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 3

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 4

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 5  
Kifungu cha 6

*(Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 7  
Kifungu cha 8  
Kifungu cha 9  
Kifungu cha 10  
Kifungu cha 11  
Kifungu cha 12  
Kifungu cha 13

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilivyopitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 14

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 15

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 16

Kifungu cha 17

*(Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 18

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 19

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 20

Kifungu cha 21

Kifungu cha 22

Kifungu cha 23

Kifungu cha 24

Kifungu cha 25

Kifungu cha 26

Kifungu cha 27

Kifungu cha 28

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilivyopitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 29

Kifungu cha 30

*(Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 31

Kifungu cha 32

Kifungu cha 33

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilivyopitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*



Kifungu cha 34  
Kifungu cha 35  
Kifungu cha 36

*(Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 37  
Kifungu cha 38

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilivyopitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 39

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 40  
Kifungu cha 41  
Kifungu cha 42

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilivyopitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 43

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 44

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 45

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 46  
Kifungu cha 47  
Kifungu cha 48  
Kifungu cha 49  
Kifungu cha 50  
Kifungu cha 51

*(Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 52

Kifungu cha 53

Kifungu cha 54

Kifungu cha 55

Kifungu cha 56

*(Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 57

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 58

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 59

Kifungu cha 60

Kifungu cha 61

Kifungu cha 62

*(Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 63

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 64

Kifungu cha 65

Kifungu cha 66

Kifungu cha 67

Kifungu cha 68

Kifungu cha 69

Kifungu cha 70

Kifungu cha 71

Kifungu cha 72

Kifungu cha 73

*(Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 74

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 75

Kifungu cha 76

*(Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 77

Kifungu cha 78

Kifungu cha 79

Kifungu cha 80

*(Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ki

fungu cha 81

Kifungu cha 82

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba katika hizi kazi hatarishi kifungu namba 82 zimetajwa pamoja na kwenda baharini mtoto, sasa nataka atufafanuliwe hiyo inakusudiwa mtoto akienda baharini peke yake au akienda na mzazi wake? Kwa sababu hizi kazi nyingine ambazo zinatajwa hatarishi labda kwa mtu ambaye hajui bahari, lakini kwa sisi watu wa Pwani kwenda baharini na mtoto wako si kazi hatarishi na ndiyo mtoto anapata kujua, vinginevyo huyu mtoto hataweza kujua hiyo ambayo baada ya mzazi kuondoka mtoto anatakiwa awe anaifahamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufafanuzi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri ufafanuzi!

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mimi naamini Mheshimiwa Mbunge kama mtoto amekwenda baharini kutembea au kuvua maana yake hatukuambiwa amekwenda kufanya nini. Kama umekwenda naye kwa ajili ya burudani sawa, lakini kama anakwenda baharini kwa ajili ya kuvua si salama.

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, anakwenda baharini anafuatana na mzazi, mzazi yuko kwenye chombo katika nia ya kumfundisha kazi, kwa hiyo na wewe mzazi unajua kuogolea na linalotokea lolote anakuwa yuko katika ngao na ana mlinzi. Kwa hiyo, ndipo ninapozungumzia mimi hapa.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nifafanue kama ifuatavyo:-

Kwenye hiki kifungu cha 77 kinachozungumzia masuala ya ajira ya watoto ya kazi nyepesi kuna kipengele kinachoruhusu mtoto wa miaka 14 kupata mafunzo sasa kama unamchukua kwa ajili ya kupata mafunzo naamini atakuwa chini ya uangalizi wako, lakini si chini ya miaka 14. *(Makofi)*

*(Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 83

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 84

Kifungu cha 85

Kifungu cha 86

Kifungu cha 87

Kifungu cha 88

Kifungu cha 89

Kifungu cha 90

Kifungu cha 91

Kifungu cha 92

Kifungu cha 93

*(Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 94

Kifungu cha 95

*(Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 96

Kifungu cha 97

Kifungu cha 98

*(Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 99

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 100  
Kifungu cha 101  
Kifungu cha 102  
Kifungu cha 103  
Kifungu cha 104  
Kifungu cha 105  
Kifungu cha 106  
Kifungu cha 107  
Kifungu cha 108  
Kifungu cha 109  
Kifungu cha 110  
Kifungu cha 111  
Kifungu cha 112

*(Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 113

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 114  
Kifungu cha 115  
Kifungu cha 116  
Kifungu cha 117  
Kifungu cha 118  
Kifungu cha 119  
Kifungu cha 120

*(Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 121

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 122

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 123

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 124

Kifungu cha 125

Kifungu cha 126

Kifungu cha 127

Kifungu cha 128

*(Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 129

Kifungu cha 130

*(Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 131

Kifungu cha 132

Kifungu cha 133

*(Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 134

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 135

Kifungu cha 136

*(Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 137

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 138  
Kifungu cha 139

*(Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 140

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 141  
Kifungu cha 142  
Kifungu cha 143  
Kifungu cha 144  
Kifungu cha 145

*(Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 146  
Kifungu cha 147

*(Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 148  
Kifungu cha 149  
Kifungu cha 150  
Kifungu cha 151  
Kifungu cha 152  
Kifungu cha 153

*(Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

ngu cha 154  
Kifungu cha 155  
Kifungu cha 156  
Kifungu cha 157

*(Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifu

Kifungu kipyaa cha 158  
Kifungu kipyaa cha 159

*(Vifungu vipya vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 160

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 161  
Kifungu cha 162  
Kifungu cha 163  
Kifungu cha 164  
Kifungu cha 165  
Kifungu cha 166  
Kifungu cha 167  
Kifungu cha 168  
Kifungu cha 169  
Kifungu cha 170  
Kifungu cha 171  
Kifungu cha 172  
Kifungu cha 173  
Kifungu cha 174

*(Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 175  
Kifungu cha 176  
Kifungu cha 177  
Kifungu cha 178  
Kifungu cha 179  
Kifungu cha 180  
Kifungu cha 181  
Kifungu cha 182  
Kifungu cha 183  
Kifungu cha 184  
Kifungu cha 185  
Kifungu cha 186  
Kifungu cha 187  
Kifungu cha 188  
Kifungu cha 189  
Kifungu cha 190  
Kifungu cha 191



Kifungu cha 192  
Kifungu cha 193  
Kifungu cha 194

*(Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Jedwali

*(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**(Muswada wa Sheria ya Mtoto wa Mwaka 2009  
(The Law of the Child Act, 2009)**

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imepitia Muswada wa Sheria uitwao *The Law of the Child Act, 2009* pamoja na mabadiliko yake kifungu kwa kifungu na kuukubali. Hivyo basi naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa *The Law of the Child Act 2009* sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki!  
*(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa  
Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**MWENYEKITI:** Nashukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kutoa hoja na hoja hii imeungwa mkono sasa taratibu zinanitaka niwahoji Waheshimiwa Wabunge kuhusiana na hoja iliyotolewa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa jinsi hiyo Bunge limemaliza taratibu zake zote.  
*(Makofi)*

*(Muswada wa Sheria ya Mtoto wa Mwaka 2009  
(The Law of the Child Act, 2009)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusoma mara ya tatu ndiyo tumekamilisha hatua zote ndani ya Bunge hili kwa hiyo, taratibu nyingine zitafuata ambapo ni Muswada huu kwenda mbele ya Mheshimiwa Rais ili kupata baraka zake ili iweze kuwa Sheria kamili na kama hilo likitendeka tunawatakia kila la kheri Wizara zote zinazohusika na Sheria hii ya mtoto jambo ambalo ni jema kwa watoto wote wa nchi yetu ya Tanzania. Tunakupongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa mara nyingine kwa Sheria hii. *(Makofi)*

Nina matangazo mawili, moja ni kuwakumbusha Wajumbe wa Kamati ya Uongozi ya Bunge kukutana Ukumbi wa Spika kwani kuna kikao pale na Mheshimiwa Spika.

Tangazo la pili linatoka kwa Mheshimiwa Hassan Rajab Khatibu ambaye ni Katibu Msaidizi wa Kamati ya Waheshimiwa Wabunge wote wa CCM, anasema taarifa ya kikao leo tarehe 4 Novemba, 2009 na taarifa hii inatolewa na Katibu ambaye ni Mheshimiwa Ali Ameir Mohamed kuwa kile kikao cha Kamati ya Wabunge wote wa CCM na Kamati teule ya Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM kitaendelea leo saa 11.00 jioni katika Ukumbi wa Pius Msekwa, ni muhimu kuhudhuria na ni muhimu kuwahi. Kidumu Chama cha Mapinduzi! *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Kidumu!

**MWENYEKITI:** Ndivyo tangazo lilivyoandikwa. *(Kicheko/ Makofi)*

Baada ya matangazo hayo mawili, naomba sasa kwa sababu muda wetu umefika mahali pa kuahirisha shughuli zetu, nawashukuru sana kwa ushirikiano mlionipa asubuhi hii ya leo kwa kazi hii iliyokuwa mbele yetu na mnajua kama kazi inakuwa ngumu kama mchezaji unacheza mbele ya kocha sasa leo Spika alikuwepo ananiangalia hapa ndiyo maana wakati mwingine nilibabaika kidogo. *(Kicheko)*

Basi kwa maneno hayo naomba niahirishe shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 12:55 mchana Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Alhamisi,  
Tarehe 5 Novemba, 2009 saa 3.00 asubuhi)*